ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge

10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya

		Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo,

		Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Saba - Tarehe 18 Mei, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kama ambavyo nilifanya jana na leo pia naendelea kwa mujibu wa marekebisho ya Kanuni zetu za Baraza la Wawakilihi tuliyoyafanya mwishoni mwa 2016, Kanuni ya 40(4) inahitaji maswali ya nyongeza yanayojibiwa kwa maandishi yawasilishwe mbele ya Baraza kupitia Taarifa ya Spika.

Madhumuni ya Kanuni hii ni kuwawezesha wananchi kufahamu majibu ya maswali hayo yanayoulizwa kwa niaba ya wananchi wanaowakilishwa kwenye chombo hiki.

Waheshimiwa Wajumbe Katika kikao cha Baraza cha tarehe 10 Mei, 2017 Mhe. Zulfa Mmaka Omar aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Fedha na Mipango na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi.

Katika kutimiza masharti ya Kanuni hiyo ya 40(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, Wizara hiyo imeleta majibu kama Waziri wa Wizara hiyo alivyoahidi.

Waheshimiwa Wajumbe napenda kuwasomea majibu hayo kwenu Waheshimiwa Wajumbe na kwa wananchi wote kwa ujumla.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar alitaka kujua kiasi cha fedha ambazo serikali inamdai mwekezaji wa Mpapindi na jibu kwa swali hilo ni kama ifuatavyo:-

“Kwa mujibu wa kumbukumbu tulizonazo mpaka mwaka 2012, mwekezaji anatakiwa alipe Dola 279,900 ambazo kati ya hizo kodi ya ardhi ni Dola 55,380 na adhabu ya kutolipa kodi hiyo ni Dola 221,550.

Waheshimiwa Wajumbe mwekezaji baada ya kupata changamoto za kibiashara zilizosababishwa na mbia wake kutaka kuuza ardhi baada ya kuwekeza, amekuwa katika mashauri kwenye ngazi mbali mbali za Mahakama hadi kufikia Mahakama ya Rufaa ya Tanzania, ambapo mwaka 2016 shauri lake lilipata hukumu.

Katika kipindi chote ambapo shauri hili lilikuwa Mahakamani na katika kuheshimu taratibu za utawala wa kisheria, serikali imekuwa ikisubiri maamuzi ya Mahakama ndipo iweze kuchukua hatua nyengine. Hivi sasa mwekezaji amewasiliana na Wizara ya Ardhi kuweza kujua jambo gani linaloweza kufanyika".

Aidha, Mhe. Zulfa alitaka kujua Serikali ina mpango gani wa kufuta '*lease'* ya mwekezaji huyo ili aweze kupatiwa mwekezaji mwengine na majibu ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

"Katika mazingira niliyoyaeleza hapo juu serikali haikuwa na uwezo wa kufuta mradi wala mkataba wa ardhi mpaka Mahakama ikamilishe hukumu yake".

Nawashukuru sana Waheshimiwa. (*Makofi*)

HATI ZA KUWASILISHA BARAZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe**.** Spika**,** naomba kuwasilishia mezaji Hotuba ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya (AR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2017.2018.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Wanu Hadhi Ameir (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezaji Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Shaibu Said Ali (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC): Mhe. Spika, kwa niaba ya

Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*, naomba kuwaka hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*PAC*) Kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mwaka 2017/2018.

Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 152

Utumiaji wa Ofisi ya Mchapaji Mkuu wa Serikali

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:**

Pamoja na kauli nzuri inayotolewa na Serikali ya Mapinduzi juu ya kuzitaka Taasisi zake zote kutumia Ofisi ya Mchapaji Mkuu wa Serikali katika kazi zake zote zinazohusu uchapaji lakini kumekuwepo muitikio mdogo kwa hili.

(a) Je Serikali imechukua hatua gani za kisheria kupitia taasisi hizo ambazo bado hazijatii amri hiyo.

(b) Kwa nini ahadi za Serikali hazitekelezwi na taasisi hizo kwa kutotii amri halali za Serikali kwa kutochapisha kazi zao katika Taasisi yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 152 lenye vifungu (a) na (b) naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, katika jitihada za kuimarisha huduma za uchapishaji, serikali imebadilisha mfumo wa uendeshaji wa Kiwanda cha Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kukifanya kuwa Wakala wa Uchapishaji wa Serikali ambao unasimamiwa na Bodi ya Ushauri katika kutekeleza kazi za kila siku.

Aidha kumefungwa mitambo 25 ya kisasa ya uchapishaji. Baada ya juhudi hizo za kukiimarisha kiwanda, sasa Wakala wa Serikali wa Upigaji Chapa anau wezo wa kuchapisha kwa ubora wa hali ya juu machapisho mbali mbali

yakiwemo Gazeti rasmi la Serikali, Miswada ya Sheria, Sheria, vitabu vya Bajeti za Serikali, Mitihani, na machapisho mengine yanayowasilishwa kiwandani kwa mujibu wa mahitaji ya taasisi husika na watu binafsi.

Aidha, kuanzia tarehe 10/05/2017 Wakala ameanza rasmi kuchapisha Gageti la Zanzibar Leo ambapo hapo kabla lilikuwa likichapishwa Tanzania Bara.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo tunaomba kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 152 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, Serikali imetoa toleo maalum kwa kuzitaka Taasisi na Mashirika yote ya Serikali kupeleka kazi zake za uchapishaji katika Wakala wa Serikali wa Uchapaji. Aidha, kama itatokea Taasisi au Shirika lolote la Serikali kwenda kinyume na agizo hilo ataripotiwa kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kwa kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

(b) Mhe. Spika, kwa hivi sasa taasisi zote zinatekeleza agizo hilo la serikali kwa kupeleka kazi zao zinazohusu uchapaji kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumuomba Mhe. Mwakilishi kama ana taarifa zozote kwa taasisi ya serikali ambayo haitekelezi agizo hili la serikali, basi anatakiwa atoe taarifa kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu KIongozi au Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili kuweza kuchukuliwa zinazostahiki.

Nashukuru Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii tena. Nataka nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini naomba kumuuliza swali la nyongeza.

(a) Mhe. Spika, Waswahili wanasema "Bora hatma", niwaulize kama kiwanda hichi ndio kimeanza kwa kasi lakini kimejipangaje kuingia katika ushindani na viwanda vyengine isije ikawa tumeingi lakini ikaja kuwa mlango tunaoingilia ndio tunaotokea.

(b) Mhe. Spika, humu alieleza ana uwezo wa kuchapisha mpaka mitihani. Je, anaweza kutusaidia mitihani yetu ya Zanzibar kuchapisha bure ili kusaidia serikali katika Wizara ya Elimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kumjibu swali lake Mhe. Suleiman Sarahan kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, nimuhakikishie Mjumbe kwamba kiwanda kimejidhatiti na kimejipanga vyema kukabiliana na kujitangaza vya kutosha kama vile ambavyo tayari kimeshakuwa kukijitangaza hata katika maeneo ya Tanzania Bara na mpaka hivi sasa kiwanda chetu cha Wakala wa Uchapaji Zanzibar kina mahusiano mazuri na Taasisi ya Uchapaji wa Tanzania Bara ambayo kwa makubaliano ya awali wamekubaliana sasa kuanza kupeana kazi kwa wale wenzetu wa Tanzania Bara ambao wapo chini ya Afisi ya Waziri Mkuu pale ambapo watakuwa na ongezeko kubwa la kazi watakuwa tayari kuweza kuzihamishia katika Wakala wetu wa Uchapaji.

(b) Mhe. Spika, swali lake la pili naomba arudie kidogo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa naomba lirudie kidogo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mhe. Spika, nazungumzia kwamba kwa sababu alipojibu alisema ana uwezo mpaka wa kuchapisha mitihani. Kwa hivyo nilikuwa nazungumza kwamba kwa sababu ni kiwanda cha serikali na Wizara ya Elimu kama elimu bure, anaweza akatusaidia kuchapisha mitihani bure kwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, tayari kiwanda kilishaanza kuchapisha mitihani kwa ajili ya vijana wetu kwa kushirikiana na Wizara husika ya Elimu. Suala la kuchapisha mitihani bure ama kwa kulipia hilo ni jambo la serikali, tukipata muongozo wa serikali kupata muongozo wa serikali kuchapisha bure tutafanya hivyo kama kiwanda, kiwanda kipi chini ya serikali na kiwanda bado kinaendelea kufata miongozo ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, ingawa sasa kiwanda kinajiendesha chenyewe kwa kuendeshwa na Bodi yake kama Wakala wa Uchapishaji, hivyo iwe Taasisi ya Serikiali, iwe mtu binafsi anawajibika kwenda kulipa katika lile toleo analohitaji kuchapishwa.

Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana na nimpongeze Mchapati wa Serikali kwa kazi nzuri anayoifanya hususan kuchapisha Gazeti letu la Zanzibar leo hapa Zanzibar.

Lakini mara tu baada ya tarehe 10/05/2017 kuchapishwa gazeti lile limetokea uhaba wa uingizaji wa bidhaa ya Gazeti la Zanzibar leo kutumika Tanzania Bara kwa wakati. Kwa sababu Gazeti la Zanzibar lakini kuna ufinyu wa usafiri wa usiku ule au alfajiri saa moja magazeti kufika katika Mikoa yetu kama Dodoma, Tanga na Dar es Salam.

Je, serikali yako imejipangaje kuona kama ilivyokuwa magazeti yanachapishwa Tanzania Bara saa mbili yamefika Zanzibar na magazeti yanatoka Zanzibar yatafika Bara kwa wakati gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza tukubaliane fika na changamoto ambayo ametuwasilishia na sisi kama wizara tunakiri ipo changamoto ya kiutendaji ambayo imekuwa ikitukabili kutokana na mazingira stahiki ya jiografia ya visiwa vyetu. Kawaida utaratibu wa magazeti mengi duniani yanakuwa yanaandaliwa katika nyakati za usiku. Lakini ukitizama kuda wa usiku si muda rafiki sana au hatuna vyombo madhubuti vya kuweza ku-*transfer* magazeti kutoka Unguja kwenda Tanzania Bara.

Mhe. Spika, lakini *concerning* yake tumeifahamu na sisi kama Wizara na serikali tayari tunatizama namna ambavyo tunaweza tukachapisha magazeti yetu haya, lakini yakenda kuingia katika *chain* nzuri ili Walaka anayesambaza magazeti yale katika Tanzania nzima ili kuweza kuwahakikishia uhai wa kiwanda chetu na kuweza kuwahakikishia wateja ambao wamekuwa wakisoma Gazeti la Zanzibar Leo ndani ya Tanzania kwa ujumla. Nakushuru Mhe. Spika.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Ahsante sana Mhe. Spika, wa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na mimi naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye kitoto (a) na (b).

Mhe. Spika, kwa kuwa katika majibu yake amekiri kwamba wamefunga mitambo mipya.

(a) Ni utaratibu gani uliotumika wa kutafuta mzabuni wa kununulia mitambo hiyo na je, nani alishinda tenda hiyo.

(b) Lakini ni gharama kiasi gani wizara yake imetumia katika kufunga mitambo hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hamida Abdalla Issa maswali yake mawili kama hivi ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, niseme tu kama ambayo utaratibu wa kizabuni ambavyo umekuwa ukitolewa. Kwanza kiwanda kilitangaza tenda bahati nzuri akatoke mtu aliyestahiki, lakini sote tufahamu kwamba mashine hizi nyengine ambazo tunazo tulipokea mchango na msaada kutoka kwa wenzetu wa Oman ambao waliamua fika kutusaidia mitambo hii ili kuweza kuleta uhai baada ya serikali kuwaomba wenzetu.

(b) Lakini hili la gharama kiasi gani zimetumika Mhe. Spika, naomba uniachie swali hili nitamjibu Mhe. Mjumbe na tutaliarifu Baraza lako rasmi kiasi gani kimetumika kwa gharama nzima ya kiwanda kile.

Nam. 81

Hatua za Kisheria kwa wanaochafua heshima ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:**

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waislamu wote Tanzania naomba suala langu 81 lipate jawabu na ukizingatia si muda mrefu panapo majaliwa tunategemea kupata mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Kwa miaka mingi Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwachukulia hatua baadhi ya watu wanaochafua heshima ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani kama wale wanaokula hadharani, wanaolewa hadharani, wanaovaa nguo zisizo na heshima n.k

Je, Serikali imejipanga vipi katika mwezi wa Ramadhani kuendelea na utaratibu huu mzuri ambao Wazanzibar wengi tunaunga mkono ili heshima ya mwezi Mtukufu iendelee kubakia Zanzibar na ule utamaduni wa watu kutoka

sehemu mbali mbali za dunia kuja kufunga Zanzibar uendelee kuipa heshima kubwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:**

Mhe. Spika**,** kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikichukua hatua mbali mbali katika kuhakikisha kwamba heshma na hadhi ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhan inalindwa na kudumu kabla na baada ya mwezi huo kama tunavyolinda heshima ya shughuli za Dini nyengine. Hatua hizi zimesaidia sana katika kulinda utamaduni wetu na kuwafanya watu wa sehemu mbali mbali za dunia kuja kutekeleza ibada ya funga hapa Zanzibar .

Mhe. Spika, miongoni mwa hatua ambazo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepanga kuchukua kwa kupitia Afisi ya Mufti ni pamoja na kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuheshimu Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Aidha kupitia Ofisi ya Mufti Maimamu wote wa Misikiti ya Ijumaa watasisitizwa kupitia hutuba zao za sala za Ijumaa, kuwakumbusha Waumini juu ya umuhimu wa kuupa heshima mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Mbali ya hatua hizo, Ofisi ya Mufti huandaa vipindi maalum vya redio na televisheni vitakavyozungumzia juu ya umuhimu wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Spika, Mufti Mkuu wa Zanzibar pia ana utaratibu wa kutoa tamko rasmi la kuukaribisha mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Tamko hili pamoja na mambo mengine litahimiza na kuwakumbusha Waumini na wananchi kwa jumla kujiepusha na matendo yote yatakayopelekea kuuvunjia heshima mwezi huu. Kama vile kula ovyo mabarabarani, kuvuta sigara, kutovaa vivazi vye heshima na kadhalika. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nashukuru kwa kuwa umekalia mwenyewe kiti hii leo na mimi nitahitaji muongozo wa kiti chako. Alituambia Mhe. Rais na wewe mwenyewe ni shahidi, maswali tunayouliza wananchi ni ya wananchi. Lakini hapa nilichouliza sicho nilichojibiwa.

Nataka muongozo wa kiti chako, nilichouliza sicho nilichojibiwa, iangalie *order paper* na jawabu lake. Mawaziri na Manaibu Waziri hawajaribu

kufuatilia hicho wanachoulizwa, na huu ndio ukweli ulivyo. Mimi nimeuliza hatua nakuja kujibiwa kitu chengine.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku naomba uulize swali la nyongeza. Wewe unadai ulichouliza sicho ulichojibiwa. Maana yake umeuliza swali la majibu ambayo unayafahamu unaitega serikali. Naomba usibishane na kiti Mhe. Jaku. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, swali la msingi kwa miaka mingi serikali imekuwa na utaratibu wa kuwachukulia hatua baadhi ya watu wanaochafua heshima ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kama wale wanaokula hadharani na wanaolewa hadharani na wanaovaa nguo zisizo sahihi. Nilikuwa nataka jawabu la swali hili.

Mhe. Spika: Naomba ulize swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, utakuwa hunifanyii haki lakini tuendelee.

a) Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi amesema kuendelea kutoa elimu ya umuhimu. Sasa bado elimu hiyo na Ramadhani inakaribia na elimu hiyo haijatolewa. Ni lini itatolewa elimu hiyo.

b) Je, Mhe. Naibu Waziri ndugu yangu na pindipo nikianguka wewe ndio utanichukua hapa kwenda kunizika kuliko mtu mwengine yeyote. Watu wanaovaa nguo fupi, wanaovuta sigara hadharani hapo nyuma katika mwezi mtukufu wa Ramadhani walikuwa wakichukuliwa na kufunguliwa kesi. Je, utaratibu huu utaendelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, nilivyoeleza katika jibu mama kwamba serikali imekuwa ikifanya jitihada za makusudi kupitia Ofisi ya Mufti kutoa elimu pamoja na mambo mengine kutoa elimu inayohusiana na suala zima la mwezi wa Ramadhani. Kwa hivyo elimu imekuwa ikitolewa kupitia vyombo vya habari kama televisheni, redio na kadhalika.

Vile vile na wakati mwengine huwa wanapita baadhi ya Wilaya kutoa elimu hiyo. Kwa hivyo Mhe. Spika, elimu inatolewa na itaendelea kutolewa.

Kubwa zaidi tunasema elimu inatolewa na tutasisitiza zaidi elimu hiyo kutolewa kama ni ukumbusho kwa sababu mwezi wa Ramadhani umekaribia. Kwa hivyo elimu imeanza kutolewa na itaendelea kutolewa kama kawaida.

(b) Mhe. Spika, kuhusiana na suala la watu ambao mavazi yao hayaridhishi. Mavazi ambayo hayaridhishi huu sio utamaduni wetu wa Kizanzibari, kufanya hivi inakwenda kinyume na silka za utamaduni wetu wa Kizanzibari pamoja na Dini zetu zote. Sasa niseme tu kwamba kufanya vitendo hivi sio vya kiungwana ni vyema wananchi tukaviepuka, Dini zetu hazitaki hivyo. Kwa hivyo nitoe wito kwa wananchi kwamba sio mwezi mtukufu wa Ramadhani ni miezi yote. Tuendelee kujiheshimu, tuendelee kuzifuata Dini zetu kama ambavyo zinavyotuelekeza kujilinda au kuvaa mavazi mazuri ili kujilinda kama Dini zetu zinavyotuelekeza.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba na mimi nimuulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa yeye mwenyewe amekiri kwamba mila na utamaduni wetu unatuhimiza na hata Dini zetu zinatuhimiza kuweza kuvaa vizuri ili tuweze kuonekana katika muonekano mzuri na kwa kuwa mwezi mtukufu wa Ramadhani unakuja na huja kutufunza kuondosha mabaya na tuyaendeleze mema. Hapa katika sheria ya mavazi inaonekana ina mapungufu na bado hatujaileta Barazani kuja kuifanyia marekebisho.

Je, Mhe. Naibu Waziri ni lini sheria hii italetwa Barazani ili sasa tuweze kupata yale mavazi mazuri yanayolindwa na sheria ili utamaduni wetu tuweze kuulinda. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Naomba ajibu Mhe. Waziri nakuona.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Nimewafahamu waheshimiwa, sheria zote ambazo zina kasoro ni wajibu wetu kuzirekebisha na kuna Tume Maalum ya Kurekebisha Sheria.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni Mhe. Mwanasheria Mkuu alifanya kazi moja kubwa sana, sekta zote aliziandikia barua na taarifa kwamba sheria gani ambazo ziko chini ya wizara zao na sekta zao. Kwa hivyo waziangalie ikiwa pamoja na Sheria hii waziangalie, kama zina kasoro basi zifanyiwe utaratibu

wa kuzirekebisha na sisi hatuna matatizo sekta inayohusika itayarishe marekebisho hayo na hatimaye italetwa hapa Barazani kwa marekebisho ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza mimi niipongeze serikali kwa dhati kabisa kwa kuhakikisha kwamba mwezi wa Ramadhani unakuwa ni mwezi mtukufu na unaheshimiwa na kila mtu. Lakini swali langu liko hapa.

Mhe. Spika, kwa kuwa nchi yetu inapokea wageni watalii kutoka sehemu mbali mbali duniani, na mara nyingi huwa wako huru kula wanachotaka, lakini kwa kuwa tumewawekea mipaka. Je, ni mahoteli gani yametayarishwa ili kuhakikisha kwamba huko wanakwenda bila ya tatizo na hawatopata athari yoyote ya kushikwashikwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, wageni wetu wanapoingia nchini mara nyingi kabla ya kuingia nchini huwa wanapata taarifa kupitia wakala wao wale ambao wanawaleta nchini kwamba sehemu ambayo mnakwenda kipindi hiki kuna mwezi mtukufu wa Ramadhani. Kwa hivyo ni vyema zaidi, na sio kwa mwezi mtukufu tu wa Ramadhani hata miezi yote ni vyema kujisitiri.

Kwa hivyo taarifa wanazipata kabla ya kuja nchini kwetu na hiyo kushikwashikwa haitaweza kutokezea, kwa sababu taarifa wanazipata kupitia wakala wao ambao wanaowaleta hapa nchini. *(Makofi)*

Nam. 11

Mikakati ya Kuhifadhi Kiwanja cha Amani

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:-

Kwanza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa dhamira sahihi ya kuendeleza michezo Zanzibar na kuhakikisha kuwa michezo mbali mbali inachezwa hapa petu, kama vile kuhakikisha Uwanja wa Amani unawekewa nyasi bandia.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha uwanja ule unapata mahitaji yake yanayohitajika.

(b) Je, kuna tahadhari yoyote iliyochukuliwa katika uwanja ule ukitilia maanani kuwa nyasi za plastiki zinaweza kuwaka kukitupwa kipande cha sigara na mashabiki.

(c) Je, kuna vifaa gani vya kuzima moto katika uwanja huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar napokea pongezi zilizotolewa na Mhe. Mwakilishi kutokana na dhamira sahihi ya Serikali kuendeleza michezo Zanzibar na kuhakikisha kuwa michezo mbali mbali inachezwa nchini petu na kuhakikisha miundombinu ya Uwanja wa Amaan inaendelezwa kwa kutiwa nyasi bandia.

(a) Mhe. Spika, wizara tayari imepanga kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazokabili Uwanja wa Amaan ikiwemo kutenga fedha katika bajeti ya mwaka 2017/18 kwa ajili ya kutatua tatizo la upungufu wa vipira (*rubber granule*) na matengenezo mengine ya kiwanja hicho.

(b) Mhe. Spika, kwa kutilia maanani kuwa nyasi za Uwanja wa Amaan ni za *plastic* na wakati wowote zinaweza kuwaka moto kutokana na mashabiki kutupa vipande vya sigara, tahadhari imechukuliwa kwa kutoa elimu kwa mashabiki na watumiaji wa uwanja kwa kuweka *poster* za matangazo kukemea uvutaji wa sigara kwenye majukwaa ya watazamaji. Sambamba na kushirikiana na Taasisi ya Zimamoto na Uokozi kutoa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya kuitumia mitungi ya gesi ya kuzimia moto.

(c) Mhe. Spika, mitungi ya gesi ya kuzimia moto ipo lakini kwa kushirikiana na Idara ya Zimamoto na Uokozi itazidi kuhakikisha kuwa inafanyakazi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nauliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu yake aliyosema kwamba mitungi ya gesi ipo lakini atahakikisha inafanyakazi.

(a) Nataka aniambie mitungi hiyo ya gesi iko mingapi katika Uwanja huo wa Amaan.

(b) Pamoja na dhana nzuri ya kutayarisha ununuzi wa *rubber granule*, ule uwanja una zaidi ya miaka saba na taratibu zake kila baada ya miezi mitatu unapotumika uwanja ule unataka uparwe na kutiwa vile vipira kurudishwa katika ubora wake. Je, kuchelewa kwenu huko hamuoni kuwa hamuutendei haki ule uwanja na kusababisha kwamba kuharibika katika sifa yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika. kwa idhini yako naomba nimjibu swali lake la nyongeza Mhe. Abdalla Maulidi Diwani lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu mama kwamba ipo mitungi hii ya gesi ya kuzimia moto katika Uwanja huu wa Amaan. Mitungi ipo jumla ya mitungi 30, kati ya mitungi hii ipo mitungi 18 ambayo inafanyakazi. Lakini Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mjumbe kwamba sasa hivi tayari mitungi hii tumeshaipeleka katika Kikosi chetu cha Zimamoto ili kufanyiwa matengenezo na mitungi hii iendelee kufanyakazi kama kawaida ili kuepusha yale majanga ambayo yatatokea pale.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mjumbe swali la (b) alirejee.

Mhe. Spika: Mhe. Diwani swali (b) lirudie kidogo alisikie.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Swali (b) nimeuliza pamoja na dhamira nzuri ya kujiandaa na ununuzi wa hizi *rubber granule* kwa ajili ya *granule* kwa ajili ya kutia kwenye uwanja kurudisha katika ubora wake. Ni miaka zaidi ya saba uwanja ule umetengenezwa na unatumika haujawahi kuwekwa *rubber granule*.

Je, hamuoni kwamba ndio mnasababisha kutoutendea haki ule uwanja kwa sababu itakuwa kila baada ya miezi mitatu unapotumika vipatikane vile vifaa kwa kuweka katika ubora wake uwanja ule.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika.

(b) Mhe. Spika, napenda nikiri kwamba ni miaka saba tayari kiwanja hiki bado hakijawekewa vipira vipya. Naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba uwanja huu tunautendea haki kwani serikali nia yake ni kuona kwamba uwanja unafanyakazi na wananchi wake wanacheza mpira kwa kupitia kiwanja kile.

Lakini Mhe. Spika, namuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba sasa hivi kama nilivyojibu katika swali langu mwanzo, tayari tumeshatenga bajeti ya kununulia vipira hivi na tumeshafanya *contract* ya wahusika ambao wanatengeneza vipira hivi na sio muda mrefu Inshaallah ataona tayari tumevitia na uwanja unafanyakazi. *(Makofi).*

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi nafasi hii kuweza kuuliza swali moja dogo sana la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri. Kwanza nimpongeze kwa majibu mazuri sana ya maswali mama ambayo anaulizwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kuwa nchi yetu tayari hivi sasa imejiunga au imepata uwanachama katika Shirikisho la mchezo wa Kandanda la *CAF*, ambayo kwa mujibu wa taratibu za Kimataifa lazima iwe na viwanja ambavyo vina hadhi inayokubalika na ni ukweli kwamba nyasi za Uwanja wa Amaan tayari zimeanza kuchoka. Nimuulize Mhe. Naibu Waziri.

Je, nyasi hizi zilitiwa mwaka gani na lini tunatarajia kuweza kubadilisha nyasi hizo ili tuendane na vile viwango vya viwanja vya kimataifa. Ahsante sana

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Rashidi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, nakiri kwamba sasa hivi tumeingia katika michezo ya kimataifa kwa kupata uwanachama wa *CAF* na hili naomba nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, lakini pia nimpongeze na Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo pamoja na watendaji wake, kwa kusimamia hili mpaka tukapata uwanachama wa *CAF*.

Pia Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba kwa kuwa suala hili ametaka kujua ni mwaka gani vimetiwa hivi vipira, naomba nimjibu kwa jibu la maandishi.

Mhe. Ali Khamis Bakar : Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake sahihi ambayo ametuletea. Baada ya hayo naomba kumuuza swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Ili kukuza suala la michezo kuna timu za mpira wa miguu za vijana majimboni ambazo zimeanzishwa. Je, wizara yake ina mpango gani wa kuzisaidia timu hizo.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe swali la msingi linahusu Uwanja wa Amaan. Mhe. Suleiman Makame Ali kwa swali la nyongeza.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba swali la msingi ni Uwanja wa Amaani lakini naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba Uwanja wa Gombani hauwaki taa hadi leo hii.

Je, ni lini uwanja ule nao utawaka taa ili kufanana kama na Uwanja wa Amani ili vijana wetu kuweza kucheza mpira wakati wa usiku kule Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana. Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Suleimani Makame Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, nakiri kwamba uwanja ule hauwaki taa kwa nyakati za usiku Uwanja wa Gombani Pemba.

Mhe. Spika, namuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba nalichukua suala lake na tutalifanyia kazi na tuone kwamba tumefanya jitihada zote ili tuone kwamba uwanja ule unawaka taa kama Uwanja wa Amaan na vijana wetu waweze kushiriki kucheza usiku. Ahsante. *(Makofi)*

Nam. 140

Kukifufua Kiwanda cha Makuta Buyu:

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Aliuliza:

Kwa kuwa Serikali ina mipango ya kufufua viwanda vilivyokufa kwa muda mrefu ili vifanye kazi. Na kwa kuwa katika eneo la jimbo la Chukwani

kulikuwa na kiwanda cha makuta maeneo ya Buyu, ambacho kilikuwepo katika kipindi cha awamu ya tano kilichoongozwa na Rais Mstaafu Salmin Amour Juma.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukifufua kiwanda kile baada ya kuwepo gofu tu ambalo halina tija kwa nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Ikulu (Kny. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 140 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba kiwanda cha Makuta cha Buyu kimegeuka gofu baada ya mradi huo kufungwa rasmi. Mitambo yote ya kiwanda imeshaondolewa kiwandani baada ya wamiliki wa mradi kuamua kuufunga.

Mhe. Spika, naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wawakilishi kuwa katika miaka ya thamanini hadi ya miaka tisini, Serikali ilifanya maamuzi ya makusudi kujiondoa katika shuhguli za uzalishaji na za biashara na kufungua milango ya fursa kwa sekta binafsi kuekeza katika sekta kama hizo za ujenzi na biashara.

Mhe. Spika, Serikali itaendelea kujikita katika uwekaji wa mazingira bora na rafiki ya uwekezaji wa miradi ya sekta binafsi, ikiwemo miradi mipya ya viwanda au kufufua viwanda vya zamani ikiwemo ya Kiwanda cha Makuta cha Buyu.

Aidha, Wizara Biashara, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na *ZIPA* itaendelea na jitihada za kutangaza fursa za uwekezaji katika viwanda katika maeneo mbali mbali ikiwemo Kiwanda hiki cha Makuta, Kiwanda cha Soda, Kiwanda cha Kusarifu chumvi na Viwanda vya uzalishaji wa Samaki na viwanda vyengine vyote vinavyoweza kuongeza tija na uzalishaji mkubwa zaidi kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwa kuwa Waziri amekiri kufungwa kwa kiwanda hicho ni changamoto gani za uwekezaji zilizompata mwekezaji huyu mpaka kufungwa kiwanda hicho.

b) Kwa kuwa mradi huu ulisaidia sana ujenzi wa nyumba kwa ubora na haraka Serikali ina mpango gani mbadala wa kuendelea na huduma hii.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Ikulu (Kny: Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, kama ambavyo jibu mama nimeweza kueleza kwamba Serikali imejiondoa katika sekta hizi binafsi, lakini kama tutakumbuka vizuri mradi huu ni miongoni ya miradi ya kwanza wakati tunakwenda katika hatua za *privatizations,* miongoni mwa jambo ambalo mradi huu uliweza kuishirikisha Serikali pamoja na mwekezaji yeye mwenyewe binafsi na katika mradi huu kulikuwa kuna *component* ya Serikali kuweza kutoa ama mtaji au dhamana kwa ajili ya mwekezaji huyu kuweza kuwekeza.

Kwa hivyo kilichojitokeza kwamba mwekezaji aliishiwa na mtaji, alikwama kwa mujibu wa sheria za utafutaji wa fedha na Serikali baada ya kuona kwamba mradi wenyewe hauwezi kuishi vizuri na umeshindwa kukamilisha taratibu zote za uwekezaji. Kwa hivyo mradi huu ukawa umekufa.

b) Serikali tunaendelea kushajihisha sekta binafsi iweze kuwekeza katika hatua hizi za majenzi na majengo na tumeanza kuona muitikio mzuri. Kuna wawekezaji wamewekeza Fumba, kuna wawekezaji wamewekeza Nyamanzi, kuna wawekezaji ambao wa taasisi wanawekeza Mbweni. Kwa hivyo wajibu wetu kama Serikali kuendelea kuweka mazingira mazuri, mazingira rafiki ili kila mwenye uwezo, kila mwenye nia na dhamira ya kutaka kuja kuwekeza nchini kwetu aje kuwekeza, bado ipo fursa kubwa ya kutosha kuweza kuwekeza kwa wenzetu wanaotaka kuwekeza katika mfumo wa *reinstate.* Kwa hiviyo imani yetu kwamba wawekezaji wakijitokeza kwa wingi wananchi wataweza kupata huduma nzuri ya makazi bora na mazuri zaidi kwa mfumo wa ubia, au ushirikiano. Wao wenyewe wawekezaji pamoja na kushirikiana na Serikali lakini wajibu wetu kama Serikali tutahakikisha mazingira mazuri

yatakayomvutia kila muwekezaji kuwaza kuja kuwekeza nchini ili wananchi wetu waweze kupata huduma nzuri ya makazi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi ningependa nimuulize Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, kwa kuwa katika maeneo ambayo Serikali imewatenda maeneo huru ili kuweza kubadilisha au kueneza uchumi ni moja ya Micheweni Pemba. Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga au kuhamasisha watu kujenga viwanda ili kujenga *assembly plans* na kuunganisha bidhaa zetu soko la Kenya, Tanga pamoja na reli zitakazokuja kuelekea Congo.

b) Tumeona sasa mfumko wa viwanda vya kutengeneza maji au hizi *bottle track water* hapa Zanzibar ambapo sasa hivi viwanda vinazidi kuongezeka. Je, Serikali haina umuhimu wa kuwalinda hawa wenye viwanda vya kutengeneza maji ya chupa ili kuhakikisha kuwa maji yanayotoka Dar es Salaam hayaingii katika soko la huku, na kuhakikisha kwamba hawa wanaotengeneza maji katika viwanda hivi soko lao linabakia kuwa la kuweza kupata faida kwa biashara yao pamoja na utendaji wao.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Ikulu (Kny: Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, wajibu wa Serikali kwa kipindi chote tumeendelea kutangaza maeneo ya Micheweni, tumeendelea kutangaza maeneo ya Amani, tumeendelea kutangaza maeneo ya Fumba kama ni maeneo huru ya uwekezaji na tunaendelea kushajihisha hivyo kwamba kila mwenye dhamira, kila mwenye nia ya kutaka kuja kuwekeza Zanzibar, maeneo huru hayo yapo na tutaendelea kuwashijihisha watu wetu waedelee kuwekeza katika maeneo hayo. Ni kweli kwamba eneo la Micheweni tukipata mwekezaji ni eneo zuri kwa ajili ya ku-*assemble* bidhaa na inaweza ikawa rahisi kwa ajili ya kusafirisha kwenda Kenya na nchi nyengine kwa upande wa Kaskazini mwambao wa bara la Afrika.

Lakini sisi tunaendelea kuhimiza kwamba Serikali tumejitoa katika kuwekeza isipokuwa tunaendelea kutengeneza mazingira mazuri ya kuwavutia na kuwafurahisha wawekezaji waje wawekeze nchi, ili wananchi wetu waweze

kupata fursa za ajira, upatikanaji wa bidhaa kwa unafuu na huduma nyengine kama hizo.

b) Kuhusu mfumko wa Viwanda vya maji. Mhe. Spika, tunaangalia kwa pande zote mbili, *pros and cons*, unapotangaza biashara huria, maana yake unaruhusu ushindani. Serikali imeruhusu biashara huria na utitiri wa viwanda ili kuweza kupata uimarishaji wa huduma bora zaidi. Madhumuni yetu na malengo yetu, viwanda vyetu vya maji viliopo nchini tutavilinda kwa wao wenywe kutambua thamani na wajibu wao wa kukuza huduma zao, kukuza ubora wa bidhaa zao ili wananchi wavutiwe na bidhaa hizo. Hatuwezi tukawa Serikali ya kulinda kama bidhaa zao zitakuwa hazina viwango, kama bidhaa zao zitashindwa ushindani wa soko. Kwa hivyo wajibu wetu sisi tunahakikisha kwamba soko lipo, wao wazalishe bidhaa ambazo zitakuwa zinawavutia sokoni kama ambazo hizo zinatoka nje ya Zanzibar.

Kwa hivyo Serikali ni wajibu weu kutengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji lakini pia tunaendelea kuwashajihisha watu wetu wanaozalisha, wazalishe bidhaa ambazo zitaweza ushindani wa soko kwa kutambua kwamba sasa hivi tuna soko huria, kila mwenye bidhaa nzuri ndiye atakayepata manunuzi makubwa zaidi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mimi ningependa kujua Zanzibar tuna viwanda vingapi hivi sasa hivi vinafanya kazi na vingapi vimekufa ambavyo havifanyi kazi, na sababu zipi zilizofanya hivyo viwanda vilivyokuwa vikafungwa.

b) Kwa kuwa nchi nyingi zenye viwanda zinalalamika na *air pollution* na kemikali ambazo zinaleta *side effect* kwa wananchi na hapa Zanzibar tumeona kwamba viwanda vingi vinajengwa sehemu holela holeta. Kila sehemu mtu ananunua anajenga kiwanda , haijawekwa sehemu maalum ya kujenga viwanda. Ni lini sasa Serikali itaandaa maeneo maalum ya kujenga viwanda na zile sehemu ambazo zinaleta athari kwa wananchi zitaondoshwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Ikulu (Kny. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Suala hili linahitaji takwimu lakini pia kila kiwanda kinachofanya kazi ama kilichokufa kitakuwa kina mazingira yake. Kwa hivyo nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba tutampatia majibu kwa maandishi ya jumla ya viwanda ambavyo vinafanya kazi, lakini pia itakuwa ni vigumu kumwambia kwamba kila kiwanda hichi kimekufa kwa sababu hii, hichi kwa sababu hii na hichi kwa sababu hii, kwa sababu viwanda hivi vinaendesha na sekta binafsi na wao sekta binafsi siamini kama kutakuwa kuna matatizo ya *management* yao wenye watakuwa tayari kuyasema kwamba kiwanda chetu kimekufa kwa sababu ya uzembe wa uendeshaji. Kwa hivyo niwahakikishie tutampa takwimu za idadi ya viwanda kwa sababu ni wajibu weu kama Serikali kuvijua viwanda vyote vinavyowekezwa nchini. Lakini sababu za kufa kwa viwanda hatutokuwa nazo.

b) Mhe. Spika, maeneo ya uwekezaji wa viwanda Zanzibar yapo Maruhubi kama ilivyo Israel, kama ilivyo Ujerumani, kama ilivyo Uingereza. Maruhubi inajulikana wazi kama *Maruhubi Industrial Park*, tunayo *Amani Industrial Park*, maeneo ya uwekezaji Micheweni, *it is Industrial Park*, tunayo maeneo ya uwekezaji ni *Fumba Industrial Park.* Kwa hivyo maeneo haya yote ni maeneo ya uwekezaji wa viwanda. Lakini inategemea aina ya kiwanda yenyewe unayotaka kuwekeza. Kwa sababu upigaji wa matofali kwetu sisi pia ni kiwanda. Kwa hivyo upigaji wa matofali haumaanisihi kwamba lazima ukaweke Fumba ndio uweze kupiga matofali, utakapokuwa na fursa hata kama mtaani, ukawa na eneo litakalotosha Serikali itakusimamia, Serikali itakuongoza na kukupatia vibali vinavyostahiki ili uweze kuwekeza kiwanda chako.

Nam. 22

Tatizo la Maji Katika Shehia ya Kiuyu – Kigongoni

Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Aliuliza:

Wakati wa kipindi cha Bajeti ya mwaka 2016/2017 ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira nilichangia kuhusu tatizo la maji ambalo lipo katika Shehia ya Kiuyu – Kigongoni na mpaka leo hii tatizo hilo lipo linaendelea.

Je, ni lini Wizara yako italishughulikia tatizo hilo ili kuwaondoshea changamoto hii wanayoipata wananchi wa Shehia hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 kama ifuatavyo:-

Wizara yangu kupitia Mamlaka ya maji tayari imekwishalishughulikia tatizo la maji Kiuyu –Kigongoni kwa uendelezaji wa kisima kiliopo katika eneo la *Amani Road*, ujenzi wa kibanda cha kuendeshea pampu, ununuzi na uingizaji wa pampu, na kazi inayoendelea sasa ukamilishaji ulazaji bomba, upelekaji wa umeme, na ujenzi wa *wellhead*.

Naomba kumtoa wasi wasi Mhe. Mwakilishi pamoja na kuwaomba wananchi husika kuwa na subra na kwamba changamoto ya upatikanaji wa maji itamalizika mara tu baada ya kukamilika kazi zilizobakia.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza maswali mawili (a) na (b).

a) Je, Mhe. Waziri ni lini Wizara yako itatoa tamko rasmi kwa wananchi hao wa Shehia ya Kiuyu Kigongoni kuzuia huduma ya kulipia maji mpaka pale suala hili litakapopatiwa ufumbuzi.

b) Mhe. Waziri ni lini mpango huu utakamilika na hasa tukielekea katika kipindi hichi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kwa kuanza na (b) Kama nilivyokuwa nimesema baada ya kukamilika kazi iliyobakia na kimoja kama itatoka jua la muda wa siku mbili, leo tuseme na kesho kazi ya ujenzi wa *wellhead* pia itakuwa imemalizika, itakia kazi ya upelekaji wa umeme nayo inagharimu kiasi kama milioni nne, kama yupo tayari kukamatana mkono pamoja na Serikali inategemea yeye lini atasema labda nguvu zake zipo tutalimaliza punde.

a) Lakini hilo la kulipia maji kama hayapatikani maana yake hakuna sababu ya kuchangia, kama hilo lipo basi tutaliweka sawa *in shaa Allah*.
Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kuweza kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu mazuri uliyotupa, naomba nikuulize.

Mhe. Waziri katika jimbo lang u la Chambani nina visima viwili vya Rasilhema Ukutini na Ngwachani na visima vile mpaka leo bado havijapata matengenezo.

a) Je, ni lini visima vile vitamaliziwa.

b) Katika kisima kilichopo Ukutini cha Ras El Khaima inasemekana kwamba kile kisima bomba zake zilizotiwa chini zimepinda. Je, utafiti gani ambao umefanyika wa kuona kama kile kisima ni kweli bomba zile zimepinda.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifutavyo.

Kwanza itatulazimu tupate taarifa za usahihi baada ya kusika kutoka kwake, tumepokea na naahidi kulifuatilia na hapo baada ya kujua changamoto iliyopo ndipo nitakuwa na nafasi ya kusema lini haya tutayafanya. Ahsante sana.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa nchi yetu imebarikiwa na mvua nyingi za masika kuwa kubwa mwaka huu na kupelekea mpaka visima kufukiwa na maji ya mvua vya serikali. Je, ni hatua gani Mamlaka ya Maji imechukua kwa makusudi ya kuweza kutibu maji haya pamoja na visima hata vya watu binafsi ili kuepusha kupata athari katika maji hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifutavyo.

Serikali kupitia Wizara yetu na kupitia *ZAWA* ambayo ni Mamlaka ya Maji tunaweka dawa kwa kiwango kinachostahiki, lakini pia niombe kwa wananchi wote tuchemsheni maji ya kunywa kabla ya kunywa.

Nam. 25

Kuweka Ulinzi Katika Wodi ya Mapinduzi Mpya

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:
Ahsante sana Mhe. Spika, lakini kabla sijauliza swali langu naomba kufanya marekebisho. Katika swali langu sijakusudia kuandikwa katika maswali,

nilikusudia kuuliza ulinzi wa Polisi kutokana na huyu mgonjwa tayari alikuwa kishafanyiwa vitendo vya kudhalilishwa na tayari aliyefanya vitendo vile alirudi tena kutaka kumdhuru. Baada ya kurekebisha naomba swali langu Na. 25 lijibiwe.

Baada ya kutokea tatizo la unyanyasaji wa Kijinsia wa mwanamke kutiwa moto huko Paje na kulazwa katika wodi mpya ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, mwanamke huyo aliingiliwa katika chumba alicholazwa.

(a) Je, Wizara yako inalijua hilo.

(b) Na kama unalijua, Wizara yako ina mpango gani wa kuweka ulinzi katika Hospitali hiyo ili matatizo kama hayo yasitokee tena.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri pamoja na marekebisho, majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye kifungu (a) na (b) pamoja na marekebisho aliyoyafanya sasa hivi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nitoe maelezo mafupi kuhusu suala hili.

Mhe. Spika, tukio la unyanyasaji wa kijinsia la uchomwaji moto kwa mwanamke huko Paje lilitokea na kuleta simanzi na mshtuko mkubwa kwa wananchi na taifa kwa ujumla. Mgonjwa huyo alifikishwa na kulazwa katika Hospitali ya Makunduchi na kupatiwa matibabu na baadae kuhamishiwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa matibabu zaidi.

Mhe. Spika, kutokana na uzito wa jambo lenyewe, Wizara haikuwa rahisi kuweza kuwazuia watu au viongozi wasiende kumuona mgonjwa hasa kutokana na silka na tabia na desturi zetu Wazanzibari kwa kufarijiana tunavyotokewa na matatizo.

Mhe. Wizara tulifanya kitendo cha kuhakikisha kwamba utaratibu wa kuangalia wagonjwa unafuatwa ipasavyo.

Saala alilolirekebisha sasa hivi kwamba kulikuwa na kiasi gani cha ulinzi wa kumlinda kijana yule. Wizara yangu baada ya kuona mtiririko wa watu wengi wakiwemo na viongozi wa Dini na viongozi wa Serikali, kwenda kumuangalia

na kumfariji mgonjwa huyu, ilifanya kitu kimoja. Ilimuweka na kumpa elimu mzazi ambaye alikuwa anakaa na mgonjwa huyu na kumuelewesha kwamba watu wanaokuja ni wengi na Wizara haiwezi kukataa moja kwa moja wasije kumuangalia mgonjwa wao.

Kwa hivyo walimtaka awe muangalifu kubaini na kuwatambua wanaokwenda kumuangalia mgonjwa kwa usalama wa mgonjwa, walimpa mambo muhimu ya kufanya ili kuweza kunusuru maisha ya mgonjwa yule. Kwanza walimpa nambari za simu za manesi na wafanyakazi waliomo kwenye wodi ile wakatengeneza vizuri kitasa cha mlango wake na wakamtaka asifungue mlango kumuingiza mtu yeyote kuja kumuangalia mgonjwa hadi aangalie kwenye waya wa dirisha na atakapokubali na kuridhika mtu ambaye anakuja kumuangalia mgonjwa ndiyo afungue mlango na kumruhusu kumuangalia mgonjwa kwa usalama wa mgonjwa.

Mhe. Spika, kitendo hicho yule mama alikifanya na siku ya pili tu baada ya kupewa elimu hiyo aliripoti kwamba amekuja kijana na kutaka kumuona mgonjwa lakini hakuweza kuingia kwa sababu mlango ulifungwa. Yule mama amesema "nimemuangalia kwenye dirisha na nimemkatalia kumfungulia". Kijana yule kwa bahati nzuri alikuwa yupo, kwa hivyo wafanyakazi walikwenda wakamuona na kumuhoji na wakaridhika kwamba hakuwa na tatizo lakini hata hivyo yeye mwenyewe alikuwa ana wasi wasi naye hawakumruhusu na wakamtaka aondoke asimuangalie mgonjwa kwa wakati ule na siku ile na siku nyengine yoyote.

Mhe. Spika, nataka nimthibitishie Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi kwamba mgonjwa yule alitibiwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa imani na upendo mkubwa sana na alitoka pale akiwa katika hali nzuri. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kumuuliza swali la nyongeza.
Pamoja na majibu yake aliyokuwa katupatia katika Baraza hili Tukufu, kama tunavyofahamu utaratibu wa mgonjwa anayepata matatizo ambaye tayari kesi yake ilikuwa imeshafikishwa katika vituo vya Polisi anakuwa na mlinzi wa Polisi.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka kujua Mhe. Waziri mtu aliyefanya kitendo hicho amepatikana na kama amepatikana ni hatua gani za kisheria zimechukuliwa na Wizara yako dhidi ya mtenda kosa huyo.

Mhe. Spika: Lirudie swali lako taratibu akufahamu.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, naomba kurudia swali langu. Nimemuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Afya pamoja na majibu yake aliyotupatia katika Baraza hili, lakini kama tunavyofahamu mgonjwa yule tayari alikuwa kapata tatizo la udhalilishaji ambalo aliunguzwa moto na tayari kesi hiyo ilikuwa ipo chini ya uangalizi wa Polisi.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka kujua Mhe. Waziri mtu aliyefanya kitendo hicho amepatikana na kama amepatikana ni hatua gani za kisheria zimechukuliwa na Wizara yako dhidi ya mtendaji wa kosa hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwa taarifa tulizonazo Wizara ya Afya ni kwamba kijana yule alipatikana mapema kabla hajaamishwa mgonjwa yule kuja Hospitali ya Mnazi Mmoja. Wakati mgonjwa yupo Hospitali ya Makunduchi tayari vyombo vya ulinzi na usalama vilishamshikilia mhalifu yule ambaye alifanya tendo lile.

Kuhusu kwamba ni hatua gani ambazo zimechukuliwa. Mhe. Spika, hili suala naomba zaidi liende katika Wizara inayohusika na kuchukua hatua kwa wahalifu ambao wanatenda makosa kama haya. Mimi kazi yangu nikiwa kama Wizara ya Afya nina kazi ya kumpokea, kumtibu na kuhakikisha afya yake ipo vizuri nimruhusu aende nyumbani kufanya mambo yake ya maendeleo.

Mhe. Makame Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.
Mhe. Spika, suala la ulinzi katika hospitali na vituo vya Afya ni muhimu sana kutokana na kwamba hali ya Zanzibar kusema la ukweli kuna baadhi ya watu hawaiombei heri Zanzibar.

Kwa mfano Kituo cha Afya Mbuzini ni shahidi, mimi na wewe tulikwenda hapana ulinzi wala hapana uzio na kupelekea vijana wa maeneo yale kufanya kituo kile kuwa ni sehemu ya starehe wakati wa usiku.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba vituo vya afya vinapatiwa walinzi pamoja na mahospitali ili kuhakikisha usalama wa wagonjwa wetu unapatikana katika mahospitali hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa hatua ya mwanzo imeweka ulinzi katika vituo vikubwa na hospitali, yaani hospitali kubwa kama Hospitali ya Abdalla Mzee, Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Makunduchi, Hospitali ya Micheweni, Hospitali ya Fidel Casro, lakini ina mpango pia ya kuweka ulinzi katika vituo.

Kwa sababu matukio kama hayo ambayo umeyataja na mengine ambayo yameshatokea tukikumbushana kama tukio lilofanyika Kiuyu Minungwini Pemba la kuchomwa moto kituo kile. Baada ya kuyaona hayo pamoja na matukio mengine tofauti ya kuhujumu mali za serikali, Wizara ina mpango kwa kweli ya kuweka ulinzi katika vituo vyetu vyote kama hali itaturuhusu. Tumuombe Mwenyezi Mungu hali ituruhusu ili tuweza kupunguza changamoto hii kwa kuweka walinzi katika vituo vyetu.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa ruhusa hii ndogo ya kuuliza swali la ngongeza.

Kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Katika jibu mama Mhe. Waziri alieleza wazi kwamba baada ya huyu mgonjwa kulazwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kulikuwa na mtiririko mkubwa wa watu, viongozi wa Dini kwenda kumuangalia huyu mgonjwa.

Swali langu linakuja hapa, kwa kuwa taratibu maalum za kuwaona wagonjwa. Ni elimu gani wameitoa kwa viongozi hao na watu waliokuwa wanakwenda kumuona mgonjwa nyakati ambazo sizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, mgonjwa huyu na wengineo wote huwa wanaangaliwa katika wakati uliopangwa wa kuangaliwa wagonjwa. Kwa hivyo muda wote ambao waliokwenda kumtizama mgonjwa huyu na ambao walifanikiwa kwenda kumuona ni wale ambao walikuwa wanafuata muda maalum uliopangwa kwa mujibu wa utaratibu na hospitali hiyo husika. Vyenginevyo ni baadhi ya wakati

tuliwaruhusu kama viongozi wa Dini pamoja na viongozi wa serikali kutokana na umuhimu wao. Asante sana Mheshimiwa.

Nam. 142

Kufukiwa Mashimo Yaliyotumika Wakati wa Ujenzi wa Baraza ya Mazizini – Fumba

Mhe. Masoud Abrahman Masoud (Kny:Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini - Aliuliza:

Mhe. Spika, katika jimbo la Dimani kuna "mahandaki" mawili yaliyowazi baada ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Mazizini – Fumba. Mahandaki hayo moja lipo Kombeni (chomoani) na la pili lipo Dimani.

(a) Je, Wizara inayo habari kwamba mahandaki hayo yaliyowazi yanachimbwa fusi na udongo na kuuzwa kinyume na sheria.

(b) Lini Wizara itayafukia mashimo hayo na kuirejesha ardhi kama ilivyokuwa kabla ya kuchimbwa fusi kwa ujenzi wa barabara.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 142 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara haina habari ya watu kuchukua vifusi kwenye mashimo mawili ya Kombeni na lile la Dimani. Hata hivyo suala hili tumelipokea na kuahidi kuwa tutalifanyia kazi.

(b) Mhe. Spika, wizara yangu pia kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Mazingira tutahakikisha tunayafukia mashimo hayo kwa kupanda miti mara tu fedha zitakapopatikana.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahante Mhe. Spika, na Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Mahandaki hayo yapo takriban miaka minane tokea baada ya kumalizika ujenzi wa barabara hiyo ya Mazizini Fumba.

a) Je, ni lini kazi hiyo ya ufukiaji itaanza na hasa kwa kuzingatia kifusi pamoja na miche ipo serikalini.

b) Je, ni lini Mhe. Waziri atakuwa tayari akayaone hayo mahandaki kwa macho yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Kama nilivyojibu katika swali mama au majibu mama kwamba pale tu fedha zitakapopatikana tutakwenda kuangalia namna gani ya kuyaziba yale mashimo. Lakini vile vile nataka nimtoe wasi wasi kwamba amesema ni miaka mingi. Nataka kumfahamisha kwamba tathmini ya mazingira maisha yote inapofanywa basi inatakiwa na Wizara husika wawe pamoja katika kutathmini na baadae kuangalia namna gani.

b) Lakini vile napenda kumuhakikishia Mheshimiwa kwa sababu hii barabara kama nilivyosema mwanzo ilikuwa na umuhimu wake na ilikuwa miaka mingi kuijenga, kwa sababu mkandarasi wa mwanzo pia alikatisha baadae akaja mkandarasi mwengine. Mimi nimpongeze sana Waziri aliyekuwepo kwa wakati ule ambaye pia ndiyo muulizaji swali mama kwamba yeye anaijua hali halisi ilivyo. Nina imani kubwa sana tutashirikiana na yeye katika kuhakikisha kwamba hii kazi tunaifanya kwa vizuri zaidi na kwa ufanisi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante Mhe. Spika, na mimi naomba nimuulize Mhe. Waziri swali langu moja la nyongeza.

Kwa kuwa maeneo ya uchimbaji wa fusi katika maeneo ya Shakani pia yapo na maeneo hayo tayari yameshakuwa hatarishi kwa wakaazi wa maeneo yale. Je, Wizara yako ina mipango gani ya kuyashughulikia maeneo hayo ili yasilete madhara kwa wananchi wa maeneo hayo na hasa ukizingatia kipindi hichi cha mvua na maeneo hayo tayari yameshaanza kuleta mmong'onyoko.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa hako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ni kweli kama alivyosema yapo hayo mashimo katika jimbo lake na kama nilivyosema mwanzo kwamba wakati tulivyokuwa tukijenga hizi barabara wakati ule tathmini ya mazingira inayofanyika ni tofauti na hivi sasa tunavyofanya. Hivi sasa tunahakikisha katika zile tathmini za mazingira kwamba tunapojenga barabara basi tunatumia utaratibu wa kuhakikisha yale

mashimo tunayafukia. Licha ya hivyo kama nilivyosema mwanzo tupo tayari kushirikiana na wale wote waathirika na mashimo haya wakati wa uchimbaji wa vifusi kwa ajili ya utengenezaji wa barabara.

Nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi tuendelee kuwa walinzi wa zile sehemu husika ili kuwafanya watu wasijenge kwanza katika maeneo yale, kwa sababu ni maeneo hatarishi kama nilivyosema sehemu zile hata sehemu za Dimani kuna watu wamejenga majumba yao juu ya sehemu zile. Kwa hivyo tukiwa walinzi na vile vile tukiwafahamisha wananchi wetu wasijenge sehemu zile hatarishi, nina imani kubwa sana tutakuwa tumechukua hatua nzuri ya kuweza kuwaokoa wananchi wetu katika hatari yoyote inayoweza kutokea hapo baadae. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi ili kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza lakini pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

a) Mhe. Spika, tunafahamu kwamba utengenezaji wa barabara unapofanyika kuna sehemu ambazo zinatumika kwa kuchimbwa majasi. Hili pia lipo katika Mkoa wa Kaskazini katika kijiji cha Kijini kuna mashimo haya pia yapo ambayo ni makubwa na ni hatarishi sana kwa wananchi na watoto wadogo. Pia na Mkoa wa Kusini kuna mashimo haya haya upande wa Kibele.

b) Je, Mhe. Waziri ni hatua gani ambazo zitachukuliwa kwa haraka kwanza kuyadhibiti haya mashimo japo kuzunguushiwa uzio tu ili wananchi na watoto ambao wanacheza katika maeneo haya ukizingatia yamo njiani na yanaonekana kwa urahisi zaidi ili Wizara iweze kulifanya suala hili kwa haraka ili wananchi waweze kuokoka na maisha yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo ni kweli kila tunapojenga barabara ni lazima tuchimbe kifusi na hizi sehemu sio kama alizosema zipo Kijini, Bumbwini, Mwambe, Micheweni, ni sehemu tofauti na tunakiri kwamba hizo sehemu zipo.

b) Lakini sisi tunalolifanya kwanza ni kutoa elimu kwa watu wetu. Nimesema mwanzo kupitia Wawakilishi waendelee kutoa elimu kwamba watoto wasipite zile sehemu hatarishi na sisi tutakapopata uwezo basi ushauri wake tutaufanyia kazi ili wananchi wetu wasiweze kuathirika na mashimo yale.

Mhe. Spika: Ahsante, Waheshimiwa maswali yamemalizika. Nina tangazo la wageni. Mgeni wa mwanzo aliyekuwepo ni Mgeni wa Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi wa Wananchi Konde, mgeni huyo ni ndugu Ali Hamad Ali. Naona hajafika juu kwenye kwenye *gallery*, wageni wengine waliokuwepo ni kwa ajili ya mafunzo ni viongozi wa Serikali ya Wanafunzi Skuli ya Sekondari Maungani, jumla yao ni 33 wanaongozwa na walimu wao 4, naomba kwa pamoja msimame. Ahsanteni.

Wapo pamoja na Spika wao ndugu Saidati Masoud Hassan. Karibuni sana Baraza la Wawakilishi, ahsanteni sana.

Baada ya matangazo hayo na kabla sijamwita Katibu nitamwita Mhe. Naibu Spika ili aje achukue kiti. Mhe. Naibu Spika, karibu.

(Hapa Mhe. Spika Naibu alikalia kiti)

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Nimesimama Mhe. Naibu Spika, hujanijibu bado.

Mhe. Naibu Spika: Afadhali umekaa Mheshimiwa, nilikuwa sijakuruhusu bado. Sawa kuhusu utaratibu.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Naibu Spika, na mimi nimefanya hivyo hivyo kwamba ulikuwa hujaniruhusu ndio maana nikakaa.

Mhe. Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 63 lakini pia nataka muongozo wako kuunganisha Kanuni ya 40(4) ambayo inasema,

"Endapo Waziri au Mjumbe atatoa ahadi ya kujibu swali la nyongeza kwa maandishi jibu la Swali hilo litawasilishwa kwa Spika ndani ya siku tatu".

Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu aliyoyatoa Mhe. Spika leo asubuhi nimefurahi sana. Lakini na mimi pia nikiri kwamba nina swali la msingi zaidi ya mwaka mmoja tunakaribia au umeshapita ambapo niliuliza juu ya bei ya

nyanya katika soko la Mwanakwerekwe hadi leo sijajibiwa. Swali hili ni muhimu kwa sababu ninajaribu kuunganisha kilimo chetu pamoja na sekta ya utalii.

Nataka nifahamu je, serikali inashindwa kunipatia mimi kwa mwaka mmoja bei ya soko la nyanya katika soko letu la Mwanakwerekwe. Naomba muongozo wako Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umesema kwamba kuna utaratibu ambao tunaoutumia na ni kwa mujibu wa Kanuni tulizonazo kwamba utauliza swali, ikiwa swali lile Mhe. Waziri atasema kwamba atalijibu kwa maandishi itachukua muda wa siku tatu kujibiwa swali lile.

Utaratibu huo umo ndani ya Kanuni zetu. Nakumbuka vizuri sana uliuliza swali hilo na kwa bahati mbaya Waziri anayehusika hapa hayupo. Kwa hivyo nafikiri tuachie sisi Mhe. Spika atalidai tena hilo swali na utajibiwa kwa maandishi kama ilivyokuwa limeagizwa na Mhe. Waziri. Hilo naona tumelimaliza. Ahsante nakushukuru.

Waheshimiwa Wajumbe nafikiri mtakumbuka sana jana kwamba Mhe. Waziri aliweza kufanya majumuisho yake akatoa hoja na baada ya hoja tuliikubali hoja ile. Sasa tutaingia katika utaratibu mwengine, kuingia kwenye Kamati, kwa hivyo nitampisha Katibu halafu baadaye Waziri atakuja.

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya wizara yangu sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu.

Naomba kutoa hoja.

MAFUNGU YA FUNGU D

FUNGU D01 - Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Fungu D0101	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	
	Jumla ya fungu hili ni	781,000

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Shamsi

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, katika uchangiaji wangu katika hotuba hii nilitaka ufafanuzi juu ya suala ya maslahi ya Madiwani.Ningeomba nipate kauli kwa Mhe. Waziri juu ya suala hili la maslahi ya Madiwani, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ndiyo tunaanza na mapato, sasa sijui mapato kwa uwelewa wako yanaingia hapa kuhusiana na hilo suala ambapo umeliuliza. Sio kwa hili limeshakubaliwa

Jumla Kuu **781,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D01 - OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Fungu PD0101 Programu Kuu ya Utaratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu hakijasomwa Waheshimiwa wache kisomwe halafu mtapiga buti.

Kifungu SD010101 Programu Ndogo ya Uratibu wa Tawala za Mikoa

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Rashid Makame Shamsi

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza niombe radhi kwa kupiga buti katika eneo ambalo silo. Mhe. Mwenyekiti katika uchangiaji wangu nilikuwa nataka kujua kwa Mhe. Waziri juu ya hoja yangu ya maslahi ya Madiwani wetu. Suala hili wanalitazamaje, napenda nipate kauli yake nzuri. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri majibu

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza

Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa umahiri wake wa kuuliza maswali. Pili naomba nimuhakikishe kwamba Mhe. Rashid kwamba ni kweli kama nilivyosema jana michango na maswali yalikuwa mingi lakini kwa sababu ya utekelezaji wa Kanuni ya Muda kwa Waziri kujibu masuala sikuweza kupata nafasi ya kuweza kujibu suala lake.

Lakini napenda nimuhakikishe kwamba mfumo wetu bado wa maslahi ya Madiwani upo katika kuwalipa posho na siyo maslahi. Hata hivyo nataka nimuhakikishe kwamba Mhe. Rashid kwamba posho za Madiwani zimepanda kwa kiasi kikubwa kulingana na zile posho za zamani toka tumefanya mabadiliko haya, na tunarajia posho hizo zipande vile vile kutokana na makusanyo ambayo yatakusanywa na Halmashauri zetu.

Jambo jengine ambalo tumewawekea Waheshimiwa Madiwani kwamba tumeamua Madiwani wote katika bajeti hii ya mwaka 2017/2018, kuhakikishia kupata vyombo vya usafiri kwa maana ya vespa ili waweze kufanya shughuli zao vizuri. *(Makofi)*

Na maposho haya sitaweza kuyataja moja moja lakini kuna posho nyingi ambazo tumeziweka kwa ajili ya kuwaongezea maslahi Madiwani wetu na kuwapunguzia ukali wa maisha.

Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Rashid Makame Shamsi

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Tuendelee

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti mimi jana nilizungumzia suala la gari za Zimamoto ambazo zimenunuliwa kwa bilioni 3,400,000,000, lakini mimi bahati mbaya nilidharurika lakini Mhe. Waziri alipokuwa akijibu nilikuwa namuona.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa bado hatujafika huko, hapa ni kwenye Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Lakini Wizara ndio iliyonunua

Mhe. Mwenyekiti: Aah! hatwendi hivyo tunakwenda kwa utaratibu, ikifika uta-*raise* hiyo *concern* yako. Lakini tunakwenda kutokana na utaratibu wa hiki kitabu kilivyowekwa

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Khamis Bakar.

Mhe. Ali Khamis Bakar : Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Waziri jana wakati akinijibu suala la Soko langu la Tumbe alinifahamisha vya kutosha, lakini mimi nimwambie kwamba alinisukumizi maneno ya kinyumbani. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, wakati soko lile linajengwa, mimi Waziri aliyekuwepo simjui, Naibu Waziri aliyekuwepo simjui na kilichotolea sikifahamu mpaka kufikia soko lile likawa halitumiki.

Vile vile soko lile limejengwa mimi nimelikuta tu kwamba mimi tayari nishakuwa kiongozi nimelikuta. Sasa basi mimi nafahamu kama Micheweni kuna Wilaya na vile vile kuna Mkoa na viongozi wa Wilaya na Mkoa wapo, lakini kuna msemo usemao, "*Mgeni awiya mwenyeji apone",* hili suala liko kiserikali na hii ni Serikali kwa kuniambia kwamba mimi nionane wananchi tu, basi naona ni jambo kidogo siwezi kulimaliza. Ningekuwa mimi naweza kulimaliza suala lile nisingeweza kulileta hapa.

Kwa hivyo naomba muongozo wake ili tuone soko lile linafanyiwa kazi kama ambavyo limekusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri majibu

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe majibu ya Mhe. Mwakilishi. Kwanza siwezi kumsukumiza. *(Makofi)*

Kama alinisikiliza vizuri sana nilipokuwa nikitoa majibu, yeye nilimuomba ende akawaelimishe wananchi wake ili wakubaliane na utaratibu wa kisheria. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kumuomba Mhe. Mwakilishi, tena nilitumia lugha ya kumuomba atusaidie kwenda kuelimisha wananchi wake na bado sikujivua.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nilisema tunafanya mazungumzo na sekta husika ambao wao ndio wanaosimamia hili soko ili tuweze kupata muafaka na soko hili liendeshwe kwa mujibu wa taratibu za kisheria, ndio jibu langu

lilivyokuwa. Kwa hivyo sikumsumiza ndugu yangu Mhe. Mwakilishi, nilimuomba akatusaidie kuwaelimisha wananchi wa jimbo lake na hilo sidhani kama nimefanya kosa.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hayo ndio yalikuwa majibu yangu na wala sikumsukumiza. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Khamis Bakar.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Sawa Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia kaka yangu lakini pia na mimi namuomba kwamba hili suala anisaidie ili tufikie hatua ambayo tumekusudia.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu katika kifungu hiki Uratibu Tawala za Mikoa nilizungumza kadhia nzima ya suala langu la barabara. Nashukuru Mhe. Waziri alinijibu kwa kina kabisa hakumungunya maneno wala kupepesa macho.

Sasa naomba atoe kauli ili iwe kama kauli ya Serikali kuhusu kadhia hii, sasa hivi ina miaka miwili barabara ile na pesa ilitolewa milioni mia moja (100,000,000/=) na nakumbuka milioni mia (100,000,000/) kipindi hicho alokuwa Waziri Mhe. Juma Duni na Naibu Waziri alikuwa Mhe. Issa Gavu na aliahidi mara tu lami itakavyopatikana ile barabara itatengenezwa. Ishakuja lami zaidi ya miaka miwili bado haijatengenezwa.

Naomba akiri mbele yangu kwamba yeye si suala lake ili azungumze na Waziri wa Miundombinu waliyochukua ile kasma ni lini barabarza ile itatengenezwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa kukazia hoja yake pamoja na majibu mazuri sana ambayo amekiri nimemjibu jana.

Ninachotaka kusema aliyekwenda alikuwa ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na ndiye aliyechukua *commitment* za Serikali. Kwa msingi huo bado jukumu lile la Serikali liko pale pale.

Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikitoa hayo majibu ambayo amekiri mwenyewe kuwa ni mazuri, nilisema tutawasiliana na Wizara husika au sekta

husika kulikumbushia jambo hili ili liweze kupatiwa ufumbuzi, kwa sababu *commitment* ile ilikuwa ni ya Serikali na siyo ya sekta moja. Kwa hivyo nataka nimuombe Mhe. Abdalla avute subra na mimi najua vile vile Mhe. Mbunge wa Jimbo la Mpendae ambaye alitoa mchango wake bado Serikali inathamini mchango wake na kama Serikali itahakikisha kwamba ahadi na *commitment* ambayo ilitolewa na Serikali tunaitekeleza kwa muda muafaka.

Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana narudia tena pale pale, nakamata kauli yake ya mwisho muda muafaka. Naomba huu muda muafaka mwakani au bajeti 2019/2020, ni hapo tu ili na mimi nipate nguzo ya kuja kukamatia kwamba bajeti iliyopita uliniambia 2019, nimestahamili mpaka 2019 hili zoezi likamilike, anijibu kauli hiyo tu baadae tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, unaposema muda muafaka maana pale Serikali itakapota uwezo, inawezekana ikawa kesho, inawezekana ikawa kesho kutwa, inawezekana ikawa mwezi ujao.

Ndani ya bajeti ya mwaka 2017/2018 tutajitahidi *commitment* ile tuitekeleze. Kwa hivyo tarehe ngapi mwezi gani siwezi kumwambia, lakini muda muafaka, inaweza ikawa kesho, inaweza ikawa keshokutwa.

Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Bwa mkwe wangu sitaki kumuuzi sana, madhali kishaniambia kwamba ndani ya bajeti ya 2017/2018 tuendelee.

Jumla ya programu ndogo hii 864,165,000

Kifungu SD010102

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii wakati nilipopeleka masuala yangu kwa maandishi katika hotuba yake kwenye ukurasa wa 12 mpaka 13 kwenye programu hii, nilitaka ufafanuzi kuhusiana na uidhinishwaji wa mikataba ya ajira kwa muda maalum. Nilitaka kujua kwamba huo muda maalum ni muda gani lakini pia wanasema kwamba waliidhinisha mikataba mipya 11, mikataba hiyo ni mikataba ya kada gani naomba nijibiwe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mheshimiwa naomba nisaidie hili kwenye kifungu husika asije akaulize kwa sababu mikataba hii hasa aliuliza kwenye Idara Maalum za SMZ.

Hawa ni askari ambao tunawahitaji wawepo katika Idara Maalum na mikataba mingi hii imeidhinishwa kwa sababu ni wengi wao wakiwa ni wateuliwa wa Mhe. Rais. Lakini mkataba mmoja tumemuajiri kwa mkataba wa miaka miwili mshauri kutoka JKT ambaye anatushauri kuhusu kuimarisha kikosi chetu cha JKU.

Kwa hivyo kada gani, ni kada za ulinzi maaskari ndio wameajiriwa katika mikataba hiyo. Ahsante sana.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilisema kwamba utaratibu unaotumika katika kuzitengeneza hizi *feeder road. N*imekuwa nina wivu kuona barabara ya Kikwajuni, Mitiulaya na nyengine za mjini zinatengenezwa hali ya kuwa kwenye watu wengi ni Wilaya ya Magharibi ikiwemo barabara yangu ya Welezo ya Hawai.

Mhe. Mwenyekiti, suala langu tarehe 24/04/2014 Mhe. Rais wa Zanzibar alialikwa kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa tawi la Mtofaani alipofika aliwakuta wananchi hali yao mbaya sana kiasi ambacho akina mama, ndugu zangu wa kike na dada zangu wanazalia majumbani hawawezi kufika hospitali kwa hali ya barabara.

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliwaahidi wananchi wale tarehe 24/04/2014 kuwatengenezea barabara yao. Sasa Mhe. Mwenyekiti, barabara hiyo mpaka leo haijatengenezwa. Nimekuwa nina wivu za Mjini kusipo shida ndio zinatengenezwa, lakini za kwetu kwenye shida hazitengenezwi. Sasa lini Mhe. Waziri lini atanitengenezea barabara yangu walioahidiwa na Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo tatizo linakuja kwamba muda wa kujibu masuala haukuwa rafiki, lakini majibu yote yapo na sisi tunafanya kazi kutekeleza Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, na kila sekta imeandaa programu yake ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi kutoka mwaka 2015/2020. Na ahadi hii mbali tu ya kuja lakini tayari ilishawekwa kwenye kitabu chetu cha ilani, kwenye ukurasa wa 149 barabara ambazo zitajengwa kupitia Ilani hii kwenye ukurasa 149 Welezo, Amani, Ng'ambu kilomita 2.9.

Kwa hivyo sisi serikali kwa maana Wizara zote zinazohusika na utengenezaji wa barabara tumetakiwa kitabu hiki tukizingatie, na ahadi ya Mhe. Rais ni ya miaka mitano. Najua Mhe. Hassan kuwa tatizo liliopo nadhani anazo baadhi ya *information*, ni juhudi gani sisi Tawala za Mikoa tunazifanya kwa ajili ya kujenga barabara ile.

Tayari tulishakubaliana na wenzetu wa *DIASPORA*-Milele *Foundation* kwa kuiweka kifusi barabara ile yote halafu serikali iweke lami. Uwezo huo serikali tunao. Kwa hivyo Mhe. Hassan namuomba asubiri tufanye mawasiliano ya kiserikali kati ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Wizara yetu pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ili tuone utekelezaji huu wa Ilani ambao ndio umetuweka hapa sisi kwenye *front bench* unatekelezeka. Kwa hivyo nimuombe Mheshimiwa avute subra ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nakubali maombi ya Mhe. Waziri lakini nataka nimwambie mambo mawili.

Barabara wanayotaka kuijenga *Milele Foundation* ni barabara ya pale *Jeshini Missile* mpaka kwenye kituo cha hospitali kipya hao *DIASPORA*. Barabara ninayoizungumzia mimi aliyoiweka ahadi Mhe. Rais tarehe 24/04/2014 ni barabara ya Hawaii, kutoka Msikiti wa Njano kwenda Mtofaani chini. Hiyo ndio ninayoizungumzia mimi, ile sio ninayoizungumza mimi. Na kutoka Welezo shamba hiyo sio, kwa sababu hii ni Tawala za Mikoa zile barabara za ndani zinashughulikiwa na uratibu wa masuala ya Tawala za Mikoa, hii ndio barabara ninayoizungumzia mimi.

Nimefahamu lakini na yeye nataka nimkumbushe tu kwamba barabara hii ina ahadi ya Rais ambayo pia Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Sasa ahadi ya Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi ambaye pia ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuiweka miaka minne sifikirii kama inapendeza, haipendezi. Naomba tuondelee lakini huku akijua kwamba pale Rais ameweka ahadi na mtekelezaji wa ahadi wa Rais ni

yeye, na hasa ukizingatia leo yeye ana kazi kubwa anafanya. Kwa hivyo naomba naamini ataitekeleza kabla ya bajeti ijayo.

Naomba tuendelee mheshimiwa. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri una majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tunazungumza lugha moja, ndio maana nimetanguliza ahadi za Ilani ana ahadi za Mhe. Rais.

Kama atakuwa amenisikiliza vizuri nimesema kwa hii ahadi ya Rais ambayo aliitoa tarehe anayoisema tutawasiliana na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili tujue ahadi hii hasa nani wa kuitekeleza, kati ya Tawala za Mikoa au Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Ikiwa ni Tawala za Mikoa hakuna tabu tuko hapa kwa ajili ya kutekeleza ahadi za Mhe. Rais na ahadi za Ilani.

Kwa hivyo Mheshimiwa nadhani hata nilivyosema tutakaa vile vile na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwanza tuchanganue, hizi njia hasa zilizoko vijijini tafsiri ya *feeder road* ni ipi na tafsiri ya *main road* ni ipi. Tukeshafikia hapo kila mmoja atapewa jukumu lake na tutalisimamia. Na ni kweli nakubali kwamba niko hapa kwa ajili ya kutekeleza maagizo yote ya Mhe. Rais, lakini tutafata utaratibu tutawasiliana na Ofisi ya Rais Ikulu ili tuweze kujua hasa mwenye jukumu hili ni nani. Lakini suala hili madhali ni ahadi ya Mhe. Rais litatekelezwa tu. Ahsante sana.(Makofi).

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa msaidieni Mhe. Suleiman Makame Ali, hapana Mhe. Simai Mohammed Said sio wewe nimeshamchagua Mhe. Suleiman.
Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi juzi nilipokuwa nikichangia nilizungumzia kuhusu barabara ya Ndagoni na kuhusu barabara ya Birikau yenye ahadi ya Rais. Na nadhani Mhe. Rais alisema kwamba atatekeleza zile ahadi zote ambazo zimeahidiwa na Mhe. Rais nadhani alilisema suala hilo na kwenye *hansard* iko. Barabara ya Birikau iliahidiwa na Mhe. Rais aliyepita Dkt. Amani Abeid Karume ni Rais aliyepita kupitia Chama hiki hiki cha Mapinduzi ambayo Ilani yake tunaitekeleza. Nataka kujua je, ni lini barabara ile ambayo ina ahadi ya miaka 10 sasa kutekelezwa ili wananchi wale kuwaondoshea usumbufu.

Vile vile kwenye suala ya barabara ya Ndagoni. Mhe. Waziri nilizungumza kuhusu barabara hiyo na Ndagoni ndiko kwenye roho ya Pemba, lakini pia vile vile vikosi vyetu wanapata tabu kwenda Ndagoni hususan wakati huu imechafuka na nilisema kwamba mpaka punda kule hendi kutokana na barabara ilivyochafuka.

Ndani ya mwaka 2013 vikosi vyetu vile ilibidi wapite njia ya Wesha kupitia baharini na wakazama baharini. Je, Mhe. Waziri una mpango gani wa kuhakikisha kwamba ndani ya bajeti hii kuiangalia barabara ya Ndagoni kwa jicho la huruma.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nimepata taarifa kutoka *control room* kule wanakoweza ku-*control* hivi vipaza sauti vyetu, wanasemaje kwamba mtu anapotaka kusimama ana-*press button* inafika mara tano. Haya ni mambo ya *electronic*. Kwa hivyo mara nyingi sana yenyewe yanakuwa hayakubaliani na hivyo. Hilo moja.

La pili ni kupiga meza, hizi meza tunazipiga kwa nguvu kiasi inatokea huku wanapiga kwa sababu ni *electronic* zinachanganyikana. Kwa hivyo nawaomba sana Waheshimiwa mpaka nikutaje, mimi nakuoneni, nikikutaja ndio una-*press* hii *button* ya kuwa unaweza kuzungumza, sio unaibonyeza, unaibonyeza tu. Mimi nakuona bila ya hicho kidude chekundu kujitokeza. Naomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kuninyanyua kwa mara nyengine tena. Mimi nadhani tuelewane Waheshimiwa Wajumbe jibu langu bado litakuwa lile lile.

Kwa mfano, hiyo ahadi ambayo ameitoa Rais Mstaafu Karume, mimi wakati huo sijawa Waziri bado lakini serikali haitegemei nani yupo. Nimesema kwamba tutawasiliana na Ofisi ya Rais Ikulu tuzione zile ahadi ambazo zimetolewe na Waheshimiwa Marais ili tuzichanganue na tujue barabara gani inajengwa na Tawala za Mikoa na barabara gani itajengwa na Wizara ya Ujenzi. Kwa hivyo mimi nadhani Waheshimiwa wote ambao wanazungumzia masuala ya barabara majibu yake ni hayo.

Hata mimi kwangu kule jimboni nina barabara ambazo zina ahadi ya Mhe. Rais, nina pale Kiongele/Mkwajuni, Mtambile/Muanda na, na, na. Lakini tutafata utaratibu wa kiserikali ili tuweze kutekeleza ahadi hizo. Kwa hivyo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wavute subra. Kama jana nilivyosema tutakaa na Wizara ya Ujenzi tuzichanganue halafu twende serikalini na hasa

baada ya kupata hizi ahadi ambazo Waheshimiwa Marais waliweza kuzitoa. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa vile Mhe. Waziri amejibu nadhani tumemfahamu na amesema kwamba atakaa na Wizara ya Ujenzi ili kufafanua barabara zipi. Kwa hivyo mimi naomba tuendelee lakini nataka kujua kwamba hatua zaidi inachukuliwa ili kuona usumbufu huu unaondoka.

Mheshimiwa tuondelee.

Jumla ya Programu Ndogo	736,835,000
Jumla ya Fungu	**1,601,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Mhe. Mwenyekiti: Tushamaliza Mheshimiwa, limeshakubaliwa. Hii ni jumla kuu si ndio. Hapa tuko kwenye jumla kuu Mheshimiwa, ilikuwa upige kule kwenye jumla ndogo, wamepewa nafasi watu watatu, sijui umenielewa.

Tuendelee.

FUNGU PD 0102 – PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA UTUMISHI NA URATIBU WA IDARA MAALUM ZA SMZ

Kifungu SD010201 Progaramu Ndogo ya Usimamizi wa Utumishi na Uratibu wa Idara Maalum za SMZ

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, sikusudii kuzuia fungu la Mhe. Waziri isipokuwa kwa *spirit* ya kutengeneza tu. Hivi sasa kuna wapiganaji ni *Senior Officers* wanastaafu, lakini mafao yao kuna malalamiko kwamba hayakutengenezwa ipasavyo au hayako katika mipango mizuri ya kutengenezwa. Na kidogo wanatoa malalamiko makubwa na si vizuri kwamba maafisa wetu hawa wapiganaji wetu na bado tunawahitaji.

Sasa ningemuomba sana Mhe. Waziri hili suala akakaa nao hawa ma-*officer* wakawapa *forum* na wao akawasikiliza kwa lengo la kuwatendea haki ili haki itendeke na wao wajihisi wanastaafu na mambo yao yanakwenda vizuri. Mhe. Waziri namuuliza tu kama analijua sawa basi kama halijui nampa taarifa hiyo ili hili suala alisimamie ipasavyo. Mheshimiwa ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na bado nataka niseme kwamba bado Yanga tunaendelea sisi kwa mwaka wa tatu kuwa mabingwa.

Nataka niseme suala hili nalijua na napokea ushauri wake kwamba nitawaita na nitakaa nao ili tutafute ufumbuzi wa matatizo yao yaliyopo. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana wakati jana nilipokuwa nikichangia nilionesha *concern* yangu ya vikosi hivi vya SMZ, kwa kuwa kipindi kile cha matatizo wanakuwa wanafanya kazi za bidii na kubwa sana.

Lakini kipindi hiki tunakuwa tunawaona kama hawafanyi kazi, lakini nia yangu niliomba kupatiwa bima za afya kwa vikosi vyote vya SMZ ili basi kuwasaidia pamoja na kuwa Mhe. Rais tunampongeza kaongeza mshahara. Lakini kuwasaidia vikosi hivi kupata bima ya afya. Sasa sikulipata vizuri hili kama Mhe. Waziri ame-*agree* au vipi ningeomba tu ufafanuzi tu zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana ndugu yangu Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa kuliona hilo na nataka nikubaliane naye kwamba vijana hawa au wapinaji wetu wote wanafanya kazi nzuri sana, na ndio maana Mhe. Rais ameamua kuwatunza kwa kuwaongezea maslahi yao.

Lakini nataka nimuhakikishie Mheshimiwa kwamba suala lake serikali tayari tulishaanza kulifanyia kazi na kwenye bajeti ya mwaka huu 2017/2018, serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 2 kwa ajili ya wafanyakazi wote wa serikali kwa ajili ya bima ya afya, wakiwemo wapiganaji wetu. Kwa hivyo ushauri wake ni mzuri na umekuja wakati muafaka. Nashukuru sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee *hundred percent.*

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi katika fungu hilo nilikuwa naangalia kuhusu maslahi ya watumishi wa Idara Maalum za SMZ kwenye fungu hilo, linasema kuajiri na kusimamia. Katika mwaka wa fedha unaoishia Juni, 30 2017 nimeona kwamba kuna vijana 22 tu walioajiriwa kutoka JKU, lakini sikuona KMKM, sikuona Zimamoto, sikuona Mafunzo.

Sasa mimi nilitaka nifahamu. Je, haya ndio yaliyokuwa mahitaji ya vijana kwa kuajiriwa au ni tatizo gani lililosababisha kama vikosi vyengine visipate nafasi za kuajiri vijana hawa. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Omar Seif Abeid, lakini kwa utaratibu wetu haturipoti askari wangapi tumeajiri, hatuwezi kusema. Kwa hivyo, aridhike na hayo maandishi ambayo yapo. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Jumla ya Programu Ndogo		185,000,000
Kifungu PD0102	Programu Kuu ya Usimamizi wa Utumishi na Uratibu wa Idara Maalum za SMZ	185,000,000
Kifungu PD0103	Programu Kuu ya Usimamizi wa Utumishi wa Idara Maalum	
Kifungu SD010301	Programu ndogo ya Usimamizi Tume ya Utumishi wa Idara Maalum za SMZ	
Kifungu PD0104	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais Tawala za Miko, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ	
Kifungu SD0104	Programu ndogo ya Uratibu wa Kazi za Mipango, Sera na Utafiti Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kupatiwa ufafanuzi. Lakini kabla ya kujenga hoja yangu nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri, kwamba leo jinsi anavyotujibu, anatujibu katika hali ya utulivu, ametulia kabisa, nadhani kwa sababu leo ndio anakaimu kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu ambariki. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa ufafanuzi uliotolewa na Mhe. Waziri mwenyewe pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha kuhusu suala la hoja

yangu ambayo nilijaribu kuijenga hasa baada ya kuona kwamba Waheshimiwa karibu sote, kila mmoja anadai kujengewa barabara zake za ndani.

Lakini kwa kuangalia mafungu ya Tawala za Mikoa na Halmashauri na kwa sababu Mfuko wa Barabara ndio unaochangia fedha hizi, lakini bado kwa kuangalia Mfuko wa Barabara fedha ambazo tunazotoa kodi ni ndogo hazitoshi. Kwa hivyo nilijaribu kupendekeza kwamba kwa kuwa sasa hivi tuna ile tozo ya shilingi mia moja, nikapendekeza basi sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao tunapaswa kuishauri serikali, kwa sababu haya mawazo ya serikali bajeti inapokuja, inakuja baada ya mawazo ya Wawakilishi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa bado nilikuwa namshauri Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Fedha ili hizi barabara zetu nyingi za ndani ziweze kujengwa, basi ni vizuri hata kama sio bajeti ya mwaka huu, lakini kwa kuzingatia bajeti ya mwaka ujao tuangalie sasa na sio kuongeza kodi. mimi nilipendekeza kuongeza tozo badala ya shilingi mia moja iwe shilingi mia moja na hamsini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu katika tozo ambayo wanaiona wananchi moja kwa moja utekelezaji wake ni hii *road toll* ambayo ya mafuta, maendeleo yake tunayaona wazi wazi bila ya kufanya matatizo yoyote. Sasa nilikuwa napendekeza labda ushauri wangu huu Mhe. Waziri nadhani katika bajeti inayokuja ikiweza kutekelezwa hii, basi naamini huu ugatuzi wa madaraka uliofanyika sasa hivi utaweza kuzisaidia Halmashauri zetu kuwa na fungu kubwa kwa ajili ya kuboresha barabara zetu za ndani. Sasa nilikuwa nataka kauli ya serikali labda katika hili namna gani litaweza kutekelezwa katika bajeti ijayo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma jana Mhe. Waziri alilizungumza vizuri sana na ndio maana tunasema wakati Mhe. Waziri anapojibu masuala muwemo humu ndani, alizungumza na hilo ambalo unalitaka wewe na ameahidi kwamba kipindi kijacho kwa sasa hivi ni vigumu, lakini mwaka 2018/2019 hilo linaweza kuwa *considered*, amelizungumza lakini namuachia mwenyewe Mhe. Waziri. Yeye amelijibu jana vizuri sana kwa kweli.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyosema lakini kwa sababu Mhe. Hamza Hassan ni mtetezi wa wengi mpaka Mjumbe wa UWAWAZA pia na barabara hizi zinapitwa na wengi na UWAWAZA pia wanazipita naomba niseme kwamba,jana kweli nilipokuwa nikitoa majibu na alipokuwa akichangia Mhe. Waziri wa Fedha, kwa sababu kama tunavyojua

sekta ya fedha na kodi inashughulikiwa na Wizara ya Fedha na nadhani Kamati ya Bajeti ya Baraza watakuwa wanajua namna ilivyozungumzwa bajeti ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, wadau wote au wahusika wengine Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora samahani, wahusika wote wa bajeti na wahusika wa ada na kodi walishirikishwa na wakaambiwa na serikali kwamba hakuna tozo wala ada itakayoongezeka, ni vigumu serikali sasa kuongeza hapa ghafla. Lakini kwa mwaka ujao wa fedha wazo lake ni zuri sana na litatupa uwezo wa kuweza kuongeza fedha au fungu kwenye ule Mfuko wa Barabara kwa ajili ya Halmashauri.

Kwa hiyo jambo hili litatekelezwa katika mwaka 2018/2019 mwaka wa bajeti. Kwa mwaka huu hatuwezi kutekeleza isipokuwa tulichokubaliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha kwamba badala ya kutegemea *source* moja tu ya Mfuko wa Barabara, miradi hii zile kilomita 50.8 za barabara za *feeder roads* tumewasiliana na Wizara ya Fedha kupitia Tume ya Mipango ili ziingizwe katika programu ya miradi itakayoombewa fedha kwa nchi wahisani pamoja na mashirika ya kimataifa, ili tuwahi na kumudu kutekeleza Ilani ya uchaguzi cha Chama cha Mapinduzi ambayo tumewaahidi wananchi.

Mhe. Mwenyekiti ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsane sana na mimi nikubaliane na Mhe. Hamza Hassa Juma maneno yake kumtabiria nyota njema Mhe. Waziri huko mbele Mungu akitujaalia penye uhai. Hoja yangu nielimishwe Skuli ya Darajani na Vikokotoni kutokana na umuhimu wake na vizuri alipokuwa akijibu alisema maendeleo yafikiwe kwa wananchi. Pili akasema ofisi inawagusa wananchi muda mfupi tu, serikali ikisikia mambo maovu haiwezi kustahamili na akataja Ilani na bahati nzuri ninayo Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Naomba nimtakie mafanikio na maendeleo ya kiuchumi.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chni ya uongozi mahiri wa Dkt. Ali Mohamed Shein inaweza kutekeleza kwa mafanikio makubwa Ilani ya CCM uchaguzi mkuu wa mwaka 2010/2015 na kuendelea na kuimarisha moja ya kitaifa na utoaji wa huduma mbali mbali za kiuchumi na kijamii.

Baadhi ya mafanikio hayo ya kujivunia ni kama yafuatayo, hali ya uchumi na elimu ya msingi. Leo kuna baadhi ya skuli darasa moja wanafunzi 60 mpaka 80 na skuli nyengine huvuja wakati kama huu wa masika. Nafikiri

atawatengenezea vya kutosha, sifikirii kama serikali itafanya kosa kuondosha skuli zile pale na zipo tangu ukoloni enzi hizo. Leo mtu akaja kutoka nje ya nchi akitaka kumuelimisha hapa niliposoma atakuta duka ni kitu cha ajabu na huku watu wanatushangaa.

Naomba atumie upole wake ambao anaaza kuutumia, anielimishe kuwa zitabaki vile au kuendelea kutaka kuziondosha skuli zile, wakati huku tukishuhudia mahudhurio ya wanafunzi wetu darasa moja watu 60 au 70, na huku tunachangishwa madeski na sisi sote mashahidi.

Mhe. Mwenyekiti: Uliza swali Mhe. Jaku maelezo ni mengi, hebu uliza swali ulilokusudia kuuliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja yangu kuwa hizi skuli zitaondoshwa au zitaendelea kubaki ili wanafunzi wapate kuzitumia.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimshukuru sana Mhe. Jaku Hashim kwa swali lake zuri ambalo litasaidia pia kutoa elimu kwa wananchi mbali ya kwamba taasisi zetu zinazohusika na jambo lile zimekuwa zikienda kwenye televisheni na redio mara kwa mara kuwaelimisha wananchi. Lakini nataka nitumie fursa hii kusema kwamba serikali inapofanya jambo lake inakuwa imepanga na huu ni mpango wa serikali. Kwa hivyo azma ya uvunjaji wa Skuli ya Vikokotoni kwa ajili ya kujenga *shopping mall* iko pale pale. *(Makofi)*

Skuli ya Darajani haivunjwi kwa sababu ni jengo la kihistoria litabakia isipokuwa litapangwa upya ndani ya jengo kwa ajili ya kuweka *structure* kwa ajili ya biashara zenye asili ya Kizanzibari. Kwa hivyo Skuli ya Darajani itabakia, Skuli ya Vikokotoni itavunjwa na watoto wanaosoma maeneo yale, kwanza tumefanya *research*, kwanza eneo lile sasa si rafiki kwa kuwepo skuli, kwa sababu hapana utulivu kwa sababu ya wafanyabiashara.

Kwa hivyo wanafunzi watakaotolewa pale, serikali ina mpango wa kujenga skuli ya ghorofa pale ng'ambu Rahaleo. Kwa hivyo wanafunzi watakaotoka pale na wengine watasoma katika skuli ya Rahaleo na tunafanya hivi kwa sababu ya maslahi ya wananchi wote wa Zanzibar.(Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, nimekuwa nikisema hakuna *center* yoyote ya mji ambayo watu wanafanya biashara katika mabanda,,Kkwa sababu pale ni *center* ya Mji

Mkongwe, tunataka tuhakikishe pale tunaweka kitu ambacho kitafanana na miji na sio vile ilivyokuwa hapo kabla.

Lakini historia ya kuvunja skuli nakubali kwamba Skuli ya Darajani amesoma pale, wamesoma watu wakubwa tu, kuna wafanyabiashara maarufu, kuna Rais Mstaafu Amani Abeid Karume amesoma pale, lakini hata skuli ya Gulioni ndio skuli ambayo amesoma Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein, lakini tukaona kwa mazingira ya sasa skuli iliyokuwepo ilikuwa haifanani na eneo lile, serikali ikaamua kuvunja na tukajenga *BoT.* (*Makofi*).

Kwa hivyo serikali inaangalia mahitaji ya wakati inafanya mambo yake. Kwa hili Mhe. Jaku Hashim namuomba akubali kwamba serikali imeshaamua na tutajenga pale *shopping mall* na Skuli ya Vikokotoni tutavunja, Skuli ya Darajani haivunjwi lakini itapangwa upya mule ndani lakini wanafunzi watakaohama Vikokotoni na Darajani wanajengewa skuli mpya nzuri ya ghorofa pale Rahaleo. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimesikia kaimu wa Makamu wa Pili pengine Mwenyezi Mungu akimjaalia huko mbele Mwenyezi Mungu akituweka hai majibu yake.

Lakini hebu tuelezwe na hii mikataba kwa nini haiwekwi wazi mkishakuitangaza. Mkataba wa Bwawani Wajumbe wanataka kuona pengine na Wawakilishi humu, mkataba wa pale ukoje.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim hoja hiyo ni nyengine kabisa haihusiani na hiki kifungu, naomba utuachie tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ungenisikiliza mpaka nikamaliza kwanza hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana, naomba utuachie tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ngoja hapa tupo kwa niaba ya wananchi, tunajadili suala la wananchi.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Serikali tumezowea humu ndani kubomoa kwanza kabla ya ujenzi kufanywa, wangejenga skuli kwanza wananchi wakaona kile kitu kwanza wakaridhika.

Mhe. Mwenyekiti: Aah! sawa Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Lakini vyengine vyovyote serikali inaweza kuja kwenda Mahakamani Mhe. Mwenyekiti, tujenge hoja, tuangalie umuhimu wa *mall.* Leo Bwawani ipo haijajengwa, Michenzai *mall* inataka kufanyika na pale tunafanya nini. Tunawatumikia kweli wananchi hivi? Leo huku serikali inasema inaondosha msongamano katika Mji Mkongwe huku msongamano unatiwa katika Mji Mkongwe....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku kaa kitako. Tunaendelea.

Jumla ya Programu ndogo		456,000,000
Kifungu SD010402	Programu ndogo ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum	2,409,800,000
Kifungu SD010403	Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum	

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Mimi sina nia ya kumnig'inia *tie* Waziri wangu na nimpongeze sana kwa kunikubalia njia yangu ya Msingini kwamba itajengwa muda si mrefu. Lakini pia nimpongeze Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kunikubalia au kumsaidia Mhe. Waziri kwa kujibu masuala ya jana. Sasa mimi katika masuala yangu ya jana nataka Waziri anitolee kauli, nilimwambia naomba tuondoke mimi na Waziri wa Ardhi kuelekea...*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilinde maana naona makofi yamekuwa mengi. Mimi na Waziri wa Ardhi kuelekea mji mkuu wa Pemba kwenda kuupanga mji wetu. Kwa hivyo, naomba kauli ya Waziri kabla ya bajeti ya Waziri wa Ardhi tuwe tumeshakwenda Pemba. Hilo lilikuwa swali la la kwanza.

Swali la pili nataka aniambie lini tunahamia Ofisi yetu ya Mkuu wa Wilaya ile iliyokuwa tunafanya matengenezo.

Na swali la tatu ilikuwa namwambia lile jina waliloipa watu ile njia ya Msingini 'Sele Manga' vipi amelikubali au laa. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Suleiman Sarahan Said - jembe lisilo mpini, kwa masuala yake.

Kwanza nimemkubalia suala la kuondoka mimi na yeye na Mhe. Waziri wa Ardhi, sio yeye na Mhe. Waziri wa Ardhi peke yao. Kwa hivyo tutaondoka mimi, yeye na Mhe. Waziri wa Ardhi kwenda kuangalia hali halisi ya mji wa Chake Chake. Hilo halina mashaka isipokuwa yeye na Mhe. Waziri wa Ardhi nadhani hilo silikubali, nitakubali tuondoke mimi, yeye na Mhe. Waziri wa Ardhi. *(Makofi)*

Suala lake la pili kuhusu suala la lililokuwa jengo la Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake. Hili jambo limezungumzwa, limeshauliziwa swali hapa Barazani na limeshajibiwa na kwa mujibu wa Kanuni limejibiwa katika mkutano huu huu wa Baraza.

Lakini kwa faida ya wananchi na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba hili jambo Mkuu wa Wilaya kwanza hakuondoshwa, aliondoka kwa ubovu na uchakavu wa jengo lililokuwepo. Kama alivyosema Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji siku ile na majibu yakatiliwa nguvu na Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kwamba iliyokuwa Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilikuwa na tatizo la kuchanganya Makumbusho na Idara ya Nyaraka, ziko pale pale kwenye makumbusho karibu na Hospitali ya Chake Chake, ikaonekana si busara kukusanya makumbusho na nyaraka.

Kwa hiyo, Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya wakati ule ikaliomba jengo lile serikalini, ilipoliomba jengo lile serikalini serikali ikakubali, ilipokubali Wizara ya Utumishi na Utawala Bora ikaingiziwa fedha kupitia Ofisi ya Nyaraka kwa ajili ya kulitengeneza jengo lile kwenye kasma zao. Ni dhahiri kwamba jengo lile sasa linahitajika litumike na Idara ya Nyaraka na hasa kwa sababu ya unyeti wa nyaraka zetu.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwanza tutafanya marekebisho ya dharura kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ili aendelee kukaa pale na juhudi zinafanyika ili aweze kupata jengo ambalo litakuwa na hadhi ya Mkuu wa Wilaya. Tatizo hili la majengo kwa Ofisi ni karibu la serikali nzima. Hata mimi Ofisi ya Rais nina tatizo kubwa sana la uhaba wa nafasi na majengo yaliyokuwa mazuri zaidi. Nikwambieni tu hizi mvua zinazotokea wafanyakazi wangu, watumishi wetu kwenye jengo la pili la Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa

Serikali za Mitaa na Idara Maalum hulazimika kutoka ndani ya jengo kwa sababu kuna mambo si ya kawaida.

Kwa hivyo jambo hili serikali inalichukuwa na serikali inaazimia na imeshaanza programu yake ya ujenzi wa majego ya serikali kwa Unguja na Pemba. Serikali imeamua kila mwaka wa bajeti itenge bajeti kwa ajili ya kujenga jengo moja litakalokuwa na uwezo wa kukaa Ofisi moja hadi tatu. Kwa hivyo niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi walielewe hili na haya maamuzi yaliyotoka yalikuwa ni maamuzi ya serikali, na sisi kama sekta husika tutahakikisha Mkuu wetu wa Wilaya anapata pahala pa kufanyia kazi penye mazingira mazuri.

Lakini suala la kuita barabara ya Sele Manga, ningemuomba asubiri kwanza tuijenge hiyo barabara halafu jina litafuata baadae. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, mpitishie fungu lake.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza. Jana wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia suala la kituo cha KMKM kilichopo Msuka, kwamba kutokana na athari zilizopatikana na kituo kile na mvua zilizonyesha, jengo lile limekuwa ni bovu hali ambayo hairidhishi na nimeona hapa kwamba mwaka huu *Alhamdulillah* mambo yamekuwa mazuri kwenye fungu lao kipindi cha 2016/17 wamepata milioni thamanini na saba, mara hii wamepata milioni mia nane na kitu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nilitaka nijue kwanza utaratibu gani utakaotumika ili kuhakikisha kwamba majengo ya kituo kile pamoja na athari zinazopatikana zilizosababishwa na mvua kubwa yanafanyiwa kazi, yanafanyiwa matengenezo makubwa ili askari wetu walioko pale waweze kufanya kazi zao kwa vizuri na waweze kufurahia kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba jibu ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Omar Seif Abeid kwa kulileta jambo hili kwenye hotuba ya bajeti lakini pia amekuwa akiliulizia maswali mara kwa mara.

Kwanza pale kuna mambo mawili. Kuna suala la mmong'onyoko wa ardhi ambao huo kwa kupitia vifungu vyetu vya KMKM hatuwezi kuukamilisha. Isipokuwa sisi na sekta husika ya Mamlaka ya Kusimamia Mazingira

tutaliweka katika mpango wa kuweza kuhami lile eneo hili la mmong'onyoko. Suala la ujenzi wa majengo jana nimelizungumza vizuri sana na sitegemei kuwa nitakuwa na majibu zaidi ya yale.

Kwa hivyo nwaombe Waheshimiwa Wajumbe uwezo wa serikali ambao umetolewa kwa ajili ya kufanya ukarabati na yako majengo ambayo yatajengwa, tuendelee kuwa wastahamilivu na Mheshimiwa hapa jana Mhe. Waziri wa Fedha alisema kuna kamati maalum ambayo imeundwa kati ya afisi yangu na Wizara ya Fedha, kukagua maeneo yote ili kujua ukubwa wa tatizo na serikali hatimae tuweze kupata ufumbuzi.

Kwa hivyo nimuombe Mheshimwa kwamba hilo jambo tunalijua na tutalifanyia kazi na hatimae askari wetu watapata pahala pazuri pa kuweza kujistiri ahsante sana.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Jumla ndogo	1,068,400,000
Jumla Kuu	**25,720,200,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D02 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu D0201 Utawala Unguja	84,555,000
Jumla Kuu	**84,555,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D0213

Kifungu PD020101	Mafunzo kwa Vijana	7,229,383
Kifungu SD010102	Uzalishaji Mali	

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi hasa nitapita njia tu kwa sababu nilipopataka nimemkosa.

Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia nilizungumza kwa hisia sana kuishauri serikali kwa nchi ambazo tuna wigo kwenye masuala kama haya kutumia Vikosi vyetu hasa nchi kama Cambodia, Vietnam, China, Indonesia na nyenginezo hasa hizo za *Far East.*

Sasa Mhe. Waziri alipokuwa akijibu katika mafunzo yake kuna maeneo ambayo vijana wamekwenda katika maeneo ya Tanzania Bara na kwengineko na hasa katika *production* ambayo iliyozungumzwa ni katika maeneo ambayo ni ya kihistoria au nitasema ni maeneo yale kwa yale miaka nenda miaka rudi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka nifahamu Mhe. Waziri na katika maeneo ya kwenye mpango wa Sera na Tafiti ya wizara yake anajipangaje katika miaka ya mbele ili kuhakikisha kwamba vijana wetu tutaweza kuwatumia ili kuweza kuzalisha mali ambazo tuweze kuuza kwa ajili ya bei nafuu kwa Wazanzibari na Watanzania, lakini pia kuziunganisha katika soko la Afrika Mashariki.

Sasa Mhe. Waziri alipojibu alinijibu juu juu tu. Sasa mimi hapa nataka nimuelewe katika suala hili zima la uzalishaji mali. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nilimfahamu sana Mhe. Simai Mohammed Said na sikumjibu juu juu tu, nilimjibu kwa yale ambayo tuliwahi kumjibu.

Suala lake hasa hili halikuwahi kujibiwa kutokana na sababu zile zile. Naomba niwe muungwana niseme suala hili hasa, maana suala lake lilikuwa na vipengele mbali mbali, lililojibiwa hasa lile la uzalishaji na yeye alisema hana matatizo na lile eneo la uzalishaji, ana tatizo na kuona kwamba uzalishaji unaofanyika ni ule ule anataka tubadilike.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Simai Mohammed kwamba kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti tumefanya utafiti wa uzalishaji katika Vikosi vyetu vyote na taarifa hizo na programu hiyo tayari tunayo, na utafiti huo ndio ambao ulitupelekea serikali ishawishike kumpata mshauri muelekezi namna ya uendeshaji na uzalishaji katika Kikosi chetu cha JKU na Vikosi vyengine.

Kwa hivyo ushauri anaotupa kwamba ameona tunajaribu tu kupeleka vijana wetu Tanzania Bara. Kwa sasa hivi ndio uwezo ulikuwa unaturuhusu lakini tunachofanya kwa mujibu wa utafiti ule na haja ipo, tukiona tumepata nafasi ya kuweza kuwapeleka vijana wetu katika maeneo hayo kwa ajili ya kuongeza

uzalishaji, mkazo mkubwa tunataka kuuweka katika uzalishaji kwenye viwanda vidogo vidogo. Kama alivyosema Mhe. Simai Mohammed Said, useremala, utengenezaji wa magari, utengenezaji wa bidhaa za chuma na kadhalika.

Kwa hivyo hilo ni *priority* yetu, ndio maana jana tulisema kwamba tunataka serikali ikiridhia tutafute eneo maalum na uko muelekeo kwamba huenda tukapewa eneo moja pale Chumbuni kwa ajili ya kukusanya viwanda vyote vya vikosi vyetu, ili vile viwanda tuwe na uwezo wa kuweza kuvifuatilia na vizalishe kwa tija kwa maslahi ya nchi yetu.

Kwa hivyo mawazo yake Mhe. Simai Mohammed Said kwanza ni mazuri. Kwa hivyo mawazo haya tutachanganya na ule utafiti ambao tumeufanya ili tuweze kufanyakazi vizuri. Ahsante sana.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nakubaliana na mawazo aliyotoa nimeridhika na niseme kwamba sisi ma-*back benchers* tunatumia ubunifu, fikra na mawazo kuishauri serikali na majibu tunayoyapata kama haya ndio tunafurahia.

Lakini tunaomba kwamba hayo maelezo aliyotupa hapa kwamba mwaka ujao tutakapokuja ahadi yake hii aliyoitoa kwenye Baraza hili tuone maendeleo. Ahsante sana naomba tuendelee.

Jumla ndogo	90,250,000
Kifungu PD 0201 Programu Kuu kwa Mafunzo kwa Vijana	7,229,383
Kifungu PD 0202 Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa JKU	

Mhe. Hassan Hafidh Khamis: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilisema kwamba wapiganaji wetu wa Vikosi vya SMZ hasa JKU wanalalamika wakanakatwa mishahara bila ya mpango au bila ya utaratibu au kinyume na matakwa yao.

Mhe. Mwenyekiti, ninavyofahamu mimi mtu kukatwa mshahara wake iwe kwa *income tax* au iwe kwa maana ya mkopo, vyengine vyovyote iwe kwa ridhaa yake mwenyewe. Mhe. Mwenyekiti, naomba kupata majibu wapiganaji wetu wamekuwa wanakatwa mishahara bila ya mpango bila ya utaratibu hasa JKU wanaambiwa chakula, magodoro, sijui kitu gani wakiangalia mishahara yao imeshapigwa panga. Mhe. Mwenyekiti, naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi juu ya suala la Mhe. Hassan Hafidh Khamis kama hivi ifuatavyo.

Kwanza hakuna mikato wanaokatwa askari isio mpango. Mkato wa *income tax* kama alivyesema yeye, mkato wa michezo na huu ni mkato wa hiari na hili nimekuwa nikilitolea ufafanuzi kila kikao, hata mwaka jana suala hili liliulizwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Jangombe, kwamba hizi lugha hizi ambazo zinazungumzwa mimi nadhani hao ambao wanakatwa michango bila ya utaratibu Mhe. Hassan Hafidh naomba uniletee. Naomba uniletee ili tuwakutanishe na hao wanaokata kama wanakata kinyume na utaratibu tuwachukulie hatua za kinidhamu. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo iko mikato ambayo sisi wizara tumeridhia, hiyo ya *income-tax* kwa maana ya *income-tax* serikali nzima. Watumishi wote ambao wanavuka kiwango cha mshahara *amount* fulani wanakatwa *income-tax.* Mikato ya michezo ndio ninayoijua na mikato mengine ni kwa ajili ya wao wenyewe ile mikato ya maafa waliyojiwekea wao wenyewe, mtu ukipatwa na tatizo unapewa ule mchango. Sasa kama iko mengine ambayo mimi siijui inawezekana. Nitakuona sana unipe mashirikiano ili tujue tatizo na tuweze kulitatua.

Suala la mkato wa chakula. Kwanza askari wote na hili nataka niseme wako Wajumbe walisema wako askari hawashibi. Utaratibu wa majeshi yote ni kutoa *ration allowance* na madhumuni yake *ration allowance* ili ununue chakula ule usikae na njaa. Juzi nilivyofanya mkutano mkuu na askari wote kule Pemba, niilitumia nafasi hii kuwaelimisha. Askari hamli mnakaa na njaa, huo si uaskari kwa sababu serikali imetoa *ration allowance* ili mle, si nyingi lakini zimetolewa, Na jana namshukuru sana Mhe. Mohammed Said Mohammed alisema kuna hii *double payment* inawezekana. Kuna posho hili la *ration allowance* ambalo linaandamana na mshahara na kuna chakula wanachopikiwa askari wale wanaokuwepo zamu, huo ndio utaratibu unaotumika.

Lakini unapokwenda mafunzo pesa zile zinatumika kwa ajili ya kukulisha wewe kule unapokuwepo *course* na utaratibu huu unatumia na wenzetu hawa wote wa vyombo vya ulinzi na usalama, kwamba ile *ration allowance* kwa kuepuka hiyo hiyo *double payment* ndio ambayo wewe unatakiwa ule. Sasa mimi nadhani lile alilolizungumza Mhe. Mohammed Said Mohammed tutaliangalia, kwamba unapewa *ration allowance* lakini unaopokuwa kwenye zamu unapikiwa chakula hili vipi. Hili naomba tulichukuwe twende

tukalifanyie kazi tuone tunaliweka sawa vipi ama tuzidishe posho ama tuwaamue vyenginevyo.

Lakini hili la kukatwa mishahara ovyo, niseme tu Mheshimiwa naomba sana kama wapo basi waje kwa sababu mimi ndie msimamizi wa wizara hii, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa hili. Nakuomba unipe mashirikiano ili tuweze kujua hasa hao wanaofanya hivyo ni akina nani ili tuweze kuchukuwa hatua, yaani sio hawa walioleta taarifa, hao wanaowakata askari ovyo ni akina nani ili tuweze kuchukua hatua kisheria ahsante sana.

Mhe. Hassan Hafidh Khamis: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na *very polite,* kweli leo anakaimu ile nafasi kubwa ya nchi hii.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tu anihakikshie Mhe. Waziri kwamba atawalinda wale askari ambao watakuwa chambo nitawaleta kujitokeza kama wanavyokatwa, yeye atawalinda wasije wakakomolewa kule vikosini, mara kapelekwa Pemba, mara huku, ikawa tena kama mtoto wa kambo, anihakikishie tu kama atawalinda basi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nadhani jibu nilompa lingetosha, kupelekwa Pemba askari sio adhabu ni utaratibu wa kawaida kwamba unapoingia kwenye mkataba unasaini kwamba utafanyakazi popote pale katika visiwa hivi viwili. Kwa hivyo sio adhabu hata kidogo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini hili la kuwalinda. Maana hata pale Ofisini kwangu kuna walinzi, nyumbani kwangu kuna walinzi, sijui nyumbani kwake kama hakuna walinzi. Kama hakuna walinzi basi niko tayari hao watu twende tukazungumze nao huko kwake ili kuwe hakuna mtu ambaye atatoa taarifa zaidi ya mimi. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nimepokea tuendelee.

Jumla	**10,094,318,000**
Kifungu PD0202 Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa JKU	10,094,318,000
Jumla Kuu	**17,323,700,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D03 - CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu D0301 Sheria na Urekebishaji 78,051,000

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia kule kwenye suala la mapato nilimuuza Mhe. Waziri kama anakumbuka, tumeona makadirio yanakua makubwa kiasi mapato hata asilimia 30 hayafiki.

Je, kulikoni kwamba ni vigezo gani wanakadiria haya mapato hata yule ambaye hata asilimia 30 hawaifiki ya mapato. Nataka ufafanuzi zaidi kwa hili.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ripoti tunayokuja nayo ni ripoti ya mwezi wa Machi tabaani itaonekana kuna mapungufu. Kama nilivyotoa mfano jana, nilitoa mfano hapa kwenye kifungu cha KVZ kwenye mradi wa Kiwanda cha Viatu, mpaka Machi tulikuwa tumepata asilimia 3.3.

Lakini mpaka jana nazungumza hapa tulikuwa tumepata asilimia 100 na haya mapato vile vile. Mapato haya yanatokana na uzalishaji na mambo mengineyo. Kwa hivyo inawezekana pengine katika msimu wa mpaka Machi muda wa kukusanya yale mapato yenyewe unakua haujafika, lakini ukienda sasa unaweza ukapata taarifa nyengine zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo hili lisimshughulishe sana ni utaratibu tu wa kawaida hatuwezi hapa kuja kuripoti mpaka tulichokikusanya mwezi Aprili na Mei, lazima turipoti mpaka mwezi wa Machi. Kwa hivyo mapato haya huwa yanaripotiwa kwa mujibu wa kile ambacho mmekikusanya na hii ndio ripoti ya mpaka mwezi Machi. Lakini tabaani mpaka tukifika tarehe 01 Julai hatutokuwa kwenye asilimia hii ndogo, tutakuwa tumeivuka na tumefika asilimia kubwa. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, tuendelee nimefahamu.

Jumla Kuu **78,051,000**

FUNGU D03 - CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu PD0301 Programu Kuu ya Huduma za Urekebishaji wa Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo

Kifungu SD030101 Programu Ndogo ya Huduma za Urekebishaji
wa Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo 52,987,000

Kifungu PD0302 Programu Ndogo ya Uendeshaji na
Uratibu wa Chuo cha Mafunzo

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi niliuliza swali na nikataka nijibiwe, lakini sikulisikia hata kama sipo lakini ilikuwa *record* yangu inafanyakazi. Niliuliza kwenye vikosi hasa sehemu ya Mafunzo kuna maduka yamejengwa karibu 17 na maghala mawili.

Je, maduka yale yamejengwa kwa utaratibu gani, yamejengwa na nani, yanamilikiwa na nani na taasisi ile husika inapata faida gani kwa muda huu uliopo. Lakini jibu lile sikulipata kwa mujibu wa *record* yangu niliyomrikodi Mhe. Waziri wakati akijibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe nahisi swali lako halikueleweka, hebu muulize tena vizuri Mhe. Waziri.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, nilipo changia juzi nilizungumza kwamba kuna maduka yanajengwa katika sehemu za vikosi kwenye maeneo ya barabarani, pale Mafunzo na ukiendea kule JKU sijui wapi. Maduka yale yamejengwa na nani na utaratibu wake umefuatwa vipi na ile taasisi husika inapata faida gani na wamiliki ni nani waliojenga wao ama watu binafsi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakumbuka vizuri sana alivyokua akichangia Mhe. Nadir, kwanza alilalamika kama tunakumbuka, alilalamika kwamba kwenye mambo ya maana hapelekwi anapelekwa kwenye mambo yasiyo na maana, na katika mambo hayo akayajumuisha kwamba tunapelekwa kwenye maduka, kwenye kilimo na akasema mara nyengine yeye hatokwenda huko.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwanza wanao-*demand* kwenye kufuatilia kazi ni kamati na hili lilikuwa ni ombi la Kamati, waliomba na sisi tukaridhia tukawapeleka. Kwanza nataka niseme hilo.

La pili maduka yote hayo anayosema kule JKU na Mafunzo yanamilikiwa na Chuo cha Mafunzo na JKU.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ni utaratibu gani ulitumika wa kuyajenga. Ni makubaliano kati ya wapangaji na taasisi husika. Kwa hivyo taasisi husika hazikutoa *single cents* kwa ajili ya ujenzi wa maduka yale, isipokuwa wale wapangaji ndio ambao wamejikubalisha kujenga kwa makubaliano maalum na taasisi husika hizo mbili nilizozitaja. Maana hizo ndizo zenye hayo maduka.

Kwa hivyo ni kiasi gani kinapatikana kwenye maduka yale kwa makubaliano yao, kwamba kwanza inaangaliwa gharama gani ametumia yule mjenzi na wakati akijenga kulikuwa kuna mashirikiano ya pamoja kati ya ma-*engineer* wa Chuo cha Mafunzo na yule mmiliki, ili kuepusha wasi-*inflate* zile bei ambazo wanaweza wakaziingiza kwenye mkataba. Kwa hivyo makubaliano ni kwamba gharama ambazo amezitumia yule mpangishwaji, kuna makubaliano maalum, asilimia fulani anajirejeshea fedha zake na asilimia fulani zinaingia kwenye Chuo cha Mafunzo.

Sasa kuhusu kiasi gani kimepatikana, hicho naomba nimpe baadae na kwa mwezi ni kiasi gani, hicho naomba pia nitampa rasmi kwa maandishi kwa kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti. Ahsante sana.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijaridhika na jibu hata moja. Nasema hivyo kwa sababu katika aliyoyazungumza inaonekana dhahiri kwamba Mhe. Waziri hana uhakika nini anakijibu.

Mimi ninayo ripoti ya *CAG* hapa, inazungumza waliyojenga maduka 17 hii hapa, ghala 2 na majina yao Said Omar Mohamed Khatib Aboud na imeeleza ripoti kamili kwamba *procedure* walizotumia makubaliano ya wizara yake na watu binafsi hayakufikia malengo yanayotakiwa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe hatuzungumzii ripoti ya *CAG* sasa hivi, kuna wakati utafika utazungumzia ripoti ya *CAG*.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Sawa. Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini unamtetea alichokijibu sio sahihi na hii ripoti ya *CAG* alichojibu sio kweli.

Maduka kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* hawapati fungu lolote, wamekwenda kinyume na sheria katika mikataba katika ujenzi na wanamiliki hajanijibu wanapata vipi, wamepeana miaka mingapi. Mkataba unatakiwa ujibu ni miaka mingapi, alikuwa aseme tu nitakwenda kuuliza kwenye wizara yangu nitakuletea jibu. Lakini anajibu kitu hana uhakika nacho.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sikuridhika kwa jibu alilonipa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimuhakikishie nilichokisema nina uhakika nacho na kile nilichokuwa sina uhakika nacho, ndio maana nikasema nitakileta kwa maandishi. Kama ningekuwa ninasema vitu nisivyovijua hata ile kumuambia nani, bei gani ningeripua tu. Lakini sifanyi hivyo kwa kuelewa kwanza Kanuni za Baraza hutakiwi kulidanganya Baraza. Lakini ameelezea suala la ripoti ya *CAG* kwani utaratibu wa ripoti ya *CAG* ukoje.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti imeletwa hapa *PAC* wamekabidhiwa, watakwenda kufanya utafiti, wao ndio watafiti wa Baraza la Wawakilishi. Sasa tusubiri ripoti ya Kamati ya *PAC* itulete itathibitisha yaliyomo hapo, kama ni ya kweli au sio ya kweli. Ndivyo Katiba inavyosema na ndivyo Kanuni zetu zinavyosema. *(Makofi)*

Sasa mimi nadhani majibu yagu niyotoa ni ya uhakika na hayo ndio majibu na sina majibu mengine zaidi ya hayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninachosema kwamba sikuridhika wala hajanijibu ukweli.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir sijakuruhusu. Nisikilize nasemaje sijakuruhusu kusimama kusema na najua mimi kwamba hujaridhika. Lakini jawabu la mwisho la Mhe. Waziri kasema hivi, "kwamba yeye hayo aliyoyasema ana uhakika nayo". Sasa wewe kama hujaridhika subiri mpaka Kamati ya *PAC* ifanye kazi kisha uje na hiyo hoja, hakuna tena la kulumbana hapa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, nisubiri wakati sasa tunapitisha vifungu. Hii bajeti tunaipitisha nisubiri lini, wakati wizara yake itakuwa imeshapita.

Mimi nilimuuliza miaka mingapi wamekubaliana *contract* wanajenga, hata kama wamekubaliana kukatiana, ni miaka mingapi hajajibu, kiasi gani wamefaidika hajajibu, nani anayemiliki nimeuliza majina ya anayemiliki maduka yale hajataja, akatae basi na hao niliowataja kama sio waliojenga.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa tena nafasi. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilieleza *concern* yangu kuhusu fedha wanazoingiziwa vikosi vya SMZ na nilieleza *specific* kwamba nitazuia Fungu la D3 mpaka nipate maelezo ya kujiridhisha ndio niweze kuliachia fungu hili.

Mhe. Mwenyekiti, nilieleza kwamba vikosi vyetu vinafanyakazi vizuri na mfano mzuri ndio kama hayo aliyozungumza sasa hivi, wanajenga majengo mbali mbali miradi. Kwa kweli tunafurahi kwa sababu tunaona hawakukaa tu kusubiri labda wafungwa wapelekewe wakawashughulikie na mambo mengine.

Lakini katika hizi shughuli wanazozifanya kuna kuwa kuna ma-*suppliers* mbali mbali ambao wana- *supply* vifaa katika vikosi vya SMZ, hasa vile ambavyo vina taasisi za ujenzi. Lakini sasa tatizo lililokuwepo Mhe. Mwenyekiti, wanakuwa wanakopa madeni yanakuwa makubwa na kwa kupitia *OC* tulizozipitisha Mhe. Mwenyekiti, hawawezi kulipa.

Leo Mhe. Mwenyekiti, labda Waziri wa Fedha anaweza akatueleza, *OC* katika kila kikosi kila mwezi wanaingiziwa kiasi gani. Kwa mfano kila kikosi wakiingiziwa milioni 20, milioni 20 zile Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kuna mahitaji ambayo kila siku yanahitajika katika vikosi vyetu, lakini kuna *bulk* ya madeni ya miaka ya nyuma inakuwa bado hawajalipa. Sasa kwa fungu tulilolipitisha haliwezi likakidhi kulipa madeni haya na hawa waliokopwe Mhe. Mwenyekiti, ni raia wetu ni wafanya biashara.

Mhe. Mwenyekiti, *ZRB* nilitoa mfano kila mwezi kama hujarejesha *return* unapigwa *penalt*. Sasa hawa walio-*supply* vifaa zaidi ya miaka miwili au miaka mitatu watawalipa lini. Kwa hivyo mimi nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, naona simuoni hapa, tuangalie katika mafungu ya Wizara ya Fedha, tuangalie ni maeneo gani tutaweza kupata pesa. Maana yake nilijaribu kuangalia katika madeni ya ndani nikaambiwa kuna ziro katika ile bajeti ya serikali, lakini huku tayari wako watu wanadai.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa nilikuwa nataka ufafanuzi zaidi kutoka kwa Waziri wa Fedha. Je, tutaweza vipi kuweza kuwasaidia hawa vikosi maalum. Sio hiki tu cha Mafunzo, huo nimetoa mfano tu lakini takribani vikosi vyote, kwa sababu wanafunzi wako kule wanataka kula inabidi waende dukani wakachukue, wanafunzi wanavujiwa inabidi wakachukue mabati kwa sababu

hawana cha kufanya. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri wa Fedha atusaidie. Je, ataweza kutoa wapi fedha kwa ajili au yale madeni yatachukuliwa yote na Wizara ya Fedha yalipwe, ili *OC* zitakazotolewa kwa vikosi vyetu ziende zikatumike kwenye matumizi ya *PBB Current Budget.*

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kuliona hili na vile vile nimshukuru kwa ushauri na mawazo aliyoyatoa kwenye bajeti iliyopita na sisi tuliyafanyia kazi. Jana alisema kwamba sasa mambo shwari, inaonesha kwamba umahiri na sisi kama Mawaziri kama Serikali tunawasikiliza sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanachotuambia. Tunapokuwa tunakataa kitu hatukatai tu, lakini tunakataa kwa hoja na tunakubali kwa hoja vile vile. Hatukatai kwa nguvu za hoja na wala hatukatai kwa nguvu za hoja.

Kwa hivyo nimshukuru sana Mhe. Hamza amekuwa ni mshauri wetu mzuri sana katika jambo hili. Bado nataka nimthibitishie ni kweli, madeni jana Mhe. Naibu Waziri aliyataja kwa vile vikosi ambavyo tunadaiwa, na sisi Chuo cha Mafunzo tunalo deni tunadaiwa. Tunadaiwa karibu milioni 639,556,162 na *suppliers* mbali mbali.Tunakiri hilo deni kuwa nalo na anayedaiwa kama hakuchukua kwa hadaa, huwa hapati matatizo na sisi tunalikubali hili deni na tutakubaliana na wadai tuone namna gani tutaweza kuwalipa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile sisi tunadai pia taasisi na watu wengine. Tutahimizana tudai tulipwe ili itupe nguvu ya kuweza kulipa madeni ya wale watu ambao wanatudai. Kwa hivyo wazo lake Mhe. Hamza Hassan Juma tunalo na tunao wote wanao tudai na wanachotudai na sisi tunao wote tunao wadai na tunachowadai. Kwa hivyo utaratibu utafanyika ili kukusanya tunachokidai, tulipe yale madeni ambayo tunadaiwa na pale itakapobidi kwamba kwetu sisi peke yetu kama kikosi au vikosi hatutamudu basi tutakwenda Serikalini tupeleke madeni haya ili Serikali iweze kulimaliza hili tatizo la kudaiwa kwenye vikosi vyetu ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake lakini kimsingi hili suala kwa kutegemea kama anavyosema kwamba wao wawatafute wale wanaowadai halafu waweze kulipa, hili suala naona litachukua muda mrefu. Ndio maana nikashauri kwamba tuangalie yale madeni ambayo wanayodaiwa hivi vikosi, madeni haya wayabebe Wizara ya fedha ili iwe ni deni la Serikali,

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kama Kikosi cha Mafunzo wao wanasema wanadaiwa milioni 600, lakini hicho wanachodai wao, hata milioni 300 hakifiki. Lakini vile vile ukizingatia Mhe. Mwenyekiti, *OC* zao wanazoingiziwa haziwezi kukidhi haja ya matumizi ya kawaida halafu vile vile wakaweza kulipa hayo madeni.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nauliza kwani kuna ugumu gani madeni haya yakachukuliwa na Serikali. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, sikufichi mimi miongoni mwa hao ma- *suppliers* ambao wanaodai hizo bidhaa waliokopesha, anadai karibu milioni 80 *supplier* mmoja tu. Sasa hebu tuangalie Mheshimiwa Milioni 80 kwa *Supplier* mmoja, vikosi hawa pengine hizo OC zao hazizidi pengine milioni 20 kwa kila mwezi, watawalipa lini, kule wale wanaathirika biashara zinakufa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa nini hili suala lisibebwe na wenyewe Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan ilikuwa tangu mwanzo *u-declare interest* yako kwenye hilo. Sasa umesema mwenyewe Mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Niweke Hansard sawa, sio mimi ninayedai yaani miongoni mwa hao wanaodai ni raia wangu ambaye yuko ndani ya jimbo langu ambaye yeye ni *Supplier*. Kwa hivyo naomba *Hansard* irekebishwe mimi sio katika hao *ma-supplier*.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa nafikiri *Hansard* tayari imeshakaa sawa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba niongeze majibu mazuri yaliyotolewa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kama alivyosema upo utaratibu wa ndani wa kushughulikia madeni sugu na suala la madeni Mhe. Mwenyekiti, haliko kwa Wizara hii, madeni yapo katika Wizara mbali mbali madeni ya ndani. Hata sisi Wizara ya Fedha tuna madeni ya ndani. Na utaratibu kwa kila Wizara ni kutizama mbinu yake ya kulipa madeni hayo. Kwa sababu tunachosisitiza sana ni kwamba Wizara na Taasisi za Serikali zitumie kwa mujibu wa makisio yao yalivyowekwa katika bajeti zao.

Sasa wakiwa wanakwenda nje ya hapo, ndio kunakuwa na matatizo ya kutolipa na haya madeni inavyoonekana ni madeni ya muda mrefu. Kwa mfano taasisi

nyingi Mhe. Mwenyekiti, zilikuwa zinadaiwa na *ZECO*, madeni mengo na ya muda mrefu lakini Serikali baada ya kuona uzito wa taasisi hizo kulipa, madeni hayo hivi sasa yamechukuliwa na Serikali.

Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Hamza, haya ni madeni ya ndani tuwaachie Vikosi wakiona yamewashinda basi upo utaratibu wa kuyarudisha Serikalini na sisi tutayapokea na tutayaangalia na kuona uhalali wake na uwezo wetu wa Serikali tutalipa taratibu kadri hali itakavyoruhusu. Lakini kwa sasa bado tuwaachie Vikosi ni madeni ya ndani sawa sawa na Idara nyengine ambazo zinakuwa na madeni ya ndani wana taratibu zao za kulipa madeni hayo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti kwa kweli hili suala bado ni gumu na suala ni gumu kwa sababu kwa inavyelekea hawa ambao ma-*supplier* wanaoidai vikosi vyetu na *specific* hichi ninachokizungumza Chuoa cha Mafunzo, bado wataendelea tena kusota na kuweza kupata hizo pesa zao ambazo ni sehemu ya mitaji ya biashara zao.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ili niruhusu tuendelee nitamuomba Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii inayoshughulikia Wizara hii, wajaribu wanapokwenda kwenye Kamati, wakae na watendaji wa Vikosi vyetu na kuyaratibu yale madeni yote ambayo ma- *suppliers* wanadai na Makamanda wetu watoe maelezo, yepi wataweza kuyalipa na waliyokuwa hawawezi kuyalipa ili yaweze kupelekwa Serikalini kwa haraka ili hawa wananchi wetu waweze kulipwa ili waendelee na biashara zao.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili nitaendelea kulifuatilia ili kuona ni mashirikiano gani baina ya Kamati na Wizara husika na Wizara ya Fedha ili kuondoa huu mzigo mzito ambao hata Makamanda wetu kwa kweli hivi sasa hivi unawapa tabu katika kufanya shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Bado tumesimama tuangalieni na sisi huku.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub nakuuliza unasemaje?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Eeeh! nipo hapa hapa Mhe. Mwenyekiti, mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku upo kwenye fungu hili, sawa endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti cheo ni dhamana na tutakwenda kuulizwa na unaambiwa unavyolikuta ovu tumia mkono mdomo wako mwanzo, ukishindwa mkono wako la pili, la tatu lichukie katika nafsi yako.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka ufafanuzi kidogo, sababu gani za wanafunzi hasa Makunduchi kupelekwa kwa gari za abiria. Mafunzo wanafunzi wanawapeleka Mahakamani kwa gari za abiria ni sababu gani za msingi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku unakusudia Mahabusu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ndio Mahabusu au wafungwa lakini ndio hakipendwi Kiswahili hicho kutumika wale Mahabusu wanapandishwa gari za abiria.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku hili suala ulilichangia katika mchango wako au ulililiuliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa bahati mbaya muda ulikuwa sio rafiki hata moja hakuwahi kunijibu.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa utaratibu Mhe. Jaku unaujua, utaratibu suala lazima au kama ulipeleka kwa maandishi Mhe. Waziri hawezi kujibu suala ambalo wewe hukulichangia, kama umepeleka kwa maandishi, kama hujalichangia hapa haliwezi kujibiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa nimelichangia dakika zangu tano nilizopewe nilikwenda mbio mbio.

Mhe. Mwenyekiti: Hili hana taarifa nalo kwa maana hiyo hukulichangia.

	JUMLA	**14,075,513,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU PD 0302	Program Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Chuo cha Mafunzo	14,075,613,000
	JUMLA	**14,128,600,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D 04 - KIKOZI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO.

Fungu D0401	Utawala Unguja	39,025,000
	Jumla Kuu	**28,815,400,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PD 0401	Program kuu ya ulinzi na Uzuiaji wa Magendo	1,328,500,000
Kifungu PD 0402	Program Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo	

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mwenyekiti, katika hili nilichangia kule kwenye utumishi wa umma lakini bahati mbaya ikawa sijalipata nimekuja katika Kikosi hichi cha KMKM juu ya ile kadhia iliyozungumzwa ya wale wafanyakazi, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, lakini hakuna aliye juu ya Katiba ya Zanzibar. Mhe. Waziri aliapa kulisimamia hili hata *Commodore* anayesimamia hii.

Mhe. Mwenyekiti, Ibara ya 118 ipo pale utumishi wa umma, nafikiri hii haikutendewa haki, kuna maagizo yalitoka ya Utumishi wa umma wale watu warudishwe kazini na kweli wale watu wamerudishwa kazini, lakini mpaka dakika hii bado hawajapokelewa na Kikosi cha KMKM watu watatu ambao mpaka dakika hii mshahara wao tokea mwezi wa Disemba mpaka leo hawajapokea.

Nitaomba sana Mhe. Mwenyekiti, ijapokuwa Mhe. Waziri kasema hili jambo atalichukulia busara, katika Katiba hakuna aliye juu ya busara. Katiba imeshaeleza na hata Sheria ya Utumishi wa Umma Na.33 ina maamuzi hayo, imempa nguvu hiyo, kwamba uamuzi wa Tume katika Kamisheni hauhojiwi na taasisi yoyote wala na mtu yeyote. Kamisheni imeshatoa maelekezo, Utumishi wa Umma umeshatoa maelekezo.

Hapa hapahitaji nguvu za kutumia busara kwa Mhe. Waziri isipokuwa Waziri hili jambo ijapo itakuwa tatizo kulisema kwenye *public* kama hapa, kwa sababu mambo ya utendaji. Je, atakuwa yuko tayari mimi na watu wawili watatu akatupa hii siri kwamba lini wale watu watarudishwa kazini.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli huwezi kutumia busara ukavunja Katiba na ukavunja Sheria. Na ndio maana nilivyokuwa nikijibu nimesema kwanza tukubaliane sote kwamba hawa watu wamevunja sheria na sheria hata kama ina mapungufu, kama haijarekebishwa hiyo ndio sheria.

Nadhani nimeeleweka na ndivyo niliviyosema kwamba kwanza hawa watu wamevunja sheria, hoja zinakuja sheria ina matatizo, ndivyo ilivyo, ndio sheria. Na nilisema kama kuna jambo limekosewa, kuna taratibu lazima zirejeshwe zifuatwe, nilisema hapa Mhe. Abdalla Maulid Diwani sijui kama ulikuwa ukinisikiliza na nikasema hawa ni watumishi wa KMKM, kuna ngazi zilipaswa zifuatwe kabla hatujafika huko kwenye Tume ya Utumishi ya Idara Maalum.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme Kamisheni ya Utumishi wa Umma haijatoa maamuzi kuhusu jambo hili, wewe ume-*quote* kifungu Na.118. Lakini nataka nikwambie hiyo Sheria ya Utumishi wa Umma nimeileta mimi hapa. Wewe angalia nyuma huko utaona Waziri gani kaileta hapa.(*Makofi*).

Kwa hivyo miongoni mwa Sheria ambazo ninazijua vizuri ni pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma. Kwa hivyo sheria zilizokuwepo ni hizo na nikasema, Kamati ya Katiba na Sheria na Idara Maalum ilituita sisi kama ni kamati inayoshughulikia sekta yetu, ile kukubali tu Kamanda kuja mbele Kamati ni busara. Sasa hata kama tunaitwa tusitumie busara hiyo, hata kama tunajua kwamba kuna sheria imevunjwa. Mimi nadhani sio sahihi wakati mwengine unapotaka kufanya hayo maamuzi ya kisheria ni vizuri pia busara, maana yake ni kusikiliza. Kwa hiiyo sisi tulitumia nafasi ya kuwasikiliza hawa ambao wamekutwa na kadhia hii. Hiyo ndio busara tuliyoitumia.

Na busara pia ya kuitumia kutaka kujua waliochukua hatua wamechukua kwa misingi gani, hizo ndio busara ambazo mimi kama Waziri ninazitumia, si busara ya kuvunja Katiba wala kuvunja Sheria. Sasa niliwaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi jana kwamba kwa sababu hili sasa lipo kwangu, niliomba tu tutumie busara ili nilijue undani wake na taasisi zinazohusika ziweze kuchukua hatua.

Sasa mimi nimuombe sana Mhe. Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Jang'ombe, bwamkwe wangu, nipo katika kulinda Katiba, nipo katika kulinda Sheria, nipo katika kulinda Kanuni. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nadhani na ndio kiapo nilichokula hata siku moja sitakwenda kinyume na Katiba hii, wala sheria zilizopo. Namuomba Mheshimiwa kwa hili tusifungue kondoo ndani ya

boksi hapa kwa sababu ufumbuzi wa hili si hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi, naomba sana.(*Makofi*).

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maombi ya bamkwe nayaheshimu sana. Lakini nataka kulithibitisha Baraza hili nilizungumza nyuma kwamba wengi hawakunielewa kwamba mimi siko katika wale waumini wa yale mambo niliyoyazungumza pale, mimi naamini zaidi Katiba na Sheria. Naomba kunukuu, halafu nitajenga hoja yangu.

Ibara ya 118 ya Katiba ya Nchi hii inasema:-

"Bila ya kuathiri masharti ya Katiba, Tume ya Utumishi zilizotajwa ndani ya Katiba zitakuwa na mamlaka yafyatayo:

Kuna mambo manne yametajwa. Moja wapo ilikuwa kazi ya hiyo Tume kusitisha au kuachisha utumishi wao, sio kikosi wala sio sehemu ni tume kwa sababu inayoajiri ni Tume.

Kwa hivyo wale waliachishwa na Kikosi. Je, hii hapa haionekani kama imevunjwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Maulid Diwani hapa kuna picha ninaipata mimi kama Mwenyekiti, ni kwamba hatushughulikii sana vifungu vya makadirio. Hilo limekuwa ni tatizo kubwa sana, badala yake tunashughulikia maelezo na utekelezaji wa mambo. Tunatakiwa tuingie kwenye vifungu. Hicho kinahusiana na nini na kifungu kuna fedha zozote ambazo zinataka kupitishwa hapa kwa kifungu hicho.

Mhe. Waziri ameelezea vizuri sana. Hatuhusiki hapa na hiyo Katiba ambayo unaizungumza lakini tunahusika zaidi na vifungu vya bajeti ya Wizara hii. Twende kwenye hoja za vifungu. Waheshimiwa mnatoka kwenye hoja za vifungu mnaingia kwenye hoja nyengine ambazo hazihusiki, tukataa mpaka kesho hapa.

Nakuomba sana Mheshimiwa tuwachie tuendelee na hoja ya vifungu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote nafikiri kifungu changu mimi kilikuwa ni suala la Utawala wa Kikosi cha KMKM na Uendeshaji, na hayo mambo ni mambo ya Utawala. Hapa hatuhesabu pesa ni utawala ni kuratibu shughuli nzima za jeshi hili. Nafikiri nilipokamata mimi

ndipo sawa sawa. La kama nyinyi mnalazimisha kwamba hivyo sivyo basi *Bismillahi* tuendelee. Lakini mimi nimesimamia hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tunaendelea kwa sababu hizo ni huduma za utawala hazihusiani na hilo unalolizungumza wewe. Tunaendelea.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Jana nilipokuwa nikichangia nilieleza hapa kwenye ujenzi wa vituo vya uokozi na uzamiaji. Nilizungumza kwamba kule Ndagoni katika jimbo langu mara kwa mara tunapata maafa yaani ya watu wanaokwenda kuvua na watu wengine yaani huwa tunaokota maiti mara kwa mara. Nilitaka kujua hapa wakati mwengine tunapiga simu KMKM pale Tundauwa nikaambiwa kwamba hakuna mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, nitaka kujua ni lini kwamba kule Ndagoni kuwekweakituo maalum cha uokozi ambacho watu wakitokewa na tatizo lile ili waweze kukabiliana nalo. Pia vile vile waweze kuwapatia mafunzo ya kutosha wale KMKM wakati linapotokea tatizo ili kukabiliana na masuala haya.

Naomba Mhe. Waziri apate kunipa majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikijibu hoja hii ya suala la uokozi, nimejibu kwa jumla na nilidhani Mhe. Suleiman alinifahamu. Suala hili ndani ya bajeti hii tuna mpango wa kununua boti mbili za uokozi ambazo fedha zake zimo ndani ya bajeti hii. Lakini kuweka boti ya uokozi na kituo cha uokozi kila Shehia, uwezo huo hatuna. Lakini katika Mkoa wa Kusini kipo kituo cha uokozi pale Mkoani na nimesema tutanunua boti yenye uwezo wa kwenda *nautical mile* 60 kwa saa.

Mhe. Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba tutakapofikia huko na tatizo la Mhe. Suleiman popote pale katika Kisiwa cha Pemba tutakuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Masuala mengine ya mafuta hakuna, hayo ni masuala ya kiuendeshaji, nadhani tutayazingatia kwa uzuri zaidi. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa maelezo mazuri ya Mhe. Waziri. Kwa hivyo mimi nimuombe tu Mhe. Waziri kwamba zaidi ni kweli kama kuweka kwa kila Shehia haiwezekani. Lakini zaidi ni kuangalia kwenye hayo mafuta ya kutosha ili kuhakikisha kwamba likitokea tatizo waweze kukabiliana nalo. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee.

	Jumla ya Programu ndogo	23,486,900,000
Kifungu PD0402	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia magendo	23,486,900,000
	Jumla Kuu	**24,815,400,000**

(Vifungu vyote vilivyotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGUD05 - KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu D0501	Utawala Unguja	52,034,000

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir unachelewa endelea na hoja yako.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimegonga mwanzo kabla ya ndio. nafikiri usiwasikiliza mambo hayo, kwa sababu wanafanya makusudi.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea na hoja yako.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niliuliza suala na katika kuchangia kwangu nilitaka kujua zile *fire* za *Airport* mbili walizonunua Wizara husika za bilioni tatu na milioni mia nne karibu kwa *fire* mbili, sikuridhika nazo kama Mjumbe wa Kamati. Nilipokwenda kwenye kutembea nilizunguka kwenye zile *fire* sikuona kabila katika *body*, nikaambiwa injini ya katapila lakini katika *body* hakuna kabila.

Mhe. Waziri katika majibu yake ya jana katika nilivyomrikodi kasema kwamba ina kabila. Mimi nilichojibiwa na Wizara husika nilipokwenda kama Mjumbe wa Kamati kwamba gari zile zimenunuliwa Dubai. Sasa Dubai kuna kiwanda gani cha gari anijibu kana anaijua Dubai sana. Lakini nikaomba kama Mjumbe wa Kamati kwa niaba ya Kamati nilitewe *specification* na bei na mikataba tuone kama kamati, haikuletwa tumekuja kujibiwa kwa mdomo na kama kuna *document* ataje kapewa nani katika Mjumbe wa Kamati. Kwa sababu kama ni hivyo hata *CAG* anapokwenda sehemu akijibiwa kwa mdomo atakuwa hana *any evidence*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli lile jibu sikuridhika nalo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir unajua tuko wapi. *(Vicheko)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwenyekiti, hapa...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir, tupo kwenye mapato. Sasa hayo yote bado, bado Mhe. Nadir.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, hofu yangu usije ukanipitisha.

Mhe. Mwenyekiti: Sikiliza Mhe. Nadir, tunakwenda kwa utaratibu, hatuendi tu kwa sababu una ajenda fulani lazima ikifika pahala unaisema. Hapa tupo kwenye mapato tunataka kupitisha vifungu vya mapato.

Mhe. NadirAbdulatif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, hofu yangu ... Haya ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea.

Kifungu D0501	Utawala Unguja	52,034,000
	Jumla Kuu	**52,034,000**

(Vifungu vyote vilivyotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU PD0501 - Programu Kuu ya Utoaji wa Huduma za Zimamoto na Uokozi

Kifungu SD0501 Programu Ndogo za Utoaji Huduma za Zimamoto na Uokozi

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mhe. Nadri hoja yako unaweza kuileta.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi narudia tena. Mimi ni Mjumbe wa Kamati. Sikuridhika kwa manunuzi hasa hali halisi ya zile fedha zilizotumika bilioni tatu na milioni mia nne kwenye *fire* mbili. Mimi wakati nimefanya uchunguzi wangu hazifikii kiwango hicho.

Baada ya hapo nikaizunguuka ile gari nikaikuta *body* haina kabila, sio tatizo. Lakini injini katapila. Injini katapila inatengenezwa Marekani, *body* imetengenezwa Dubai, wakati Dubai hakuna kiwanda cha gari.

Mimi niliomba *specification* kwa niaba ya Kamati, nikaomba vielelezo havikuletwa, tumeletewa majibu ya mdomo. Sasa mimi naomba majibu halisi atupe ukweli wa gari zile hazifiki thamani ile. Zipo *fire fighters* zinafika hata Dola milioni tatu lakini sio zile kwa thamani ile. Ndiyo maana mimi nikasema sitaki kwenda kurandishwa kwenye mihogo na samaki, nataka nione vitu vyenye fedha. Mimi ni Mheshimiwa siwezi kupelekwa kwenye mabonde ya mihogo na samaki.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hiyo ni moja katika kazi yako, pahala popote ambapo mnapelekwa mnakubaliana na Kamati utakwenda. Hiyo ni moja katika kazi yako, siyo kutizama tu wapi kimenunuliwa hiki na wapi kina *mark* hii, hapana. Ujue kwamba umeapa na umekula ahadi kwamba utatekeleza yale ambayo utapewa kama ni kazi yako ya Uwakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme kwamba mimi namtambua kuwa yeye ni Mhe. Mwakilishi, amechaguliwa na wananchi wa Jimbo la Chaani. Na mimi Waziri vile vile ni Mwakilishi, nimeifanya kazi hii ya kuwa Mwenyekiti wa Kamati karibu miaka 13. Kamati zote hizi ambazo zinafanya kazi Baraza la Wawakilishi ukiacha Kamati inayohusika na Masuala ya Uwezeshaji na Wanawake ndiyo sijaifanyia kazi. Lakini zote kwa jumla zinabadilika tu majina mimi nimezifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimthibitishie Mhe. Nadir kwamba mimi utaratibu wa Mjumbe kufanya kazi kwenye Kamati nauwelewa vizuri sana, wala asiwe na wasi wasi. Ndiyo maana nikasema kama ulivyosema Mwenyekiti kwamba Kamati inafanya kazi. Sasa kama mtu mwenyewe hutaki kwenda kuangalia jambo kwenye Kamati, hilo ni jukumu lako wewe mwenyewe. Lakini mimi nadhani hilo umeshalitolea maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, jana nimesema hapa magari yote yana kabila na tumefuata *specification* na ndio maana serikali tukayapokea. Kusingekuwa na *specification* tusingeyapokea. Suala aliloli-*raise* kwamba Dubai hakuna kiwanda cha kutengeneza magari. Mimi nadhani anajua utaratibu wa Kampuni zinazounda zana hizi ama magari, boti, meli, zinakuwa na matawi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano kuna Kampuni ya DAMI inafanya kazi ya kutengeneza boti. Makao Makuu yake yapo Uholanzi. Lakini kuna nchi nyingi ambazo wana *branch* na wana *assemble* kwa kutumia jina lile la ile Kampuni ilipo. Kwa hivyo kutoka Dubai na yeye ni mfanyabiashara ningeelewa kwamba jambo hili angelielewa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la bei aah! sasa sisi zilijitokeza karibu Kampuni 13, tukachagua kampuni ambazo tumeziona, tumeridhika na bei yake. Mimi nadhani Mheshimiwa kazi ya *spesification*, kazi ya kwamba hajaridhika na bei, hiyo kazi sidhani kama ataifanya hapa Barazani. Kuna utaratibu wa kiserikali uliowekwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana mamlaka. Yeye kishasema kwamba hakuridhika, amuachie Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu aende akafanya kazi hiyo, halafu ripoti atakayoileta hapa tutaipa *PAC* itaweza kufanya kazi. Sasa kama yeye hajaridhika, sisi tulio wengi tumeridhika na hilo jambo, serikali imeridhika ndiyo maana ikakubali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo suala la kutoridhika wala mimi simlazimishi kwamba aridhike au asiridhike, aendelee asiridhike maisha. Lakini utaratibu wa kiserikali utafanyika ili kama kuna ubadhirifu, kuna nini utajulikana baadae.

Mhe. Mwenyekiti naomba niseme hilo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri nimemfahamu vizuri Mhe. Waziri na ndio maana nikasema kwa lugha nyepesi kabisa, siyo kwamba nakataa kwenda kwenye mabonde lakini hivi vitu vya maana hatuonyeshwi na haya ndio madudu yanayofichwa na unamsikia anavyojibu. Lakini tuendelee lakini mimi si-s*upport* bajeti hii nzima.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadiri ningekushauri kwa kuwa una haki kama Mhe. Mwakilishi ya kutaka hayo ambayo umeyauliza, unaweza kuomba kwa kupitia Baraza la Wawakilishi. Haki hiyo unayo, unaweza kuomba na unaweza kupatiwa. Lakini isitoke hapa, kuna utaratibu maalum ambao unaweza kuufuata na ukapata hizo *specification* kutoka kwenye Wizara ya Mhe. Waziri.

Nafikiri hilo linaweza likafanyika.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri jibu lake umemsikia kwamba nikitaka nisitake wamesharidhika. Na mimi nawambia mimi sijaridhika waachie waridhike wao wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea**.** Mhe. Jaku ukigonga mara moja nakusikia na nakuona mimi ujue niko mbele wewe uko huko, kwa hivyo nakuona.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi hunioni, msema mkweli mpenzi wa Mwenyezi Mungu. Nimeshainuka mpaka amekushitua Katibu.

Mhe. Mwenyekiti: Aah! kama kugonga...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa tuwache huko tusilumbane.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku ina maana kama umegonga na sijakuchagua, ina maana sijataka kukuchagua wewe kuna wengine pia wapo. Ndiyo maana yake. Usilazimishe kila saa nikunyanyuwe wewe Mhe. Jaku. Hiyo haiwezekani. Wote humu mnahaki sawa, nimeshakuchagua mara mbili na hii sasa hivi ya tatu unalalamika nini. Tunaendelea, sitaki kaa chini, sitaki kaa chini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Utaratibu Mhe. Mwenyekiti, ni watu watatu, huyu ndiyo wa kwanza, mimi wa pili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub nitakutoa nje. Tuendelee.

Kifungu SD0501	Programu Ndogo za Utoaji Huduma za Zimamoto na Uokozi	386,001,000
Kifungu PD0501	Programu Kuu ya Utoaji wa Huduma za Zimamoto na Uokozi	**386,001,000**

(Vifungu vyote vilivyotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU - PD0502 PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu SD050201	Programu Ndogo ya Uwendeshaji na Uratibu wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mimi hapa sina makubwa, nilikuwa nataka nimsaidie Mhe. Waziri kuweka *Hansard* sawa, wakati anatoa maelezo yake Wajumbe walitaka kujua pia suala la kwamba namba ambazo zinazotumika wakati wa *emergence* au pale yanapohitajika

magari kufika hasa ya *fire* katika maeneo na Wilaya tofauti. Alisema kwamba namba zipo katika vituo na atazitoa, lakini nambari husika ambayo inayotumika na uokozi au *fire rescue* ni nambari 114.

Sasa ningemuomba Mhe. Waziri ili kuweka *hansard* sawa aitambue hiyo namba na ili wananchi wanaotusikia wapate kujua.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli alivyokuwa akitoa mchango wake ufafanuzi niliutoa bahati nzuri yeye keshaanza kuitaja Namba 114 ndiyo namba yetu ya Zimamoto pale wananchi wanapotaka huduma hii. Nilichosema mimi inapendeza zaidi kama utawasiliana na kituo kilicho karibu, unaweza ukawasiliana namba hii lakini pia unaweza ukawasiliana na kituo kilichokaribu ili ile huduma ikafika kwa haraka.

Lakini ninakubaliana na yeye kwamba namba ya Zimamoto ni 114. Namshukuru sana Mhe. Simai kwa kutukumbusha hili, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea....

Jumla ya programu ndogo hii ni		7,274,499,000
Kifungu PD0502	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Zimamoto na Uokozi	7,274,499,000
Jumla Kuu		**7,660,500,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D06 - KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu D0601	Utawala Unguja	
	Jumla ya kifungu hiki	45,530,000
Jumla Kuu		**45,530,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D06 - KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu PD0601	Programu kuu ya Ulinzi wa Nchi, Raia na Mali zao

Kifungu kidogo cha SD060101	Programu ndogo ya huduma ya Ulinzi	5,000,005
Kifungu PD0601	Programu Kuu ya Ulinzi wa Nchi, Raia na Mali zao	505,000,000
Kifungu PD0602	Programu kuu ya Uendeshaji na Utawala wa Kikosi cha Valantia	
Kifungu SD060201	Programu ndogo ya Usimamizi na Utawala wa Kikosi cha Valantia	9,683,400,000
Kifungu PD00602	Uendeshaji na Utawala wa kikosi cha Valantia	9,683,400,000
Jumla kuu		**10,188,400,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D07 - MKOA WA MJINI/MAGHARIBI

Kifungu D0701	Programu kuu ya Mipango na Sera	45,530,000

Mhe. Abdalla Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipochangia nilitoa ushauri wa baada ya kuvunjwa pale makontena nikasema je, inaonaje Serikali yangu kupitia Manispaa isitengeneze pale *temporary parking* kwa uhaba wa *parking* watu wanaoenda zao *Stone town* kule kwa matatizo, ili mpaka watakapokuwa tayari wajenzi wao wawambie wale watu waondoke. Kwa sababu sasa hivi kwamba kuelekea bandarini ni usumbufu hakuna sehemu ya *parking*, lile eneo sasa hivi liko wazi tu kama kikosi kisichokuwa rasmi kimefungwa. Hili sijapata jibu naomba sana Mhe. Waziri kwa hili halafu tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa muangalie ni wapi munauliza swali. Hii ni sehemu ya mapato Mhe. Abdalla Diwani.

Mhe. Abdalla Diwani: Na hiyo *parking* pia mapato aitowe inaingiza, ndio maana nikauliza hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Lakini hoja yako haiko hivyo. Nitamuachia Mhe. Waziri ajibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwanza kwa kutuelekeza kwamba tuulize masuala kwenye ile sehemu husika. Hapa ni kuingiza mapato na amesema sehemu ya *parking* lakini mpaka sasa hatujalifanya kama ni eneo la *parking.* Kwa hivyo haliwezi kuingia hapa.

Lakini kwa sababu huko mbele usije ukanipigia buti tena, naomba niseme kwamba ushauri wake tunauchukua tunakwenda kuufanyia kazi, tukiona kuna muda wa kuweza kufanya hilo ambalo umetushauri basi hatuna tatizo nalo hili. Lakini tukiona tumebanwa na muda wa utekelezaji, hilo jambo hatutoweza kulifanya.

Lakini nitoe ufafanuzi tuu kwa lile ulolichangia la kusema kuna gari kubwa pale na vijana wamekaa ,wale vijana wamekaa pale kwa madhumuni ya kupambana na watu wabishi wasifanye biashara pale, ndio lengo lenyewe.

Lakini itakapofika pahala ile kazi iliyokusudiwa na wamekaa pale kwa ajili ya kulilinda lile eneo lisitumike kwa matumizi mengine zaidi ya yale ambayo Serikali imeyapanga. Kwa hivyo hawapo pale kwa sababu ya jambo jengine lolote na ndio maana umewaona wamekaa, wao wanamsubiri yule ambaye atataka kwenda kutumia nje ya yale matumizi ambayo Serikali imekubaliana kuyafanya. Lakini ushauri wako tunauchukua.

Ahsante.

Jumla ya kifungu	45,530,000
Jumla Kuu	**45,530,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kama tunavyoona muda wetu unakaribia kumaliza na bado kuna vifungu kama vitano ambavyo hatujamaliza. Kwa hivyo ningeomba sana ningemuomba Mwanasheria Mkuu atengue kifungu cha Kanuni ya Muda ili tuweze kuendelea na shughuli yetu na kuimaliza mchana huu wa leo. Mhe. Mwanasheria Mkuu karibu.

KUTENGA KANDO KANUNI YA MUDA

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru nadhani Waheshimiwa Wajumbe wanatambua ukishaanza kuingia kwenye Kamati ya Kupitisha Bajeti huwezi tena kuahirisha, inabidi tuendelee mpaka tumalize. Kwa msingi huo Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja ya Kutenga Kando Kanuni ya Muda ili tumpe fursa Mhe. Waziri na Wajumbe wa Baraza kuweza kupitisha vifungu vya bajeti hii mpaka hapo tutapomaliza.

Kanuni ya 23 (4) ndiyo Kanuni ya Muda. Kwa hivyo naomba kutenga kando Kanuni hiyo ili tuendelee mpaka hapo tutapomaliza. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mwanasheria Mkuu ameshatowa hoja ya kutenguwa Kanuni ya muda kwa hiyo niwaulize Wajumbe waliokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, Waheshimiwa msiwe wabishi. *(Makofi)*

Nauliza tena naomba Waheshimiwa tumeshaanza Mhe. Mwanasheria Mkuu amesema kwa kuwa tumeshaianza hii tuimalize leo. Nawaomba sana msiwe wabishi nimewaona kuna wengine hawataki lakini nauliza tena, wanaokubaliana na hoja hii wanyooshe mikono, waliokubali wameshinda tunaendelea. *(Makofi)*

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU D07 - MKOA WA MJINI/MAGHARIBI

Kifungu PD0701	Programu kuu ya kuimarisha shughuli za Serikali katika Mkoa
Kifungu SD 070101	Programu ndogo ya kuimarisha za Serikali katika Mkoa

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti nikushukuru wakati nikichangia nilichangia juu ya suala zima la Masheha, nikawa na *concern* mbili tofauti. C*oncern* moja juu ya ucheleweshwaji wa uteuzi wa Masheha na kupelekea matatizo makubwa katika majimbo yetu, tunafanya kazi katika maeneo ambayo hatuyaelewi kama yetu ama si yetu. Kwa sababu katika jimbo langu kuna Shehia mpya iliyotangazwa ya Mapinduzi.

Shehia hii baada ya kutangazwa ya Mapinduzi kwa mujibu wa mipaka, inakuwa jimbo la Shaurimoyo. Sasa sielewi nani afanye huduma, ama afanye Kwahani, ama afanye Shaurimoyo. Kwa sababu mipaka imeshatangaziwa Masheha hakuna. Nikasema kadhia hii ni tatizo na muda umekuwa mrefu, karibuni tangu tumemaliza uchaguzi mwaka mmoja na miezi mitatu.

Lakini ya pili nilikwenda katika suala la ugonjwa na sikutaka kuwataja na si vizuri mimi kuwataja lakini tuna Masheha wengi wagonjwa. Sheha wa Amani yuko kitandani, Sheha wa Mkele yuko kitandani. Na kwa mujibu wa utaratibu Sheha ndio anliyekula kiapo cha utendaji wa kazi na ndio mwenye bendera katika eneo lake, ingawa Sheria inampa mamlaka ya kuwa na Wajumbe kumi wa Baraza la Sheha. Sasa lakini wakati ananijibu Naibu Waziri aliniambia Mkoa wa Mjini/Magharibi ni nyeti. Masheha wanakuwa na kazi nyeti. Mimi ninataka nimueleweshe kwa sababu mwenzangu ana awamu ya kwanza ya uongozi ndani Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kabla ya kuwa Mwakilishi, nimekuwa Diwani miaka kumi lakini mwaka 1997 niliteuliwa na Sheha Kwalimsha Shekhe Shafi, kuwa ni mjumbe wa Baraza la Sheha. Sasa majukumu hayo nyeti ya Sheha nayafahamu na ndio maana ninapofika pahala tukimuona Sheha anazembea kufanya mambo nyeti, tunamzuia baadhi ya kazi na tunazikaimu kwa watu wengine.

Sasa huu unyeti anaosema yeye ambapo mimi nilikuwa mjumbe wa Baraza la Sheha mwaka 1997 mpaka mwaka 2000 ambapo sifa nzuri zikanipelekea kuwa Diwani, ni unyeti gani huo unaotupelekea mpaka sasa hivi tunashindwa kuyafanya haya masuala kuyarekebisha.

Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo la kuzuwia fungu. Mimi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri kwa sababu nimeshafuatilia kwa muda mrefu na nimefuatilia katika kuondosha migongano baina ya jimbo na jimbo. Sasa hili mimi limenigusa pande mbili. Nina mgongano Makadara na Mitiulaya, nina mgongano Mapinduzi na Mkele juu.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri aniambie kwamba jambo hili halitochukua muda mrefu tutaondosha hii kadhia, lengo na dhamira ni kuwatumikia wananchi. Katika maeneo haya wananchi utumishi wao hautekelezeki vizuri.

Ninakushukuru Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nichukue nafasi kumshukuru Mhe. Ali Salum Haji Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Kwahani Mnadhimu wetu wa Chama cha Mapinduzi ndani ya Baraza.

Na ninataka nikubaliane naye kwamba uongozi wa Shehia anaujua kwa sababu ya yale maelezo ambaye yeye mwenyewe ameyasema, na mimi nathibitisha hilo kwa sababu na mimi ni muhusika katika maeneo haya ya Wilaya ya Mjini katika uongozi katika kipindi kirefu kidogo, walio wengi wanajua.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ninataka niseme kwamba ni kweli tatizo la Masheha limekuwa ni la muda mrefu na tumekuwa tukipokea maoni na changamoto zilizopo katika utendaji wa Masheha. Hivyo hatuna budi kuwa makini sana katika uteuzi huu wa Masheha na tayari mapendekezo kutoka kwenye Shehia husika, Wilaya husika, Mkoa husika yameshakuja kwenye meza yangu. Na mimi tayari nimeshayaidhinisha, yaani nimeshakubaliana nayo baada ya kukamilika utaratibu wa kufanya mambo mengine ya *vetting* kutokana na tuhuma na mambo mbali mbali tuliyoyapata ilibidi tuwe makini sana katika kuteuwa Masheha katika kipindi hiki. Kwa hivyo si muda mrefu ndani ya mwezi huu Mhe. Mkuu wa Mkoa atawatangaza Masheha wapya. *(Makofi)*

Lakini jengine kuhusu mkanganyiko wa mipaka. Mimi najua kwamba mamlaka ya utawala ndiyo yenye mamlaka ya kutangaza mipaka ya kiutawala na mipaka hiyo tayari imeshatangazwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali. Mhe. Rais aliidhinisha kuitangaza na mimi nikiwa Waziri ninayesimamia sekta hii nikaitangaza. Kuna jambo la kiufundi lilitokezea, tunawasiliana na sekta husika ifuate utaratibu ule ule ambao Mhe. Rais ameipanga ile mipaka ya kiutawala.

Sasa sitaki kusema hapa kwa sababu kuna mamlaka nyengine ambazo zinahusika na jambo hilo tayari mamlaka hizo tumekaa nazo ili turejeshe ile mipaka ambayo Mhe. Rais ameipanga kama ni mipaka ya kiutawala.

Zaidi ya hayo naomba Mhe. Mwakilishi aelewe hivyo kwamba hilo jambo serikali tumeshalishughulikia na litapata ufumbuzi si muda mrefu kutoka sasa. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa mara nyengine tena na nimshukuru Mhe. Waziri na nimshukuru kwa dhati na mimi nimemfahamu. Ninasubiri kwa hamu kauli yake ya kwamba si zaidi ya mwezi mmoja Mkuu wa Mkoa atatangaza Masheha wapya na yale mengine yatafuata taratibu za serikali.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nimepokea kwa furaha kubwa kazi hii kwangu itanipungukia na wananchi wangu watapata faraja kutunukiwa katika utumishi mzuri na serikali yao.

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kuna msemo unaosema, "mti wenye matunda haweshi kupigwa mawe au makwipi kwipi", lakini mimi sijakata tamaa, haya mawe ninayorembewa ndio mti unaozaa mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nisome *hansard* ya tarehe 19 Oktoba, 2012 alisema Mhe. Spika sisi uheshimiwa wetu tunaowitwa umetokana na wananchi kwa kukubali Katiba hii, ndio tumeitwa Waheshimiwa Wajumbe kwa ajili hiyo wananchi wameamua kutuchagua nendeni huko mukatuulizie masuala yetu. Kwa hivyo itapofika pahali hatutimizi wajibu wetu narudia maneno hayo…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub nisikilize, wewe una tatizo mimi nafikiri, haiwezekani. Ujenge hoja kile kitu ambacho kinatokana na hili ambalo tunalizungumza, mbona unasema vitu vyengine Mhe. Jaku?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa…

Mhe. Mwenyekiti: Jenga hoja kama una suala hujaridhika na ulivyojibiwa…

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mchuzi huwezi kupika bila ya viungo, ndio hoja inakuja, ungenisubiri kwanza dakika mbili. Lakini kama unataka hivyo hakuna tatizo.

Kwanza nimshukuru Mhe. Mussa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, Mhe. Mussa alikaribia kulia jana hapa…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku hilo suala ni wewe umeuliza? Suala langu wewe ulichangia katika kifungu hicho, kama hukuchangia kaa huna ruhusa ya…

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa nafikiri tukatoe *hansard* sasa hivi na niko tayari hata kupigwa mikwaju humu ndani. Tukatoe *hansard* sasa hivi kabla sijachangia...

Mhe. Mwenyekiti: Sasa nenda kwenye hoja yako hadithi za nini…

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sasa Mheshimiwa kiti chako kinayumba husimamii hoja, unayumbisha kiti mheshimiwa. Sasa uzungumze kitu ulichokuwa na uhakika nacho mheshimiwa, wewe kiongozi.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea, endelea…

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Eeeh! Hayo ndio maneno sasa.

Mhe. Mussa Ali Mussa alikaribia kulia jana hapa, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu alikaribia kulia.

Nilisema kuna watu wanavunjiwa nyumba, hali ya maisha ni ngumu.Tokea mtu anajenga serikali ilikuwepo wapi. Pana Sheha, Naibu Sheha, Halmashauri, maisha ni magumu tusione sisi Waheshimiwa tunapokea humu ndani nje hali ni mbaya nje.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni eneo lake lile, imevunjwa nyumba vibaya mno. Tuelimisheni hii ni dhamana, hali hairidhishi, hali ni tete, kwa utaratibu gani…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa unataka ujibiwe au unatoa *speech* wewe? Mhe. Waziri hakuchangia. Mhe. Waziri hakumbuki kwamba wewe umechangia hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi niko tayari hivi sasa niadhibiwe humu ndani ya Baraza kama sikuchangia kitu hicho. Sasa nani mkweli?

Hoja nataka kufahamishwa utaratibu nyumba zile zimevunjwa kwa misingi gani. Sasa unakuja unaniambia sijachangia, kama sijachangia nisingesimama hoja. Mimi ni Mwakilishi ninasimamia hoja yangu…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umeshauliza suala kaa kitako. Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani zile busara alizozikataa Mhe. Abdalla Maulid Diwani ndio mwahala kama humu zinahitajika, na Mheshimiwa umetumia busara.

Mimi ninayo orodha ya watu ambao wamelisema jambo hili na majibu yake hatuna tatizo kuyatoa kama serikali. Maana ndio kazi yetu. Mimi kwa faida ya Baraza na ili limekuwa likirejewa sana kunukuliwa Mhe. Rais kwamba ametuhimiza na anatuhimiza Mawaziri tuwe tunajibu majibu ya uhakika, na kazi hiyo tunaendelea kuifanya kwa sababu kama hatukumsikiliza yeye, hatuna mwengine wa kumsikiliza. (*Makofi*).

Sasa saa nyengine kinanukuliwa kifungu na kumnukuu Mhe. Rais kama kwamba Mawaziri hawatoi majibu. Sasa Waziri mimi na wenzangu Mwenyezi Mungu atuongoze tuweze kutoa majibu sahihi ili wananchi waelewe nini tunachokisema.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa suala hili limezungumzwa na Wawakilishi. Mhe. Abdalla Maulid Diwani, Mhe. Mussa Ali Mussa na wengine, Waheshimiwa wengi kidogo wamelichangia jambo hili. Na sisi *as a serikali*. Serikali kazi yake ni kuwahudumia wananchi wala si kuwabughudhi na kuwaingiza katika umaskini jambo hili. Lakini serikali inawahudumia wananchi kwa kufuata misingi ya Sheria na Katiba na Kanuni zilizopo na miongozo ya serikali inayotolewa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo hili la uvunjaji wa nyumba katika maeneo ya Kianga lilianzia wapi? Lilianzia baada ya kuonekana uvamizi wa vianzio vya maji unafanyika na serikali tukasema itafika pahala tutoe maamuzi magumu. Kwa hivyo taarifa nilizonazo zilivyokuja kwenye deski langu kama Waziri ni hizi zifuatazo. Naomba niziseme hizo na kama kutakuwa kuna taarifa za ziada, nipo tayari kuzisikiliza na hatimae kwenda kuzifanyia kazi ili tujue ukweli wa mambo ulivyo. (*Makofi*).

Taarifa nilizonazo kwamba timu ya Wilaya ya Magharibi ilikwenda kwenye *site* ikakuta kwa wakati huo nyumba nne tu ndizo ambazo zilikuwa zimejengwa katika eneo husika, zikatiwa alama X na kuambiwa kwamba eneo hilo haliruhusiwi kujengwa toka mwaka 2015. Na wahusika wote wakapewa maelekezo kwamba eneo lile haliruhusiwi kujengwa. Niko tayari kusikiliza maelezo yatakayotolewa ili serikali iweze kuyafanyia kazi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, timu ya Wilaya ilivyotoka, ikenda timu ya ulinzi na usalama, naweza nikahojiwa hapa *why* timu ya ulinzi na usalama, tumezungumzia suala la vianzio vya maji. Kwa hivyo nayo ilikwenda kujiridhisha kuangalia hiyo hali.

Mhe. Mwenyekiti, mara ya tatu ikenda timu nzima wakiwemo watu wa ardhi, watu wa mipango miji, wakaona hali inavyoendelea ya ujenzi. Sasa na maagizo na amri za serikali zikatolewa za kuvunjwa na kufanya mambo mengine. Hiyo ndio taarifa ambayo mimi ninayo katika deski langu kama Waziri. Na nasema Waheshimiwa Wawakilishi kama Wawakilishi wa wananchi wanayo haki ya kuwatetea wananchi, na sisi serikali vile vile kazi yetu ni kutoa huduma bora kwa wananchi na kutaka wawe na maisha mema. (*Makofi*).

Jambo hili liko katika hatua ya wahusika kwenda Mahakamani. Sina taarifa sahihi kama tayari wameshafungua hilo shauri au namna gani. Kwa hivyo serikali haipendezewi na jambo hili hata kidogo kama kweli wameonewa. Nataka nieleweke kama kweli wananchi wameonewa, serikali hatupendezewi hata kidogo na kuonewa kwa wananchi. Lakini kama na wananchi nao hawakufuata utaratibu, nadhani na sisi tuwe sehemu ya kuweza kutoa taaluma juu ya masuala haya.

Serikali haina nia mbaya na kama hili jambo litabainika vyenginevyo, hizo taarifa zilizopo sivyo zilivyo basi serikali haishindwi kuchukua hatua na kumrejeshea mwananchi haki yake na kuweza kulifanyia kazi. Kwa hivyo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe jambo hili Mwakilishi muhusika wa eneo binafsi alinipigia simu mimi wakati jambo hili linatokea. Ni mara yangu ya kwanza kusikia hilo jambo na nikalishuhudia tena, lakini nikatafuta taarifa nikazipata taarifa. Taarifa zinazohusu utaratibu mzima uliotumika mpaka kulifanya jambo hili.

Kwa hivyo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kwamba hapa tunaidhinisha matumizi na matumizi haya ni kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Hili jambo maoni waliyoyatoa Waheshimiwa Wawakilishi na Serikali nasi itabidi tufanye utafiti wa kina, ukweli uko wapi, baada ya haya ambayo tumeyapokea kwa wananchi au kwa Waheshimiwa Wawakilishi kutoka kwa wananchi lakini yamepitia kwa Waheshimiwa Wawakilishi, tujue ukweli wa mambo ulivyo, serikali inayo utaratibu kama kuna jambo, kama kuna mtu ameonewa basi huyo mtu haki yake itarudi tu kwa njia yoyote ile.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa tukitaka tulimalize hapa kwenye bajeti ambayo Mhe. Waziri Haji Omar Kheir ndio anaipitisha, ambaye siye aliyepeleka kijiko, nadhani Waheshimiwa wenzangu Wawakilishi mtakuwa kidogo. Kwa hivyo mimi nadhani cha msingi niwaombe Mhe. Mwenyekiti, kupitia kwako Waheshimiwa Wajumbe wale wote ambao wamelichangia jambo hili wangepaswa kugonga mguu kutaka ufafanuzi wa jambo hili.

Ufafanuzi wangu ndio huo kwamba hili jambo serikali tumelisikia na tunalifanyia uchunguzi kujua ukweli wa jambo hili uko wapi na hatimae serikali tutaweza kutoa taarifa rasmi juu ya tukio hili.

Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri, nafikiri maelezo yako yanatosha kabisa na kwa sababu serikali imesema inalifanyia uchunguzi suala hilo tuiachie serikali ifanyie uchunguzi na ripoti italetwa. Hapa mjadala nimeshaufunga tunaendelea.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi wakati nachangia nilizungumza kwa hisia kuhusiana na masuala ya vijana na Mhe. Waziri alitoa maelezo ya kina na nilimfahamu vizuri, lakini katika eneo moja sikupata ufafanuzi mzuri na moja kati ambayo niliyoyaona ni katika kifungu cha Katiba cha 32 (2), ambacho Mkuu wa Wilaya anaweza akipenda na bila kuathiri masharti yoyote katika Katiba hii au Sheria nyengine yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili ndio sisi tunapitisha hizi Sheria ambazo serikali Kuu inakwenda kuzisimamia. Sasa migongano inapotokezea baina ya kwenye Mikoa yetu, kwa mfano kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuna Baraza la Sanaa, kuna Bodi ya Sensa na Filamu, nafikiria pia kuna na Makamishna wa masuala ya utamaduni.

Sasa ninachotaka kutoka kwa Waziri anihakikishie tu basi kwamba katika maeneo yote na sheria ambazo Baraza hili tunazotunga hasa sisi Waheshimiwa ili kuisimamia na kuishauri serikali, Baraza hili haliwi *undermine* na maamuzi yanayochukuliwa katika Mikoa huku kwa kutumia kivuli au wakati mwengine cha Wenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Sasa cha msingi nataka tu Waziri anihakikishie kwamba Sheria ambazo tunazitunga kwenye Baraza hili zitasimamia ipasavyo na kwamba Serikali Kuu ndio serikali mama na kwenye masuala mazima ya ugatuzi ya Mikoa yote na Wilaya hakutakuwa na migongano katika maeneo yote.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Simai Mohammed Said na nilidhani majibu niliyoyatoa jana yalikuwa yanatosha, lakini kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa jumla naomba niseme kwamba pamoja na kifungu hicho cha Katiba alichokisema, lakini

Mkuu wa Mkoa ndiye anayesimamia shughuli nyengine zote za serikali ndani ya Mkoa wake.(Makofi).

Hili analolisema nadhani anazungumzia kuhusu nyumba za starehe na nyumba za kupiga mziki. Jana nilisema kwa nini serikali ilichukua maamuzi na jukumu hili akakabidhiwa Mkuu wa Mkoa ndani ya Mkoa wake. Kila Mkuu wa Mkoa alikabidhiwa ndani ya Mkoa wake jukumu hili. Kwa hivyo niseme kwamba mziki katika maeneo yasiyo stahili hautapigwa, isipokuwa kwa kibali maalum kwa mujibu wa sheria kama alivyosema Mhe. Simai Mohammed Said.(*Makofi*).

Lakini mziki katika maeneo mawili kama nilivyosema jana, hasa *disco* eneo la Hoteli ya Bwawani ambalo linakidhi vigezo na eneo la Hoteli ya Ngalawa. Hili tokea mwanzo limeruhusiwa lakini liliruhusiwa kwa muda na kwa sababu serikali ilikuwa inajiridhisha na hofu ambayo ilikuwa imetanda ya madawa ya kulevya, ya unyanyasaji kijinsia na mambo mengine. Kwa hivyo serikali ikasema kwamba tunatoa ruhusa mpaka saa sita mziki katika maeneo haya uendelee. Tukafanya kazi ya kufanya utafiti serikali, tulipoona mambo ambayo yalijitokeza mwanzo yamepungua, tukasema tunaongeza muda mpaka saa nane ya usiku. Mpaka sasa hivi muda huo ndivyo ulivyo na kutakuwa na utaratibu wa watoto walio chini ya umri hawataruhusiwa.

Mhe. Simai Mohammed Said wewe umetembea nchi nyingi, kuna nchi nyengine muingiaji ana kadi yake ile inayoonesha umri, baada ya muda wanakuja kufanya *inspection* wakiona kwamba umri wako haustahiki, wanampa adhabu mwenye ukumbi na yule mtoto anafungiwa kwa utaratibu ambao wamejiwekea. Sisi hatujafika huko lakini mimi nadhani niseme tu kwamba wahusika wote, kwa maana ya watu wa sanaa, watu wote wa habari wahusika kwenye hivyo vikao ambavyo amevifanya Mhe. Mkuu wa Mkoa walishirikishwa. Kwa hivyo na sisi jana nikasema serikali haijapata kuzuia *disco*, kwa sababu tunajua haya ni maeneo ya kukonga moyo vijana. Lakini tutatoa ruhusa kwa utaratibu ambao hautaathiri maadili ya Wazanzibari.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mimi nadhani Mhe. Simai akubali kwamba sisi tunasimamia sheria na Mkuu wa Mkoa anatakiwa asimamie hizo sheria, katika utekelezaji wa majukumu yao na kazi hizi zinafanywa kwa mashirikiano. Nimuombe Mhe. Simai ushauri wake aliousema kama kuna mapungufu yaliyopo katika utekelezaji wa jambo hili, basi tutafanya tathmini juu ya kazi ambayo imefanywa na halafu tutajua wapi tumekosea, tujirekebishe na wapi ambapo panahitaji pawekewe mkazo ili mambo yetu yaweze kwenda vizuri,

maadili ya Wazanzibari yawepo lakini vile vile na vijana wapate nafasi ya kuweza kukonga mioyo yao katika maeneo yale. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Waziri ametoa maelezo mazuri na pia maelezo ya jana, lakini moja ambacho alichokizungumza na nikanukuu kifungu cha Katiba ya Zanzibar, labda nimuulize kwa urahisi.

Katika Mikoa hii na sisi tunakwenda katika suala zima la mfumo wa ugatuzi ni kwamba kuna Serikali Kuu na kuna Serikali zetu hizi ambazo ni za Mikoa na Halmashauri, ambazo viongozi wake wametajwa na wanateuliwa na Mhe. Rais. Suala ni kwamba anihakikishie kuwa sheria zinazotungwa hapa mbali ya hizo za mambo ya muziki lakini na nyengine tofauti, ni kwamba sheria zinazotungwa na Baraza la Wawakilishi ambazo zinasimamiwa na Serikali Kuu hazitakuwa *undermine* au kufanywa kwamba ziko chini au Serikali Kuu inakuwa iko chini ya Serikali za Mikoa kwa kutumia kivuli cha uenyekiti wa Mkuu wa Ulinzi na Usalama wa Mkoa. Sasa mimi hoja yangu ni kwamba anihakikishie tu basi kwamba Serikali Kuu ipo itasimamia na sheria zote ambazo zimetungwa na Baraza la Wawakilishi tutakwenda baada ya hayo tunasonga mbele. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri alilizungumza labda alizungumze *in a way* unavyotaka wewe, lakini amelizungumza vizuri sana Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kama ulivyosema nimelizungumza vizuri. Kwanza serikali yenyewe ndio inayoleta hizo sheria hapa Barazani.

Kwa hivyo serikali inahakikisha kuzisimamia hizo sheria na pale sheria inapokuwa ina ukakasi ndio maana tunaleta marekebisho au tunaiandika upya. Kwa hivyo Serikali Kuu ipo hasa hii ya Mapinduzi ya Zanzibar toka mwaka 1964 na itaendelea kuwepo na tutahakikisha kwamba Wakuu wa Mikoa hawafanyi kazi kinyume na sheria zilizopo. Ahsante sana.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante tuendelee na tumeweka vizuri sawa *hansard.*

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea, tumeshamaliza Mheshimiwa umechelewa kuja, endelea.

Jumla ya Programu Ndogo	321,434,000
Jumla ya Programu Kuu	**321,434,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PD 0702 Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mkoa wa Mjini/ Magharibi

Kifungu SD 070201 Programu Ndogo ya Utawala na Uongozi wa Mkoa

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi,

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri na jana nilichangia sana katika sehemu hii hasa katika mambo ya sanaa. Kwa sababu tukiangalia Mhe. Waziri alivyojibu namshukuru, nampongea, lakini lengo kubwa nililochangia na dhamira yangu nchi yetu tumekubali utalii na pato kubwa tunapata kutoka kwa utalii na watalii wanapokuja wanataka kustarehe katika nchi. Kwa hivy, tuangalie usalama wa mkoa wetu lakini sio kuzuwia kabisa suala hili likawa hamna starehe kwa ajili ya hawa wageni wetu, na kama itakuwa Wazanzibari mila zinaharibika basi tuzuwie Wazanzibari wasiingie waingie watalii wanaotoka nje ya nchi tu, kwa sababu wao wanataka kustarehe hawaelewi kitu chengine.

Halafu jengine leo nataka nitoe taarifa, kuna kongamano la Mashekhe wanaandaa saa nane. Kongamano hili lengo kufunga hizi sehemu zote za starehe. Sasa mimi nasema jamani tusichanganye mambo ya Dini na haya ni mambo ya ajabu sana, kwa sababu mimi najua mambo haya mara nyingi ukiingia kwenye mambo haya ukiwa hutaki, ni muamsho unakuwa wewe.

Sasa haya mambo ni ya kitalii na mambo haya tunapata kodi kwenye nchi yetu yanachangia. Sasa mimi naomba sana Mhe. Waziri umenijibu vizuri na hili kongamano leo linalofanywa tuwasikilize. Lakini hapo hapo pia tuangalie uchumi wa nchi yetu na dhana nzima ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante nakushukuru sana.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, nilipochangia kwa maandishi nilimuomba Mhe. Waziri aliangalie suala zima la lile shimo la maji pale Mitondooni ambapo pana ujenzi unaofanywa

pale. Huyo anayejenga anasema anafanya nyumba ya ibada, lakini hivi sasa mpaka leo nimepita ana-*concentrate* kwenye ujenzi wa maduka, milango ya maduka na maji yote ya mtaa ule pale ndio yanakwenda pale.

Sasa yeye ujenzi wake ule anataka kuya- *divulge* maji yaende yakakere wananchi, imekuwa kilio kikubwa sana pale. Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri kupitia Mhe. Mkuu wa Mkoa kuna kamati ile inayosimamia ujenzi, ramani ya mkoa, wende wakaangalie pale kama kweli kuna *benefit* kubwa kwa wananchi, sawa ujenzi uendelee. Lakini kama ni kero na kuwaudhi wananchi basi usimamishwe, yule bwana apatiwe mahali pengine aendelee na ujenzi wa kitu anachokitaka.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwa hilo ombi tu ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, Mwakilishi wa wananchi jimbo la Dimani kwa ushauri ambao ametupa na kweli kutokana na muda sikuweza kutoa ufafanuzi juu ya jambo hili.

Kwanza nakubaliana na ushauri wake kwamba Kamati ya *DCU* ambayo inashughulika na masuala ya ujenzi itakwenda pale na kuna mambo mengi sana ya kufanywa kutokana na athari za kimazingira, tuangalie kama ripoti ya kufanya utafiti wa mazingira inakubaliana na *concept* yake au haikubaliani. Kama haikubaliani basi serikali itatoa maamuzi ya kusitisha ujenzi ule.

Na kabla ya hapo tulishasitisha kwa muda lakini kama anaendelea, maana yake anakaidi maagizo ya serikali. Kwa hivyo nakushukuru Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame kwa kutu-*alert* hilo na kamati nzima ya *DCU* ambayo inatoa vibali vya ujenzi ndani ya Mkoa wa Mjini/Magharibi itafika *site* na itaangalia hiyo na tutachukua hatua mara moja kama anakwenda kinyume na utaratibu. (*Makofi*).

Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana mimi katika kuchangia kwangu njana nilisema tu kwamba sina nia ya kuzuwia bajeti hii wala sina tatizo, isipokuwa nataka kupata ushauri juu ya ufanisi wa maendeleo ya Manispaa zetu tatu.

Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu naipongeza kwa dhati kabisa kuona mandhari au ramani ya Mkoa wetu wa Mjini/Magharibi kwamba mkoa umestahiki kuwa

na Manispaa tatu. Katika kuhama katika Manispaa hizo kuna mali za Manispaa zetu. Manispaa ya Mjini ina mali nyingi na mali hizo wamemiliki wao peke yao. Kwa kuwa wenzetu hawa wamepata kazi kubwa ya kuwa Manispaa na hawana kitu katika mikono yao. Je, Mhe. Waziri ana ushauri gani wa kuhakikisha kwamba magari ya kuzolea taka pamoja na makontena sehemu mbali mbali angalau wakapatiwa Magharibi 'A' na 'B', kama ni chanzo cha kuendeleza maisha yao huko mbele watajitegemea zaidi.

Nataka ushauri tu mimi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nalo suala lake Mhe. Ali Suleiman Shihata lilikumbwa na ule ule utaratibu wa muda, lakini majibu yake yapo.

Najua *concern* ya Mhe. Mwakilishi hasa kwa Manispaa zake za Magharibi 'A' na 'B'. Ni kweli Manispaa hizi miundombinu yake haijawa vizuri, lakini hata vifaa vya usafiri haijawa mizuri. Lakini kwa Manispaa ya Mjini magari ambayo yaliyopo yalilengwa kwa ajili ya Manispaa za Wilaya ya Mjini na pale inapotokezea haja ya kusaidiana, kwa sabab taasisi hizi zote zinasimamiwa na chombo kimoja huwa tunafanya hivyo kwa mambo yale ya *emergency*. Hata hivyo Ofisi yangu imeshaandaa andiko maalum la mradi na kuwasilisha Tume ya Mipango kwa ajili ya kupeleka kwa wafadhili ili na Manispaa hizi nazo ziweze kupata vitendea kazi kwa ajili ya ufanisi wa Manispaa zetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile *master plan* mpya, *master plan* ya mji ndani ya Mkoa wa Mjini/Magharibi, kama nilivyotoa taarifa jana hivi karibuni tu *master plan* hii, mpango huu utazinduliwa rasmi pale *Mapinduzi Square* kwa ajili ya kuoanisha katika Manispaa hizi za Magharibi 'A na Magharibi 'B', ni eneo gani panahitaji miundombinu gani na maeneo gani panahitaji huduma za jamii gani.

Suala la mali ni kweli mali nyingi sasa hivi zinaonekana kwenye Manispaa ya Mjini. Suala hili kwa mujibu wa sheria yetu wenyewe tuliyoipitisha, inatambua kumpa uwezo Waziri muhusika kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha kuona kama kuna vitu tunaweza tukavihaulisha tukavipeleka sehemu nyengine. Kwa sababu hizi mali zote ni za serikali. Kwa hivyo ikitokea haja hiyo nadhani kwa mujibu wa sheria iliyopo Waziri mwenye sekta inayohusika na Waziri wa Fedha tutakubaliana ili tuone tunasaidianaje kuhusu kuona Manispaa gani inahitaji raslimali gani ili iweze kufanya kazi zake vizuri. Kwa hivyo naomba tuvute subra na kwa sababu hili jambo ndio tumelianza sasa, najua sisi wizarani pale tumeshaanza kazi ya awali na tutalifanyia kazi baada ya kuwasiliana na

Waziri anayehusika na masuala ya fedha ambaye ndiye mmiliki wa mali zote za taasisi za serikali.

Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana majibu mazuri ya Mhe. Waziri sina matatizo nayo naomba tuendelee, lakini pamoja na hilo naongezea tu kidogo. Pamoja na huo mgao utakaoangaliwa masoko yaliyokuweko Magharibi 'B' pia yaangaliwe ili kupata manufaa kwa Magharibi yetu 'B' tuliyokuwanayo. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Jumla ya programu ndogo	1,961,366,000
Jumla ya Programu Kuu	**1,961,366,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PD 0703 Serikali za Mitaa	Programu Kuu ya Usimamizi na Uendeshaji wa
Kifungu SD 070301 Mitaa Baraza	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Serikali za
	la Manispaa Mjini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti ahsante, kwanza naomba kukuletea *hansard* hii yale niliyoyazungumza upate kuhakikisha ujiridhishe, anayehusika aje achukue *hansard* ampelekee Mhe. Mwenyekiti, kwanza ili kuhakikisha nilichokizungumza.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, unajua kiongozi mzuri ni yule anayesimamia hoja yake kwa kikamilifu, nilikuwa nataka kujua dhamana wa kufunga magari maeneo ya Mji Mkongwe ni Polisi Jamii au Manispaa. Kumekuwa na usumbufu wa kutosha na sheria gani kama kuna Polisi Jamii walioruhusiwa ku-*charge* shilingi 10,000 gari ile na pesa zinakwenda wapi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, dhamana wa nidhamu ndani ya mji wowote ule hasa unaohusu vyombo vya usafiri ku-*park* inakuwa ni ya Manispaa. Kwa hivyo dhamana ni Manispaa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri umejiridhisha na *hansard* yangu na maneno yangu, mimi huwa sisemi uongo sana hapa aghalabu itokee tu kuteleza. (Makofi).

Ikiwa dhamana ni Manispaa sasa sheria gani iliyowapa wale kufunga gari kule na kuwasumbua watu na baadhi ya wengine kufungiwa na wengine kutofungiwa, na baadhi ya Waheshimiwa yameshawakuta hayo, isipokuwa gari za SMZ tu na za Waziri hazina usumbufu huo. Tumelalamika sana suala hilo Mhe. Waziri, tupeni kama *plate number* au vyengine sio mimi, mimi nina vespa tu Mhe. Waziri. watu wanateseka na usumbufu huo wakifukuzia kwenye boti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku Hashim hodari sana wa kueleza utaratibu na hili suala juzi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais walilijibu.

Sasa kwa mujibu wa utaratibu kitu chochote ndani ya miezi mitatu hakitakiwi kisemwe tena. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais juzi suala hili wamelijibu vizuri sana na Mhe. Jaku sina hakika kama alikuwepo. Sasa kwa hoja hii mimi nadhani majibu yaliyotolewa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais juzi kama anaweza kuyaongezea Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anaweza kuyasema, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa haina haja kwa sababu limeshajibiwa halitaki kujadiliwa tena sasa hivi. Ningekuomba sana Mheshimiwa nenda kwenye *hansard* ukaangalie majibu ya serikali, halafu baadae kama utataka ufafanuzi wa ziada tunajua nini cha kufanya. (Makofi).

Lakini Mheshimiwa inatosha kwa leo tunaendelea.

Jumla ya Programu Ndogo		2,935,517,000
Kifungu SD 070302	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa Baraza la Manispaa Magharibi 'A'	822,883,000
Kifungu SD 070303	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa Baraza la Manispaa Magharibi 'B'	

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri au Manispaa Magharib 'A' na 'B' zilikuwa Wilaya moja tu au ilikuwa Halmashauri moja. Tumegawana raslimali watu magari, fedha, lakini kwa bahati mbaya sana

mpaka leo bado wataalamu ndani ya Maofisi ni kidogo sana. Sasa jana katika maelezo nilimuuliza Mhe. Waziri ni lini atatupatia wataalamu kwenye Manispaa 'A' na 'B'.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Masoud Abrahmana na Mhe. Rashid Makame Shamsi aliuliza suala hili, na Mhe. Naibu Waziri alijaribu sana kulitolea ufafanuzi.

Lakini maelezo ya jumla niliyoyatoa kwamba hivi sasa na leo hii tunavyozungumza kuna vikundi kazi vitano vya sekta mbali mbali vinafanya kazi ndani ya mwezi mmoja na nusu au miwili viwe vimekamilisha hiyo kazi. Nikasema kuna kikundi kazi cha raslimali watu ambacho kinaongozwa na Naibu Katibu Mkuu masuala ya utumishi wa umma, kikundi kazi cha miundo ya utumishi ambacho kinaongozwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuna kikundi kazi cha sera na sheria ambacho kinaongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu, kuna kikundi kazi cha *awareness,* kueneza uelewa kwa wananchi kwa umma kinaongozwa na Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na kuna kikundi kazi cha fedha kinaongozwa na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha.

Katika hadidu rejea ambazo wamepewa ni pamoja na kuona mahitaji ya *local government* zetu zote. Kwa hivyo baada ya kazi hiyo kukamilika serikali itafanya kazi ama ya kuhamisha watumishi waliopo katika serikali kwenye sekta nyengine kuwapeleka kwenye *local government,* kama hakuna serikalini kuajiri ili Halmashauri hizi ziweze kufanya kazi zake vizuri.

Kwa hivyo vikundi hivi vitakapomaliza kazi yake ndani ya miezi miwili, hili tatizo ambalo amelizungumza na nimshukuru sana Mhe. Rashid Makame Shamsi amelizungumza suala hili basi suala hili litaweza kupatiwa ufumbuzi wake. Kwenye *local government* zote katika kuelekea kwenye ugatuzi wa madaraka. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, naendelea tena kumshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake wa kina kabisa na tunaridhika.

Mhe. Mwenyekiti, nilishauri hasa katika Manispaa Magharibi "B" kuhusu suala zima la barabara ya Fuoni, nilieleza kwamba barabara Fuoni ni barabara mpya ya kisasa serikali imetumia fedha nyingi sana. Lakini kila siku zikienda ile haiba yake inaanza kuondoka kidogo kidogo na hasa kwa kuangalia ile michanga ambayo hakuna watu ambao wamepangwa kwa ajili ya kusafisha

kama zinazosafishwa barabara nyengine za hapa mjini. Sasa tulikuwa tunataka *atleat* Mhe. Waziri anambie basi labda kuna utaratibu gani wa kuandaa vile vikundi vya kusafisha barabara ili nayo ikaendelea kuwa na haiba yake kwa muda mrefu pamoja na bustani pale katikati. Ahsante

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, natambua mchango wake kama nilivyosema nalo suala hili lilikubwa na ule muda wa kutokuoa ufafanuzi.

Barabara ya Fuoni ina mambo miwili, ina suala pale pahala panapo tuwama maji, ambapo kama mlifuatilia juzi Mhe. Rais alipokuwa anatembelea maeneo yaliyoathirika kuna maelekezo rasmi ambayo Mhe. Rais ameyatoa juu ya ufumbuzi wa eneo lile pale, nalo pia linatoa pia haiba ya uzuri wa ile barabara.

Kwa hivyo wizara zinazohusika, Wizara ya Ardhi, Wizara yangu na Wizara ya Ujenzi tumepewa jukumu kwa ajili ya kuona kwamba lile tatizo linapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Lakini katika suala hili la mchanga na kuondosha haiba, nikuombe Mhe. tulichukuwe hili na twende tukalifanyie kazi ili haiba ya barabara ile ibakie. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri asione tabu ndo tunajenga.

Mimi nipo kwenye usimamizi wa Serikali za Mitaa, Baraza la Manispaa Magharibi "B". Wasimamizi wa Baraza la Manispaa ni Madiwani. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko kabisa hii *ceiling* waliopewa Magharibi "B", Madiwani hawajakaa hata siku moja kuijadili bajeti yao, kutoa mipango yao mpaka leo Mhe. Waziri anaomba pesa tumpitishie hapa.

Nini matokeo yake. Mhe. Mwenyekiti, matokeo yake huko sasa watakwenda kugombana, haya malengo yaliyowekwa kila mmoja ataomba mimi nipewe huku, nimewe huku, maana yake hawajakaa hawajapanga nje ya utaratibu.

Sasa Mhe. Waziri kama kawaida yangu mimi simuondolei fungu, lakini namuomba tena kwa kweli hili si, Wazungu wanasema *is not health situation*, hii sio hali nzuri, watakwenda kugombana watatuparaganya na huku Mhe. Mwenyekiti, tuna majimbo saba mazito Wilaya ya Magharibi "B". Unajua uzito wa Wilaya ya Magharibi.

Sasa ikiwa *ceiling* tunawapa, wasimamizi wetu ndio Madiwani hawajakaa na Mkurugenzi wao wakapanga wakagawana, tutakwenda vipi. Kwa hivyo namuachia mwenyewe Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nataka niendelee kumshukuru sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na nimtoe hofu, sioni tabu nilijifunza vizuri sana Mheshimiwa alipokuwa Waziri wa Wizara hii namna alivyokuwa akinyanyuka mara kwa mara. Kwa hivyo sioni tabu Mheshimiwa usiwe na wasi wasi kwa sababu ni wajibu wangu nitowe ufafanuzi wa namna ya serikali inavoweza kufanya kazi. Kwa hilo najua unanikumbusha lakini unajua.

Lakini la pili ni kwamba hizi fedha ambazo tunazipitisha hapa ni ruzuku kutoka serikalini. Fedha hizi kama ulimsikia jana Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ni fedha ambazo zimetoka katika sekta zile ambazo ambazo zinagatuliwa na matumizi yake tayari yapo, na kwa hili nitahakikisha ninasimimamia vikao vya Madiwani vinafanyika ili kupata uwelewa wa matumizi ya fedha hizi.

Kwa sababu wao ndo wanatakiwa wasimamie haya matumizi na zile pesa ambazo zitakushanywa na wao. Kwa hivyo bado hatujachelewa. Hii ni ruzuku tu ni sawa sawa na kukwambia mtu kwamba wewe pamoja na uwezo ulionao, lakini nakugaia koti hili, najua unazo nyingi lakini mimi nimeamua kukutunuku hili.

Kwa hivyo hizi itakuwa ni ziada ya zile fedha ambazo Waheshimiwa Madiwani watakwenda kuzipanga na hizi watazisimamia. Na pale utaratibu kama nilivyosema ule wa ugatuzi ule, utakapokuwa ushaanza kutoka chini kuja juu pengine mwakani bajeti ijayo haitakuwa hivi. Hapa zitakuja fedha zitakozotolewa na serikali ambazo wananchi wenyewe watakuwa wameibua miradi kutoka kwenye ngazi ya Shehia, kwenye Mabaraza ya Wadi na hatimae Halmashauri na hatimae kwenye Kamati ya Maendeleo ya Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa mwaka huu kwa sababu tumetaka serikali ianze kugatua kwa baadhi ya sekta, ndio maana Serikali imezitoa hizi pesa kama ruzuku. Kwa hivyo tutajitahidi tuwasimamie wasigombane ili haya mambo yaliyopangwa na serikali yaweze kufanya kazi vizuri.

Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendea, tumemaliza tumemaliza hapa.

Jumla ndogo	879,800,000
Jumla ya Programu ya usimamizi na uendeleshaji wa serikali za Mitaa	400,638,200
Jumla Kuu	**6,921,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU - D08 MKOA WA KUSINI UNGUJA

Kifungu D0801 Mipango na Sera	13,008,000
Jumla Kuu	**13,008,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D08 - MKOA WA KUSINI UNGUJA

Kifungu PD0801 Uratibu wa Maendeleo ya Mkoa Kusini Unguja

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa nilikuwa na malengo ya kuchangia hapa, pa kuhoji hapa katika fungu hili. lakini moja nataka nifahamu.

Mhe. Waziri alitoa maelezo mazuri lakini tatizo kwangu mimi liko eneo moja. Mhe. Mwenyekiti, katika suala la barabara hasa *feeder roads* zinazosimamiwa na Mkoa na Halmashauri zetu za Mkoa Kusini, Wilaya Kati. Jimbo langu ambalo mimi nawakilisha hapa tuna Shehia kumi na tatu na katika eneo la Tunguu pana Afisi ya Mkoa, Afisi ya Chama cha Mapinduzi zipo huko huko katika Wilaya Kati lakini pia kuna Vyuo Vikuu pale pamoja na Makao Makuu pia ya Polisi Mkoa wa Kusini.

Tatizo linakuja hapa barabara ambayo inayotoka kutoka Istiqama kwenye *Zanzibar University*, lakini pia na ile ya Tunguu kwa ujumla niliozungumza jana ya kutoka kwa mzee wa kazi kwenda mpaka Titiani, ambayo ina kilo mita 4.2. Sasa kwa kweli serikali wawekata viwanja, watu wanaoishi ni wengi, sasa ile njia imekuwa ni muhimu sana kwa wananchi, na natambua kuna umuhimu sehemu nyengine.

Lakini pia na eneo la kwa Kozi mpaka kuja Jumbi, barabara ile kwenye kona imeharibika yote hasa baadhi hizi mvua, yaani kama wananchi wangu wananisikia hapa na wananchi ambapo pia wa maeneo ya jirari wanatumia barabara ile kwa Mkoa wa Kusini.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri kwa huruma kabisa anifanyie nafasi ya upendeleo anisaidie, yaani kwa sababu sote ni Tunguu na Tumbatu ni wamoja. Mimi pia sura yangu kama Mtumbatu. Sasa naomba sana aniangalie kwamba hizi barabara ataweza kutusaidia katika Mkoa wetu wa Kusini ili wananchi hawa wote pamoja na viongozi wanaokaa maeneo haya na majimbo ya jirani wataweza kufaidika. Naweza kutumia hii miundo mbinu iliyokuweko. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai Mohammed Said Mhe. Waziri alilielezea vizuri sana suala zima la *feeder roads* na akasema watafanya kazi pamoja na Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano na wanatakaa vikao ili kuhakikisha vipaumbele vya hizo *feeder roads* wapi watakwenda. Sasa sijui kama ana jengine zaidi hilo, naona kama una- *lobby*, unaomba kwamba ufikiriwe zaidi.

Nafikiri Mhe. Waziri amekusikia.

Mhe. Simai Mahammed Saidi: Mhe. Mwenyekiti, hapa nalia ndani moyoni mwangu lakini chozi halitoki, lakini Mhe. Waziri kalielewa. Mimi nataka aniambie tu nakuonea huruma nitafuatilia, anambie tu, hasa katika maeneo haya niliyoyataja mengine tuko tayari kustahamili. Lakini haya ya Tunguu hizi kilo mita 4.2 pamoja Kwa Kozi. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, hali ni mbaya wananchi wanapata tabu sana.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa nimekusikia Mheshimiwa mimi ninachoona ni kwamba tunarudia sana, hatutomaliza mpaka saa 12 na jioni tunatakiwa turudi.

Sasa tukiwa tunarudia kila mtu anakuja na *issue* yake moja, Mhe. Waziri anajibu halafu anakuja na mwengine hatumalizi leo. Kwa hivyo kalisemea kwa ujumla, naomba ulipokee hivyo. Sasa kama unajaribu *lobby*, kwa maana kwamba unamtaka Waziri afanye hiyo kazi, kwa wakati wako muone Waziri.

Naomba tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Saidi: Nomba Mhe. Waziri aniangalie tu. Ahsante Mhe.

Jumla ya programu hii 200,012,700,052/-

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji Khamis Mussa, kifungu kimepita, kimeshapita. Kifungu kimekubaliwa umechelewa Mheshimiwa. Tunaendelea. *(Makofi)*

Jumla ya Programu Kuu Uratibu ya Shughuli za Maendeleo ya Kusini Unguja ni **200,012,700,052**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu DP 0802 Uendeshaji Na Uratibu Wa Mkoa Wa Kusini Unguja

Kifungu SD080201 Uendeshaji na Utawala wa Mkoa wa Kusini Unguja

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina nia ya kuzuia fungu isipokuwa katika kuchangia na hasa hizi shughuli za uratibu na kunako haya mambo ya maendeleo, nilimuomba Mhe. Waziri aliangalie jengo ambalo lina karibu miaka minane halijapata ile *support* hasa katika hizi programmu kuu za Serikali kunako jengo la Mkuu wa Wilaya ya Kati.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nilikuwa nataka tu Mhe. Waziri aniwekee sawa, akeshaniweka sawa katika jambo hili kwa serikali itatia nguvu gani ili Mkuu wetu wa Wilaya yule awepo katika maeneo mazuri na yanayoridhisha ili afanye kazi vizuri basi. Baada ya hayo tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimshukuru Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa hoja yake ni kweli kuliangalia, nitaendelea kuliangalia ni kweli kutokana na ukubwa wa jengo lilivyo, linahitaji mradi maalumu ili tuweze kulifanyia kazi na liweze kumaliza na tumjengee mazingira mazuri Mhe. Mkuu wa Wilaya.

Sasa nimuombe tu Mhe. Miraji kwamba hili atuachie kwa sababu ndani ya bajeti hii hakuna kifungu cha mradi ambacho kitafanya kazi hii na tunategemea *O.C.* Lakini kwa *O.C* peke yake hatuwezi kumaliza.

Kwa hivo nimuombe Mhe. Miraji mimi nitaendelea kuliangalia na kutafua njia nyengine mbadala za kutafuta wahisani ili waweze kuchangia jengo hili. Lakini

kwa mwakani kwenye bajeti ya mwakani, tutaamua kwenye Mkoa wa Kusini kuona tunalipa kipa umbele jengo hili ili liweze kukamilika na liweze kutumika kwa ile dhana ambayo imekusudiwa kufanyika.

Kwa hivyo katika hili namshukuru Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa kunikumbusha na mimi nimpe ahadi kwamba nitakaa na uongozi wa Mkoa wa Kusini mwakani kwenye bajeti ya mwakani ili tuone tunalipa kipa umbele jengo hili. Ahsante sana.

Kifungu SD080201	Uendeshaji na Utawala wa Mkoa wa Kusini Unguja	1,531,748,000
Kifungu PD0803	Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa	
Kifungu SD080301	Usimamizi wa Serikali za Mitaa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini.	462,100,073
Kifungu SD080302	Usimamizi wa Serikali za Mitaa Halmashauri ya Wilaya ya Kati	611,227,000
	Jumla ndogo	1,073,400,000
	Jumla Kuu	**2,817,900,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D09 - MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Kifungu D0901	Mipango na Sera	13,008,000
	Jumla Kuu	**13,008,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGUD09 - KUIMARISHA SHUGHULI ZA SERIKALI KATIKA MKOA

Kifungu SD090101	Kumairisha shughuli za Maendeleo ndani ya Mkoa	222,029,000
Kifungu PD0902	Uratibu na Uendeshaji wa Shughuli za Mikoa za Wilaya na Shehia	1,482,371,000
Jumla Kuu		**1,482,371,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu PD0903	Programu Kuu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa	
Kifungu SD090301	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa Halmasharu ya Wilaya ya Kaskazini A	758,827,000
Kifungu SD090302	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B	599,273,000
Jumla		**1,358,100,000**
Jumla Kuu		**3,062,500,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D10 - MKOA WA KUSINI PEMBA

Kifungu D1001	Mipango na Sera	11,708,000
Jumla Kuu		**11,708,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D10 - MKOA WA KUSINI PEMBA

Kifungu PD1001	Programu Kuu ya Kusimamia Shughuli za Serikali Katika Mkoa	
Kifungu SD100101	Programu Ndogo ya Kusimamia Shughuli za Serikali katika Mkoa	175,985,000
Jumla		**175,985,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu PD1003	Programu Kuu ya Uendeshaji na Utawala wa Mkoa Wilaya na Shehia	
Kifungu SD100301	Programu Kuu ya Uendeshaji na Utawala wa Mkoa Wilaya na Shehia	2,141,835,000
Jumla		**2,141,835,000**

Kifungu PD1004	Programu Kuu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa	

Kifungu SD100401	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa Baraza la Mji Mkoani	478,142,000
Kifungu SD100402	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa Baraza la Mji Chake Chake	

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nilinde. Hata kama mmechoka subirini kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri kuhusu ujenzi huu wa jengo la Qatar jipya na wale watu ambao ni Qatar kongwe, wale watu ambao wako nje. Naomba ufafanuzi Mhe. Waziri hivi hilo jengo letu jipya litakuwa katika muundo gani. Maana yake tunaweza tukalifanya kama *mall*, halafu wale watu wetu wa nje ikawa tuwatengenezee mazingira ya kawaida ambayo wataweza kuuza biashara ndogo ndogo au wale wale wanarudi ndani. Kwa sababu lile jengo ni jengo la kisasa. Nataka kufahamu hapa kidogo Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, *spirit* ya serikali ni kuhakikisha kwamba wafanyabiashara waliokuwepo kwanza warudi pale. Lakini jana nilitoa maelezo kwamba muundo gani wa soko hili, nilisema hili soko linasimamiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Kwa hivyo tutakaa na Wizara ili tuweze kuona ni taratibu gani za ule ujenzi wa soko ulivyo. Tutakapopata taarifa, maana yake nachelea kutoa taarifa ambazo sio sahihi.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Mjumbe, kwanza wafanyabiashara waliopo watazingatiwa kwanza huo ndio utaratibu wetu, kwamba unapomtoa mtu na unatengeneza kitu kizuri basi ni vizuri umrejeshe pia na yule ambaye umemuondosha. Kwa hivyo nikuombe Mhe. Suleiman Sarahan au kwa maarufu wa Sele Manga, nikuombe uvute subra ili hili jambo tulifanyie kazi pamoja na Wizara husika ili tuweze kutoa majibu sahihi.

Kwa msingi huo jibu lake tutalileta kwa kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Mazingira ili kueleza ni muundo gani wa lile soko uko. Hivi sasa nitashindwa kumpa maelezo. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu SD100402	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa Baraza la Mji Chake Chake	438,439,000
	Jumla	**916,581,000**
	Jumla Kuu	**3,234,400,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D11 - MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Kifungu D1101	Mipango na Sera	11,708,000
	Jumla Kuu	**11,708,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D11 - MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Kifungu PD1101	Programu Kuu ya Kusimamia Shughuli za Serikali Katika Mkoa	
Kifungu SD110101	Programu Ndogo ya Shughuli za Serikali katika Mkoa	209,562,000
	Jumla	**209,562,000**
Kifungu PD1103	Programu Kuu ya Uendeshaji na Utawala wa Mkoa, Wilaya na Shehia	
Kifungu SD110301	Programu Ndogo ya Uendeshaji na Utawala wa Mkoa, Wilaya na Shehia	1,465,938,000
	Jumla	**1,465,938,000**
Kifungu PD1104	Programu Kuu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa	
Kifungu SD110401	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa Baraza la Mji Wete	934,412,000
Kifungu SD110402	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa Halmashauri ya Wilaya Micheweni	679,188,000
	Jumla	**1,613,600,000**
	Jumla Kuu	**3,289,100,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D12 - OFISI YA USAJILI WA VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHO

Kifungu D1202	Utawala	61,000,000
Kifungu D1203	Ofisi ya Mrajis, Vizazi na Vifo	173,152 ,000
Jumla Kuu		**234,152,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D12 - OFISI YA USAJILI WA VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHO

Kifungu PD1201	Programu Kuu ya Kusajili Vizazi, Vifo na Kadi za Utambulisho	
Kifungu SD120101	Programu Ndogo ya Usajili wa Vizazi, Vifo na Kadi za Utambulisho	1,272,800,000
Jumla		**1,272,800,000**
Kifungu PD1202	Programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Usajili wa Vizazi, Vifo na Kadi za Utambulisho	
Kifungu SD120201	Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Usajili wa Vizazi, Vifo na Kadi za Utambulisho	1,716,799,000
Kifungu SD120202	Programu Ndogo ya Ofisi Kuu Pemba	171,201,000
Jumla		**1,888,000,000**
Jumla Kuu		**3,160,800,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tukae. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, kwa hoja zao nzuri ambazo zimepata majibu zote. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio hayo.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na Mhe. Waziri. Wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono. Wanaokataa. Wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukuwe fursa hii adhimu kwanza kabisa kumpongeza Mhe. Waziri kwa kujibu hoja zake vizuri sana. Vile vile kwa uchambuzi mzuri ambao ameufanya hasa katika masuala ambayo bado yanaendelea kufanyiwa kazi na serikali. Kwa hivyo naamini mimi Waheshimiwa Wajumbe walikuwa makini katika kusikiliza na hii itasaidia sana katika kufanya shughuli zetu za kufuatilia utendaji wa serikali. Nikupongeze sana Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Vile vile niwapongeze na Waheshimiwa Wajumbe wote ambao kwa kweli wameonesha hamu yao kubwa ya kuona namna gani Wizara hii inafanya kazi na itafanyakazi hasa kwa kutumia bajeti hii. Niwapongeze sana. *(Makofi)*

Lakini niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe tufuate Kanuni na utaratibu tulionao ndani ya Baraza la Wawakilishi, kwamba mtu anataka kuuliza pale ambapo alitia nia au aliweka nia ya kusema kwamba hapa mimi nitazuwia kifungu, na sio kila pahala ambapo mtu anaweza au anastahiki kuuliza suala. *(Makofi)*

Lakini jengine pale ambapo Mhe. Waziri ameshatoa majibu na kufanya ushindani, mimi nafikiri sio jambo zuri sana kama sisi Waheshimiwa. Kwa

hivyo ningewaomba sana kwa utaratibu tuliojiwekea wenyewe Waheshimiwa, na huu ni utaratibu wa hivi karibuni tu, tuendelee nao ili tuweze kuleta mafanikio ndani ya Baraza hili.

Niwashukuru sana na niwapongeze lakini kwa muda ambao tumeongeza lakini bado mmekuwa wastahamilivu, lakini tutaendelea jioni wakati ule ule saa 11:00 tufike hapa leo jioni.

Kwa maana hiyo naahirisha hadi jioni au nasitisha kikao hadi jioni saa 11:00. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

(Saa 8:20 mchana kikao kiliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi Kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Utaratibu

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana nimesimama kwa kanuni ya 72(1) lakini nakazia 72(2) kuhusu kiwango cha vikao vya Baraza la Wawakilishi nusu ya wajumbe, lakini vile vile kanuni ya 72(2) mara baada ya uamuzi wowote kutolewa ikiwa ni mjumbe yoyote aliyehudhuria atapiga kwa kudai kwamba mbali ya Spika, wajumbe ambao waliopo chini ya nusu ya wajumbe wote, basi Spika atathibitisha kuwa wajumbe waliopo ni chini ya nusu ya wajumbe wote atasimamisha kwa muda wa dakika tano, huku mhudumu kwa maelekezo ya katibu atapiga kengele kwa vituo yaani sio mfululizo.

Ningeomba sana hatuwezi kusoma hotuba ya bajeti ya Wizara kama hii mna watu 15 ndani ningeomba sana utumie busara zako Mhe. Mwenyekiti, tuahirishe kwa dakika tano baada ya muda tuendelee naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana katibu hebu hakikisha akidi ikoje.

Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa kanuni yetu kama ilivyosomwa hapa na Mjumbe, kwa sababu ukumbi haujakamilika naahirisha kikao hichi kwa dakika tano na wajumbe wote walioko nje warudi ndani haraka iwezekanavyo.

(Saa 11.05 Baraza liliahirishwa kwa muda wa dakika tano kutokana na kutokutimia kwa akidi)

(Saa 11.20 Jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kuna jambo kwanza lazima tuzungumze pamoja na kwamba tulichelewa kutoka najua mmechoka, lakini kitendo kama hichi si kizuri kukirudia tena. Kwa sababu tumeshindwa kuendesha kikao tukitizama mbele Serikali haipo na Serikali ndio inayohojiwa hapa, kwa hivyo tunapaswa *back benchers* wawepo lakini na benchi la mbele vile vile liwepo. Kwa hivyo tuwe makini katika kusimamia kanuni zetu na taratibu ambazo tumejiwekea. Ahsante.

Makadirio ya Mapato na Matumizi Kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 -Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni ya leo kutujaalia kufika hapa kwa ajili ya kuendeleza shughuli zetu, kabla sijaendelea naomba kidogo kufanya marekebisho unajua wataalam wazungu wanasema kuna *slippery of the tongue* lakini kumetokea sijui niseme *slippery of the computer*. Hiki kitabu hiki mkikitizama waheshimiwa kama mshaona pameandikwa mwaka wa fedha 16/17 lakini tulichokipeleka ambacho tumekifanyia *Proof reading* kilikuwa kinaonyesha 17/18 kumetokea nini huko uchapaji hatujui, lakini kwa ufupi tunaomba radhi mjue hilo kwamba tumelirekebisha kwamba pana makosa kidogo hapo mjue kwamba tumerekebisha ni 17/18.

Lakini ni suala ambalo linashangaza kwa sababu *draft* tuliyopeleka Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa inaonyesha wazi wazi kwamba ni 17/18 kwa hivyo naomba radhi kwa hilo hata kama mashine zimefanya makosa sisi ndio wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote, sinabudi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia afya njema, hekima na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kila siku ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kutupa rehema zake tuweze kutekeleza vyema mipango na malengo tuliojipangia kwa manufaa ya wananchi na nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima natoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein kwa umahiri wake katika kuiongoza Zanzibar. Chini ya uongozi wake, Serikali imetekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi ilizozitoa kwa wananchi wa Zanzibar wakati wa uchaguzi Mkuu kama zilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa nguvu na afya njema Rais wetu katika kuiongoza vyema Zanzibar yetu.

Mhe. Mwenyekiti, sote tunakumbuka kwamba, Mheshimiwa Rais aliahidi kupandisha kima cha chini cha mshahara kutoka TZS 150,000/= hadi TZS 300,000/= ifikapo Mwezi wa April 2017. Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuitekeleza ahadi hiyo. Hatua hii imeudhihirishia ulimwengu kwa kiasi gani Mheshimiwa Rais anavyowajali wafanyakazi wa Zanzibar na wananchi kwa ujumla na alivyo muungwana katika kutekeleza ahadi zake anazozitoa kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia kutumia nafasi hii kumpongeza kwa dhati Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mahonda kwa kusimamia vyema utekelezaji wa shughuli za Serikali ndani na nje ya Baraza lako kwa vitendo. Mafanikio ya Ofisi yetu kwa kiasi kikubwa yametokana na miongozo na maelekezo anayotupa ambayo yamesaidia sana katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe Mwenyekiti, pamoja na Mhe. Spika, Naibu Spika, na Mwenyekiti mwenzako

kwa kazi mbali mbali na majukumu unayotekeleza kwa ufanisi mkubwa chini ya uongozi wenu sisi wengi tumejifunza sana kwamba tunaweza tukafanya kazi kwa kushirikiana kwa pamoja na hekima zenu na busara zenu zimesaidia sana kuendeleza mbele juhudi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii maalum kuishukuru Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalumu za SMZ ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Machano Othman Said, Makamo wake na wajumbe wake wote, aidha namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya PAC Mhe. Miraji Khamis Mussa pamoja na Makamo wake na wajumbe wake wote kwa kazi nzuri walizofanya za kutushauri na kutuelekeza ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapiduzi Mhe. Haji Ussi Gavu Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka kwa uongozi wake mahiri na ushrikiano aliotoa wakati wa kukaimu nafasi yangu kwa vipindi viwili tofauti, aidha napenda kuwashukuru Mawaziri, Manaibu Mawaziri Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa mashirikiano yao jinsi walivyonisaidia katika kutekeleza majukumu ya ofisi yangu.

Mhe. Mwenyekiti, Natumia fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa Waziri anaeshughulikia masuala ya Utumishi wa Umma wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Angella Kairuki na watendaji wake wote kwa mashirikiano mazuri ya kikazi.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila ikiwa sitoishukuru familia yangu kwa msaada wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku. Bila ya ustahamilivu wao na mashirikiano yao nisingeweza kuitendea haki nafasi hii. Aidha, niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Makunduchi kwa kuendelea kuniunga mkono na naomba waendelee kuniunga mkono na mimi nawaahidi nitawatendea haki, na kutekeleza majukumu yangu ipasavyo katika kuwatumikia. Pia napenda kumshukuru Naibu Waziri wangu Khamis Juma Maalim Muwakilishi wa Jimbo la Pangawe kwa kusaidia vyema kutekeleza makumu ya ofisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru kwa moyo wote Katibu Mkuu Ndugu Yakout Hassan Yakout, Naibu Katibu Mkuu anaeshughulikia masuala ya Utumishi wa Umma, Ndugu Seif Shaaban Mwinyi na Naibu Katibu Mkuu anaeshughulikia masuala ya Katiba, Sheria na Utawala Bora Ndugu Kubingwa Mashaka Simba kwa mashirikiano yao makubwa wanayonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi yetu na katika kuandaa na kukamilisha hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumalizia shukurani zangu kwa kumshukuru Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa Jaji Mkuu, Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, DPP, Wenyeviti, Makamishna na Wajumbe wa Bodi, Watendaji Wakuu wa Kamisheni na Tume ya Utumishi Serikalini, Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa utendaji na ushirikiano wao wanaonipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Uwaziri kwa Ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii itahusisha maeneo manne makuu ambayo ni:- Muundo na majukumu ya Ofisi, Muhtasari wa Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017; Muhtasari wa Utekelezaji wa Malengo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na Muelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

MUUNDO NA MAJUKUMU YA OFISI

Mhe. Mwenyekiti, kimuundo Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria,Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina taasisi 22 zikiwemo Idara 8 zilizochini ya Wizara moja kwa moja na Taasisi 14 zinazojitegemea. Idara zilizo chini ya Wizara ni Kama ifuatavyo:-

i. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
iii. Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi;
iv. Idara ya Mipango Rasilimali Watu;
v. Idara ya Serikali Mtandao (E-Government)
vi. Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa;
vii. Idara ya Utawala Bora; na
viii. Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi zinazojitegemea ni pamoja na :

i. Kamisheni ya Utumishi wa Umma;
ii. Tume ya Utumishi Serikalini;
iii. Chuo Cha Utumishi wa Umma;
iv. Mahkama;
v. Tume ya Utumishi ya Mahkama;

vi. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu;
vii. Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka;
viii. Ofisi ya Mufti;
ix. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana;
x. Tume ya Kurekebisha Sheria;
xi. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi;
xii. Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
xiii. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na
xiv. Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina majukumu yafuatayo:-

i. Kuandaa na kusimamia Mipango, Sera, Sheria na Tafiti zinazohusiana na Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora;
ii. Kusimamia shughuli za Uendeshaji na Utumishi katika Ofisi;
iii. Kusimamia Utawala Bora ;
iv. Kusimamia shughuli za Mhimili wa Mahkama;
v. Kusimamia shughuli za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu;
vi. Kusimamia shughuli za Mkurugenzi wa Mashtaka;
vii. Kusimamia shughuli za Tume ya Kurekebisha Sheria;
viii. Kusimamia utekelezaji wa Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
ix. Kusimamia Utumishi wa Umma;
x. Kusimamia Utunzaji, uhifadhi, na utumiaji wa Nyaraka na Kumbukumbu;

Kusimamia Serikali Mtandao (e-Government)
xi. Kujenga uhusiano na ushirikiano mzuri na vyombo vya Kitaifa na Kimataifa;
xii. Kuratibu na kusimamia shughuli za Ofisi ya Mufti;
xiii. Kuratibu na kusimamia shughuli za Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana; na
xiv. Kusimamia shughuli za Ofisi ya Hakimiliki.

MUHTASARI WA MATUMIZI NA MAPATO
KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliidhinishiwa jumla ya Tzs.19,073,300,000/=. Hadi kufikia mwezi Machi 2017 jumla ya Tzs.13,094,802,554/= zimepatikana sawa na asilimia 69 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo, Tzs.8,281,551,084/= zilipangwa kulipia mishahara na stahiki mbalimbali za watumishi na Tzs.4,813,251,470/= kwa matumizi mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ilikadiriwa kutumia ruzuku ya Tzs.1,323,700,000/= na hadi kufikia Machi 2017 imepokea Tzs.1,015,383,384/= sawa na asilimia 77. Aidha, kwa kazi za maendeleo Tzs.1,740,195,000/= ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Tzs.900,000,000/= ni Mchango wa Serikali na Tzs.840,000,000/= ni msaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2017, Tzs.1,306,030,000/= zimepatikana sawa na asilimia 75, ambapo Tzs.647,430,000/= ni Mchango wa Serikali na Tzs.658,600,000/= zilitoka kwa Washirika wa Maendeleo.
Mhe. Mwenyekiti, Ofisi pia ilikadiria kukusanya Tzs.453,244,000/= ili kuchangia mapato ya Serikali. Hadi Machi, 2017, fedha zilizokusanywa ni Tzs.342,750,249/= sawa na asilimia 76.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inasimamia Mafungu 9 ambayo ni G01-Ofisi Kuu; G02 Mahkama; G03-Ofisi ya Mwanasheria Mkuu; G04-Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka; G05-Tume ya Kurekebisha Sheria; G06-Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; G07-Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi; G08-Kamisheni ya Utumishi wa Umma na G09-Tume ya Utumishi Serikalini.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2016/2017

G01- Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Mwenyekiti, Fungu la G01 linahusu Programu tano ambazo ni Programu ya Usimamizi wa Watumishi; Programu ya Usimamizi wa Nyaraka na Mawasiliano ya Serikali; Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora; Programu

ya Usimamizi wa Masuala ya Dini; na Programu ya Mipango na Utawala. Aidha, katika fungu hili la G01 kuna Programu ndogo kumi (10)

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017 utekelezaji wa programu za Fungu G01 ni kama ifuatavyo:-

Programu: Usimamizi wa Watumishi wa Umma

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii inatekeleza programu ndogo mbili ambazo ni Maendeleo ya Rasilimali Watu na Maendeleo ya Miundo na Mifumo ya Taasisi.

Programu ndogo*: Mendeleo ya Rasilimali Watu,*

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina lengo la kuendeleza mipango ya upatikanaji wa Watumishi wenye sifa watakaopelekea kutoa huduma bora kwa Wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, Programu hii imetoa mafunzo kwa Maafisa Utumishi juu ya utayarishaji wa Muongozo wa Mpango wa Rasilimali Watu wa miaka mitano Unguja na Pemba. Aidha, imefanya vikao vya Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi wa Wizara zote na kujadili masuala mbalimbali ya kiutumishi.

Mhe. Mwenyekiti, Mafunzo juu ya Muongozo wa Mpango wa uandaaji wa Viongozi katika Utumishi wa Umma Unguja na Pemba yametolewa. Aidha, mapitio ya mkataba wa udhamini wa mafunzo kwa watumishi wa umma yamefanyika. Pia Programu hii ndogo imeendesha majadiliano na kuidhinisha Mpango wa Rasilimali Watu wa miaka mitano katika Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2017/2021 kwa Wizara zote ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma kifungu cha 56.

Mhe. Mwenyekiti, Mfumo wa kieletroniki wa Taarifa za Watumishi umeimarishwa kwa kupata vifaa vya kutendea kazi ikiwemo kompyuta 8. Aidha, uratibu wa mafunzo yanayotolewa na washirika wa maendeleo umefanyika uliohusisha nafasi 47 za mafunzo mafupi nchini India, nafasi 8 za Shahada ya pili nchini Japani na nafasi 14 nchini Korea zimepatikana.

Programu ndogo*: Maendeleo ya Miundo na Mifumo ya Taasisi.*

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii inalengo la kuimarisha mfumo wa miundo ya kiutumishi na maslahi ya watumishi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, Programu hii imeratibu utayarishaji wa Mikataba ya Utoaji wa Huduma kwa Mteja katika Wizara na Taasisi za Serikali na kushiriki katika zoezi la Tathimini ya Kazi na Madaraja kwa mujibu wa uzito wa kazi husika *Job Evaluation and Grading Exercise.*

Mhe. Mwenyekiti, katika kusimamia Muongozo wa Upimaji Utendaji kazi kwenye Taasisi za Umma, *Program* hii imewapanga Watumishi wa Umma katika Miundo ya Utumishi kwa mujibu wa sifa za kielimu, uzoefu wa kazi na kufanya mapitio ya Miundo ya Utumishi na Miundo ya Mishahara. Aidha, imeingiza Miundo ya Utumishi katika mfumo wa Malipo ya Watumishi *Pay Roll System* pamoja na kufanya marekebisho ya Mishahara kwa Watumishi wa Umma.

Programu*:* Uimarishaji wa Kumbukumbu na Mawasiliano ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii inatekeleza program ndogo mbili ambazo ni Usimamizi na Uendeshaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa.

Programu ndogo: *Usimamizi na Uendeshaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.*

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ndogo ina lengo la kuendeleza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika utoaji wa huduma na shughuli za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, Programu hii ndogo imefanikiwa kuandaa miongozo mitatu ambayo ni Muongozo wa matumizi ya barua pepe, Muongozo wa usimamizi na uratibu wa miradi ya *TEHAMA* ya Serikali na Muongozo wa matumizi bora ya Kituo cha kuhifadhia taarifa. Vile vile, Programu hii kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeandaa Rasimu ya Mswaada wa Sheria ya Serikali mtandao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kuongeza uelewa juu ya dhana ya Serikali Mtandao, vikao 8 vilivyowahusishwa Wakurugenzi wa Utumishi na Uendeshaji, Wakurugenzi Mipango Sera na Utafiti, Maafisa *TEHAMA* wa

Serikali na waandishi wa habari Unguja na Pemba vimefanyika. Aidha, vipindi 3 vya Radio na Televisheni vimerushwa hewani vilivyozungumzia dhana ya Serikali Mtandao.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuratibu na kusimamia shughuli za TEHAMA, Programu hii imeandaa mfumo unaolenga kuweka tovuti *(Website Hosting)* katika Taasisi za Serikali zikiwemo Ofisi ya Rais Ikulu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

Programu ndogo*: Uhifadhi wa Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.*

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ndogo ina lengo la kuhifadhi na kusimamia Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kwa matumizi ya Serikali na jamii.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, Wizara 6, Taasisi na Mashirika 3 ya umma yamefanyiwa ukaguzi wa kumbukumbu na kupatiwa ushauri juu ya utunzaji na uhifadhi bora wa kumbukumbu ili kupunguza mrundikano wa majalada. Toleo maalumu la Udhibiti kumbukumbu zilizofungwa limetolewa kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali Unguja na Pemba. Aidha, mafunzo juu ya utunzaji na uhifadhi kumbukumbu yametolewa kwa watendaji 78 wanaosimamia utunzaji kumbukumbu na Masheha 198 Unguja na Pemba maelezo ya kina juu ya utekelezaji program hii yanapatikan kwenye hotuba ya bajeti ukurasa wa 12 hadi 15 .

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya majalada 203 yamehaulishwa kutoka mfumo wa karatasi kwenda mfumo wa ki-eletroniki. Kitengo cha ukusanyaji kumbukumbu simulizi kimeanzisha ambapo jumla *CDs* 56 za aina hiyo zimekusanywa na kuhifadhiwa. Aidha, huduma za utafiti zimetolewa kwa watafiti 226 ikiwemo wenyeji 221na wageni 5.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la ukosefu wa Ofisi ya Nyaraka Pemba limepatiwa ufumbuzi kwa kulifanyia matengenezo makubwa jengo la mahakama ya kale lililopo Kichugwani Chake - Chake, Pemba. Matengenezo ya jengo hilo yamekamilika na kukabidhiwa rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

Programu: Usimamizi wa Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, Program hii ina lengo la kuimarisha misingi ya Utawala Bora katika utekelezaji kwa Taasisi za Umma.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia machi 2017, progamu hii, imekusanya taarifa muhimu kwa ajili ya uandaaji wa ripoti ya mwaka ya masuala ya Utawala Bora. Taarifa hizo zimekusanywa kutoka katika Wizara, Taasisi za Serikali na kwa wananchi katika shehia ambapo shehia mbili zimehusika katika kila Wilaya za Unguja na Pemba, Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya kina juu ya utekelezaji wa program hii yanapatikana katika kitabu cha hotuba ukurasa wa15 hadi 17.

Mhe. Mwenyekiti, program hii imeandaa viashiria vya utawala bora ili vitumike katika kujipima kwa kiasi gani Taasisi zimefanikiwa au kutofanikiwa katika kutekeleza misingi ya utawala bora. Viashiria hivyo vitatumika pia katika kukusanya taarifa za kila robo mwaka zinazohusiana na utekelezaji wa utawala bora katika taasisi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Muongozo wa Utawala bora umeanndaliwa kusaidia watendaji wa Serikali na wahusika wengine ili kuimarisha misingi ya utawala bora katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku ikiwemo uwajibikaji, ufanisi na tija, haki za binadamu, mapambano dhidi ya rushwa, maadili ya viongozi na jamii kwa jumla. Aidha, elimu ya Utawala bora imetolewa kwa wananchi kupitia kamati za masheha ambapo jumla ya kamati 100 za Shehia zimefikiwa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuongeza kasi ya uwajibikaji katika sekta za umma na binafsi, mafunzo ya uwajibikaji yametolewa kwa watendaji mbali mbali wakiwemo Wakurugenzi Utumishi na Uendeshaji, Maafisa Wadhamini, Wahasibu Wakuu, Wakaguzi wa Ndani wa Hesabu, Maafisa Manunuzi, Maafisa Utumishi wa Wizara zote na Jumuiya zisizo za kiserikali (NGOs) Unguja na Pemba. Aidha, Walimu Wakuu wa Skuli za Sekondari za Wilaya ya Mjini wamepatiwa mafunzo yanayohusiana na utawala bora ambayo yamesaidia kuongeza kasi ya uwajibikaji.

Mhe. Mwenyekiti, vipindi 31 vimeandaliwa na kurusha hewani kupitia Shirika la Utangazaji (ZBC) ambavyo vinaelimisha masuala ya utawala bora. Kati ya hivyo, vipindi 21 vilirushwa hewani kupitia redio, vipindi 5 vilitangazwa katika televisheni na vipindi 5 vimerushwa kupitia maelezo baada ya habari.

Mhe. Mwenyekiti, vikao vya mashirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, vimefanyika vilivyo jadili masuala ya utawala bora, kubadilishana uzoefu, utaalamu na ushiriki wa Zanzibar katika vikao vya kikanda na kimataifa. Aidha Idara ilishiriki katika maazimisho ya siku ya maadili na haki za binadamu 10/12/2016 siku ya sheria duniani kuanzia tarehe 4 hadi tarehe 9 Februari, 2017 zikiwa na lengo la kuimarisha misingi ya utawala bora na utawala wa sheria.

Programu: Usimamizi wa Masuala ya Dini

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina lengo la kuratibu na kusimamia shughuli zinazoihusu Ofisi ya Mufti kwa kutoa Fatwa na kutoa miongozo kuhusu masuala ya dini.

Mhe.Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, mahusiano na Taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi na kuendeleza uhamasishaji wa amani na utulivu nchini. Aidha, maswala ya waumini mbali mbali yamejibiwa, migogoro ya kidini imetatuliwa, uratibu na usimamizi wa vikao vya Kamati ya Kitaifa ya kuthibitisha kuandama kwa mwezi umefanyika na kuendeleza utaratibu wake wakufanya ziara kwa baadhi ya Misikiti na Vyuo vya Qurani. Maelezo ya kina juu ya utekelezaji wa program hii yanaonekana ukurasa wa 17 hadi 19.

Mhe. Mwenyekiti, Misikiti 42 na madrasa 79 imetembelewa kwa madhumuni ya kuwakumbusha walimu wa madrasa na Maimamu juu ya wajibu wa kudhibiti na kupambana na mmong'onyoko wa maadili uliojitokeza ndani ya jamii yetu, pamoja na kukemea vitendo vya ubakaji, ulawiti madawa ya kulevya na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Aidha, jumla ya migogoro 123 inayohusiana na ndoa na talaka imepokelewa na kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, vipindi vya mawaidha ya dini ya Kiislamu vimetolewa kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar *(ZBC Redio)* vinavyohusu ihisani na wema wa dini nyengine, ndoa za utotoni na athari zake na tabia njema ni kizuizi cha fujo. Aidha, maswala mbali mbali yanayohusu ndoa, talaka, mirathi yamejibiwa na jumla ya vipindi 300 vya maswala na majibu vimerushwa kupitia *ZBC Redio*. Pia, Ofisi imepokea migogoro ya Misikiti 5 na kuipatia utatuzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuendeleza mahusiano mema kati ya Taasisi mbali mbali za kidini za ndani na nje ya nchi, Ofisi ya Mufti imepokea wawakilishi kutoka nchi tafauti ikiwemo; ujumbe wa Mufti Mkuu wa Msumbiji, ujumbe wa kidini kutoka Kuwait, ujumbe wa Tabligh kutoka Misri na wawakilishi wa Shule za Feza kutoka Uturuki. Pia, wawakilishi kutoka Balozi za Marekani, Ujerumani na Mashirika ya Kimataifa ikiwemo UNDP, SAVE THE CHILDREN, KONRAD ADENAUER ya Ujerumani wameitembelea Ofisi ya Mufti.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) limeahidi kuendeleza mashirikiano yake na Ofisi ya Mufti wa Zanzibar kwa kugharamia mikutano ya kudumisha amani na utulivu nchini kama ilivyofanya katika kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa 2015. Aidha, Chuo Kikuu cha Azhar cha Misri kimekubali kugharamia mafunzo ya mwezi mmoja ya uongozi kwa Taasisi za kidini kwa mashekhe 3 wa Zanzibar yatakayofanyika nchini Misri.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi ya Mufti, wafanyakazi 2 wamepatiwa fursa ya mafunzo kwa ngazi ya Shahada pamoja na kuimarisha Maktaba ya Kiislamu kwa kutafuta vitabu vyengine muhimu kwa ajili ya maktaba hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

Programu: Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti**,** Programu hii inatekeleza programu ndogo tatu ambazo ni Uongozi na Utawala; Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu wa Masuala ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Pemba.

Programu ndogo: *Uongozi na Utawala*

Mhe. Mwenyekiti, Program hii ina lengo la kutoa huduma za Ofisi, kusimamia Watumishi na kuratibu shughuli za Ofisi kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia machi 2017, kupitia programu hii, vikao 3 vya Kamati ya Uongozi, vikao 4 vya Kamati Tendaji, vikao 3 vya Bodi ya Zabuni

na vikao 3 vya Kamati ya Zabuni, pamoja na vikao 2 vya mashirikiano kati ya SMZ na SMT na vikao 2 vya Washirika wa Maendeleo vimefanyika. Vikao hivyo vilijadili masuala mbali mbali kuhusiana na mashirikiano na utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Maelezo zaidi yanapatikana ukurasa wa 19 hadi 20 wa kitabu cha bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii imeandaa Mkataba wa Utoaji wa Huduma kwa Mteja ambapo nakala 800 za mkataba huo zimecha pishwa. Mkataba huo utawekwa katika tovuti ya Wizara ili wananchi wapate fursa ya kuuelewa na kuutumia.

Mhe. Mwenyekiti, Semina na mafunzo mbali mbali yakiwemo mafunzo ya utunzaji kumbukumbu na nyaraka, mafunzo ya kuandaa Mpango wa Rasilimali Watu na Mpango wa Uandaaji wa Viongozi wa Wizara yamefanyika. Aidha, wafanyakazi 8 wakiwemo wanawake 5 na wanaume 3 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi nchini India na wafanyakazi 32 wakiwemo wanawake 20 na wanaume 12 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali nchini.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji zimetolewa zikiwemo upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

Programu ndogo: ***Mipango, Sera na Utafiti***

Mhe. Mwenyekiti, Program hii ndogo ina lengo la kuimarisha shughuli za Mipango, Sera na Utafiti na Usimamizi wa Programu/ Miradi ya Ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, kupitia programu hii mipango ya bajeti na ripoti za utekelezaji za kila robo mwaka zimeandaliwa na kuwasilishwa katika mamlaka husika. Aidha, programu hii imeandaa na kukamilisha Sera ya Malipo ya Watumishi na Wanasiasa. Sera ya Msaada wa Kisheria imewasilishwa katika kikao cha Makatibu Wakuu na kupata maoni. Sera ya Usimamizi wa Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ipo katika maandalizi. Vile vile, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini pamoja na ukusanyaji wa taarifa za Takwimu za Ofisi umeimarishwa.

Programu ndogo: *Kuratibu Shughuli za Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora*

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ndogo ina lengo la kutoa huduma za ofisi, kusimamia Watumishi na kuratibu shughuli za Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, programu hii imeratibu shughuli zote za Ofisi kwa upande wa Pemba. Kusimamia shughuli za uendeshaji na utumishi ikiwemo kuwajengea uwezo Watumishi ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Watumishi 4 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu ambapo wanaume 2 kwa ngazi ya Shahada ya kwanza na wanawake 2 kwa ngazi ya Stashahada. Aidha, jumla ya vikao 4 vya kazi vya Wakuu wa Taasisi na Idara vimefanyika. Maelezo ya kina juu ya utekelezaji wa program hii yanapatikana kwenye hotuba ya bajeti ukurasa 19 hadi 22.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

TAASISI ZINAZOPATA RUZUKU

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina taasisi 4 zinazopokea ruzuku ambazo ni: Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Chuo Cha Utawala wa Umma, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki. Utekelezaji wa majukumu katika taasisi hizo ni kama ifuatavyo:-

KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

Programu ndogo: *Usimamizi wa Masuala ya Dini*

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Kamisheni ya Wakfu ni kusimamia mali za Wakfu, Mali za Amana, Mirathi ya waislamu, Sala na Mabaraza ya Iddi kitaifa, Hijja, Zakka, Sadaka na Misaada ya Kheri.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, jumla ya tirka 1254 zilifunguliwa na tirka 1034 za mirathi zenye thamani ya Tzs.28,376,840,106.40/= zilifungwa na warathi kupewa haki zao. Aidha, ushauri wa kisheria kwa kesi 70 umetolewa, mizozo 30 imetatuliwa na 14 inaendelea kutafutiwa suluhu ambapo

mizozo 26 imepelekwa mahakamani na kesi 56 zimesimamiwa katika mahakama mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi na utunzaji wa Mali za Wakfu na Amana umeenedelea vyema. Jumla ya nyumba 567 zimekaguliwa, nyumba 26 zimefanyiwa matengenezo yaliogharimu Tzs.94,006,050/=. Kodi ya Tzs.438,280,170/= kwa nyumba na Tzs.3,915,000/= kwa mashamba imekusanywa. Maelezo ya kina juu ya utekelezaji wabajeti yanapatikana kwenye hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 22 hadi 24.

Mhe. Mwenyekiti, Zaka na misaada ya kheri yenye thamani ya Tzs.270,603,955/= imekusanywa na kugawiwa kwa wanufaika. Sala na Mabaraza ya Iddi Kitaifa yameratibiwa vyema ambapo Sherehe ya Iddi el Fitri ilifanyika Wilaya ya Mjini Unguja na Idd el Hajj ilifanyika Wilaya ya Mkoani Pemba kitaifa. Aidha, Kamisheni imeratibu safari za hijja ambapo jumla ya mahujaji 1077 kati ya mahujaji 1906 wa Tanzania nzima walisafirishwa na Taasisi za Hijja za Zanzibar. Maandalizi kwa ajili ya ibada ya Hijja ya mwaka 1438AH sawa na 2017 yanaendele.

Mhe. Mwenyekiti, elimu inayohusiana na majukumu ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imetolewa ambapo jumla ya vipindi 15 vya TV na redio vimerushwa hewani. Vipeperushi 611 na vitabu 5 vya Muongozo wa Wakfu pamoja na Muongozo wa Zaka vimegaiwa. Makala moja inayohusiana na masuala ya Wakfu imeandikwa katika gazeti la Zanzibar leo. Programu za uelimishaji kwa watoto, vijana, wazee na kinamama katika shehia ya Michamvi imefanyika pamoja na kushiriki katika maonyesho ya siku ya Sheria ili kukuza uelewa wa jamii juu ya majukumu ya Kamisheni ya Wakfu.

Mhe. Mwenyekiti, Watumishi 5 wakiwemo wanawake 3 na wanaume 2 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu. Watumishi 2 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya Wakfu na Mali ya Amana. Aidha, wafanyakazi 30 wakiwemo wanawake 11 na wanaume 19 wamepatiwa mafunzo ya ndani.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

CHUO CHA UTAWALA WA UMMA

Programu ndogo: *Kuwajengea Uwezo Watumishi wa Umma*

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii inalengo la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, jumla ya Watumishi 880 kutoka Wizara/Idara za Serikali, Taasisi zisizo za Serikali na Mashirika ya Umma wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali zikiwemo maadili na mawasiliano katika Utumishi wa Umma, Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma, utunzaji kumbukumbu, ununuzi na ugavi pamoja na utunzaji wa ghala.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya Watumishi wa Umma wapya 254 walipatiwa mafunzo elekezi. Watumishi 120 kutoka Taasisi mbali mbali za Serikali na Binafsi wamepatiwa mafunzo ya utatuzi wa migogoro na itifaki. Zoezi la kuimarisha Mitaala limeendelea ambapo mitaala 3 imeandaliwa kwa ajili ya mafunzo ya Shahada ya Kwanza katika fani ya Uongozi wa Rasilimali Watu, Utunzaji kumbukumbu na Uhusiano wa Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya Wanafunzi 1470 wanaendelea kupatiwa mafunzo ya muda mrefu. Wanafunzi 1450 wamefanya mitihani yao ya muhula wa Julai – Disemba, 2016 katika ngazi ya Cheti na Stashahada ambapo miongoni mwao Wanafunzi 1125 walimaliza Chuo na kutunukiwa Shahada katika Sherehe za Mahafali zilizofanyika mwezi machi 2017. Vilevile mahafali ya kwanza yamefanyika katika Tawi la Chuo Pemba ambapo Wahitimu 112 walitunukiwa Vyeti katika ngazi ya Cheti na Stashahada.

Mhe. Mwenyekiti, vikao 3 vya Baraza la Chuo vimefanyika ambapo vimejadili mambo mbali mbali ikiwemo uanzishwaji wa mafunzo ya Shahada ya Kwanza na mafunzo kwa watendaji wangazi tafauti Serikalini. Aidha, vikao 2 vya taaluma vimefanyika kujadili uanzishwaji wa mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za wanafunzi *(Data base)* na uchaguzi wa serikali ya wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

OFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI

Programu ndogo: Usimamizi wa Hakimiliki

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii inalengo la kuimarisha usimamizi wa hakimiliki kwa kuongeza ufanisi katika usajili, ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kwa wenye hakimiliki, na kuelimisha jamii juu ya dhana na masuala ya Hakimiliki.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, jumla ya kazi za hakimiliki 802 zimesajiliwa na kuingizwa katika mfumo wa kieletroniki kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu na kuwa na takwimu ya wanufaika wa mirabaha. Aidha Bodi ya hakimiliki imezindunduliwa na imeanza kufanya kazi zake kwa kutoa miongozo katika utekelezaji wa shughuli za Ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, Mirabaha yenye thamani ya Tzs.60,138,000/= imekusanywa kutoka kwa watumiaji mbali mbali wa kazi za hakimiliki kibiashara. Utaratibu wa kuzigawa kwa wenye hakimiliki wapatao 1,237 umeanza kufanyika. Aidha, wabunifu na wasanii wagonjwa 35 Unguja na Pemba wamepatiwa kiasi cha fedha kinachotokana na eneo malumu la mirabaha ambapo jumla ya Tzs.5,977,732/= zilitumika kwa shughuli hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi katika maeneo mbali mbali ya wauzaji kazi za hakimiliki umefanyika ambapo watumiaji 105 wa kazi za hakimiliki kibiashara wamekaguliwa, wakiwemo wenye maduka ya kuuza na kukodisha kazi za vinasa sauti vya kusikia na kuonekana. Watumiaji hao walielimishwa juu ya matumizi sahihi ya kazi za hakimiliki na kuwataka kukata leseni ili waweze kufanya biashara zao kihalali.

Mhe. Mwenyekiti, vikao viwili kati ya Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki na Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni vilivyolenga juu ya kupanga mikakati ya kupambana na uharamia, kusimamia maadili katika Sanaa, ubunifu na matumizi ya vielelezo vya sanaa za jadi (*Traditional Cultural Expressions*) vilifanyika.

Mhe. Mwenyekiti, vipindi 18 vya televisheni vilirushwa hewani kupitia ZBC-TV kwa lengo la kuwaelimisha watumiaji, wamiliki na jamii kwa jumla juu ya haki za wabunifu na wasanii. Vipindi hivyo pia vililenga kuelezea umuhimu wa kulipia Mirabaha kwa matumizi ya hakimiliki. Lengo ni kuinua kipato cha wabunifu, wasanii na Taifa kwa ujumla. Aidha, mfanyakazi 1 alihudhuria

mafunzo ya muda mfupi juu ya usimamizi wa hakimiliki katika mfumo wa kidijitali.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Programu ndogo: **Kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma**

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ndogo ina lengo la kusimamia maadili ya viongozi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2017 programu hii imepokea na kuhifadhi jumla ya fomu 1,620 za tamko la mali na madeni ya Viongozi wa Umma. Tume inaendelea kupokea fomu za Viongozi wapya, Viongozi walioshindwa kuwasilisha fomu zao kwa wakati na Viongozi wanaostaafu. Aidha, Viongozi ambao hawakuwasilisha kabisa au walichelewa kuwasilisha fomu zao bila ya sababu za msingi zinazokubalika, utaratibu wa kuwaita katika vikao vya Tume ya Maadili utafanyika. Orodha ya Viongozi wa Umma waliowasilisha fomu imeshachapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali (tangazo namba 10 na 40 la mwaka 2017) kama Sheria ya Maadili inavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza kazi ya uhakiki na uchunguzi wa taarifa za mali na madeni ya Viongozi wa Umma, watumishi 13 wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma wamepatiwa mafunzo maalum yanayohusiana na kazi hizo ambapo hatua inafuata ni kufanya uhakiki wa taarifa wa viongozi wa umma. Matarajio ya Tume ni kuanza kazi ya uhakiki katika kipindi cha robo 4 ya mwaka fedha April/June, 17.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya kina juu ya utekelezaji wa Tume ya Maadili yanapatikana kwenye hotuba ya bajeti ukurasa 28 hadi 30.

Mhe. Mwenyekiti, Tume imeendelea kuimarisha mfumo wa ki-elektroniki utakaotumika katika shughuli za usajili na uwekaji wa taarifa za mali na madeni ya Viongozi wa Umma. Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni uingizwaji wa taarifa za msingi za Viongozi wote wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, elimu imetolewa kwa Viongozi wa Umma kuhusu umuhimu wa Maadili kwa Viongozi wa Umma, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na utaratibu wa kujaza fomu za tamko la Mali na Madeni. Jumla ya Mikutano 30 imefanyika kati ya hiyo Unguja 24 na Pemba 6. Mikutano hiyo ilihusisha Viongozi wa Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Viongozi wa Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kukuza uelewa wa jamii juu ya Tume na Kazi zake, vipindi viwili vya Redio, vipindi viwili vya Televisheni vinavyozungumzia majukumu, uwezo wa Tume pamoja na wajibu wa Kiongozi wa Umma vimeandaliwa na kurushwa hewani. Aidha, vipeperushi 4,000 vinavyoitambulisha Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma vimechapishwa na kusambazwa. Tume imeandaa matangazo mafupi (*Jingles*) na mchezo wa kuigiza, lengo ni kuelimisha jamii.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuijengea uwezo Tume, mashirikiano na Ofisi ya Sekretariet ya Maadili ya Viongozi wa Umma Tanzania Bara yameimarishwa ambapo mafunzo kwa watendaji yametolewa. Uandaji wa Kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma namba 4/2015 na tafsiri ya Sheria hiyo zinaendelea kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

G02 - MAHKAMA KUU

Programu: Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina lengo la kusimamia utoaji na upatikanaji wa haki kwa kusikiliza na kutolea maamuzi kwa kesi za madai na jinai katika ngazi mbalimbali za Mahkama.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017 programu hii imetekeleza jukumu lake la usimamizi wa upatikanaji wa haki ambapo imesimamia jumla ya mashauri 16,795, miongoni mwa hayo mashauri 6,935 ni mapya na mashauri 9,860 ni ya zamani. Kati ya hayo, mashauri 12,595 yametolewa maamuzi. Angalia kiambatanisho 1.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Mradi wa Mageuzi ya Sekta ya Sheria *(Legal Sector Reform Program)* Mahkama inaendelea na hatua za kuanzisha mfumo wa kisasa wa kusajili kesi kwa kutumia mfumo wa kielektroniki. Aidha, mafunzo kwa maafisa TEHAMA na Makarani wa 25 wa Mahkama kuhusu matumizi ya mfumo huo yametolewa.

Mhe. Mwenyekiti, jengo la Mahkama ya watoto Mahonda Mkoa Kaskazini Unguja limekamilika na kufunguliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, Mahkama mpya ya mwanzo katika Wilaya ya Micheweni - Wingwi imefunguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuadhimisha Siku ya Sheria Zanzibar, kwa mara ya kwanza Mahkama iliweka mabanda ya maonesho katika viwanja vya Maisara kwa lengo la kuwaunganisha wahusika wote wa sekta ya sheria ili wananchi kupata taaluma ya kisheria kupitia maonesho hayo.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

G03 - OFISI YA MWANASHERIA MKUU

Programu: Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina lengo la kuishauri Serikali katika masuala ya kisheria ikiwemo kuandaa mikataba ya kitaifa na kimataifa, kutayarisha miswada ya sheria, kusimamia mashauri kwa niaba ya Serikali na kuandaa hati na Nyaraka za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017 jumla ya miswada 8 imeandaliwa na kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi kwa lengo la kupata sheria mpya au kufanyia marekebisho zile zilizoonekana na makosa. Aidha, Ofisi imeaandaa na kuchapisha kanuni 10 za Sheria mbali mbali ili kuzifanya sheria hizo zitekelezeke kwa ufanisi zaidi. Pia matangazo ya kisheria (*Legal Notice)* 132 yameandaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa usimamizi wa mikataba, Ofisi imeendelea na jukumu lake la kupitia na kutoa ushauri kwa mikataba mbali mbali iliyowasilishwa. Jumla ya Mikataba 129 na hati za maelewano (MOU) 21 zimepokelewa na kutolewa ushauri. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu

imeendelea kusimamia mashauri 77 Mahkamani. Miongoni mwa mashauri hayo, 20 ni mapya na 57 ni ya zamani. Kati ya mashauri hayo; 14 yametolewa uamuzi na mashauri 63 yanaendelewa kusimamiwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuwajengea uwezo watendaji wa Ofisi, mafunzo mbali mbali yametolewa kwa watendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na maafisa wengine wa Serikali. Mafunzo hayo yamehusu usimamizi wa Mikataba ya mafuta na gesi asilia, majadiliano (Negotiation skills) kupitia mikataba pamoja na usimamizi wa mikataba ya ujenzi ambayo iliwashirikisha wanasheria na wahandisi wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

G04 - OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Programu: Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii inalengo la kusimamia mashtaka yote ya jinai Zanzibar isipokua Mahkama za Kijeshi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, programu hii imesimamia kesi za jinai ambapo jumla ya kesi 1,779 zimefunguliwa katika mahkama mbali mbali za Unguja na Pemba. Kesi 1,420 zimeshatolewa uamuzi na kesi 359 zinaendelea katika hatua tofauti. Aidha, uendeshaji wa mashtaka katika Mahkama ya Wilaya Mkoa wa Kusini Unguja huko Makunduchi umeanzishwa.

Mhe. Mwenyekiti, mkakati wa kupambana na kesi za udhalilishaji umeanzishwa ambao unawahusisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mahkama pamoja na Jeshi la Polisi. Kupitia Mkakati huo, jumla ya kesi 54 zilifunguliwa na kuanza kusikilizwa mahkamani ndani ya mwezi wa Machi. Utekelezaji wa Mkakati huo umesaidia katika kuharakisha uendeshaji wa kesi na kupunguza matukio ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, elimu kwa umma imeendelea kutolewa kuhusu upatikanaji wa haki za jinai ambapo jumla nakala 2,000 za Jarida la Shahidi zimechapishwa na kusambazwa katika Ofisi zote za Masheha Unguja na Pemba, Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Wizara zote 13 za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi imeratibu vikao vya pamoja kati ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa na Wilaya kwa lengo la kujenga mashirikiano na kufanya kazi kwa pamoja ili kupata ushahidi kwa wakati. Aidha, vikao na Masheha wa Shehia zote kwa kila Wilaya Unguja na Pemba vimefanyika kwa lengo la kushajihisha upatikanaji wa haki za jinai kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, mkutano wa kuviweka pamoja vyombo vyote vya Serikali vinavyohusika na masuala ya makosa ya jinai umefanyika ambapo pamoja na mambo mengine umeshajihisha kupambana na makosa ya udhalilishaji wa wanawake na watoto pamoja na kesi za madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 6 wanaume 4 wanawake 2 katika kada ya sheria na utawala yametolewa na wanasheria 16 walihudhuria warsha mbali mbali za mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi ambayo yameongeza ujuzi wa kutekeleza vyema majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti (*Zanzibar Law Resource Centre)* kimeendelea kutoa mafunzo ya sheria kwa watendaji mbali mbali wakiwemo wanasheria na watendaji wengine wa Serikali na taasisi binafsi. Kituo kimeendelea kutoa mafunzo ya ngazi ya stashahada (*Diploma*) ya sheria pamoja na ngazi ya cheti.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

G05 - TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Programu: Usimamizi wa Mapitio ya Sheria

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, programu hii imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kukamilisha mapitio ya Sheria 6, ambazo ni Sheria ya kuanzisha Ofisi ya Mufti namba 9/2001, Sheria ya Usajili wa Nyaraka, Sura ya 99/1919, Sheria ya Urithi wa Ardhi, Sura ya 101/1926, Sheria ya Udanganyifu wa Mazao, Sura ya 109/1934, Sheria ya Fidia kwa wafanyakazi 15/1986 na Sheria ya Afya na Usalama Kazini namba 8/2005.

Mhe. Mwenyekiti, elimu imeendelea kutolewa kwa umma ambapo jumla ya vipindi 30 vikiwemo 19 vya Redio na 11 vya Televisheni ambapo vilirushwa

hewani kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC). Aidha, semina kuhusu mapitio ya Sheria kwa makundi mbali mbali zilifanyika wakiwemo Mahakimu, Mawakili wa kujitegemea, Wanasheria wa Serikali, Walimu, Wanafunzi, Viongozi wa Dini, Askari Polisi, Asasi za kiraia na wanajamii wa Wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa umeimarika kwa kushiriki mikutano mbali mbali na kulipia ada za uanachama wa Umoja wa Tume za Kurekebisha Sheria za Afrika Mashariki na Kusini (ALRAESA) na Umoja wa Tume za Kurekebisha Sheria za nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola (CALRAs) kwa mwaka 2016/ 2017.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli za uendeshaji zimesimamiwa ambapo mafunzo yametolewa kwa watendaji wa Ofisi. Watumishi 2 wanaendelea na mafunzo ya Shahada ya Pili katika fani ya Sheria chini ya udhamini wa Washirika wa Maendeleo. Aidha, mafunzo ya ndani kuhusiana na uandishi wa Sheria, mafunzo ya zimamoto na uokozi na mafunzo ya huduma ya kwanza yamefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

G06 - OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Programu: Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina lengo la kufanya ukaguzi wa mazingira, ukaguzi wa kompyuta, ukaguzi wa maeneo hatarishi *(Risk based Audit)*, ukaguzi yakinifu *(Value for Money)* na mafunzo ya muongozo wa ukaguzi *(Regulatory Audit Manual).*

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, Ofisi imeendelea na majukumu yake ya ukaguzi wa mahesabu ya mwaka 2015/2016 katika Taasisi mbali mbali za Serikali kwa kufuata muongozo wa ukaguzi ambapo Wizara zote za Serikali, Mashirika, Taasisi pamoja na miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo zilikaguliwa. Aidha, Ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2014/2015 imekamilika na tayari imeshawasilishwa kwa mamlaka husika kama Sheria inavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, mafunzo ya muda mfupi yametolewa kwa Watumishi 25 wanawake11na wanaume14 katika maeneo ya ukaguzi yakinifu, tathmini ya kugundua maeneo hatarishi ya ukaguzi *(Risk Based Audit)* na mafunzo ya viwango vya ukaguzi vya kimataifa. Aidha, mafunzo ya muda mrefu yametolewa kwa Watumishi 15 wanawake 8na wanaume7 katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukaguzi wa hesabu za viinua mgongo pamoja na fidia kufikia Machi 2017, Ofisi imekagua majalada 1,630 ya wastaafu pamoja na fidia kwa wafanyakazi walioumia kazini. Kati ya hayo majalada 780 yamekaguliwa kwa ajili ya malipo yanayotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango, majalada 845 yamekaguliwa kwa upande wa malipo ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) na majalada 5 kwa ajili ya fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

G07 - MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI

Programu: Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina lengo la kutoa elimu kwa Umma juu ya kuchukuwa hatua za kinga dhidi ya Rushwa na kufanya uchunguzi wa vitendo vya Rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017, jumla ya tuhuma 71 za makosa mbali mbali yakiwemo kuomba na kupokea Rushwa, matumizi mabaya ya Ofisi, matumizi mabaya ya mali za umma, kukwepa kulipa kodi, Rushwa katika zabuni na Rushwa katika uchaguzi yameripotiwa na kuchunguzwa. Kati ya tuhuma hizo tayari majalada 11 yamefikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua za kisheria na majalada 4 yapo mahkamani.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii imefanikiwa kufanya udhibiti katika mashindano ya Mpira wa Miguu ya Kombe la Mapinduzi (Mapinduzi Cup) na kufanikisha kuongezeka kwa mapato yaliyotokana na mechi hizo kwa ZFA. Vilevile, Mamlaka ilifanikiwa kufanya udhibiti kwa upande wa Bandarini Pemba kwa meli ya Mapinduzi II kwa lengo la kuokoa upotevu wa Mapato ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa elimu juu ya Rushwa na athari zake inawafikia wananchi, Programu imefanikiwa kuanzisha Ofisi inayotembea *(Mobile Office)* ili kurahisisha utoaji wa huduma zake na kuwafikia wananchi katika maeneo yao. Hatua hii imesaidia sana katika kuwafanya wananchi kutambua uwepo wa Mamlaka na kuweza kuripoti vitendo vya rushwa vinavyotokea katika maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti, Mikutano iliyolenga kukuza uelewa wa jamii kuhusu majukumu ya Mamlaka na umuhimu wa kuepuka vitendo vya Rushwa imefanyika kwa taasisi za Serikali Unguja na Pemba. Mikutano hiyo ilihusisha taasisi mbali mbali ikiwemo ZRB, ZAWA, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Jeshi la Polisi. Aidha, vipindi vya redio na Televisheni vimeendelea kutolewa ili kuwapatia wananchi elimu juu ya madhara ya rushwa na athari zake.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii imefanikiwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu watendaji wake ndani na nje ya nchi ili kuweza kufanikisha kazi za Mamlaka kama zilivyopanga. Mafunzo haya yalihusisha fani mbali mbali ikiwemo biashara na uwekezaji, hesabu za manunuzi na upelelezi *('Tax Avoidance and Avasion' and 'Advanced finger Print').*

Mhe. Mwenyekiti, programu imefanikiwa kuadhimisha Siku ya Rushwa Duniani tarehe 10/12/2016 zilijumuisha taasisi tano zinazosimamia maadili na utawala bora. Taasisi hizo ni pamoja na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Idara ya Utawala Bora, Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora, Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma pamoja na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mgeni Rasmi katika maadhimisho hayo alikuwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

G08: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Programu: Usimamizi wa Watumishi wa Umma

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina lengo la kuimarisha mifumo ya uendeshaji wa usimamizi wa Rasilimali watu katika utumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia machi 2017, Programu hii imefanikiwa kuchapisha na kusambaza nakala 1,300 za Muongozo wa Ajira pamoja na kujenga Uelewa juu ya Muongozo huo kupitia semina 6 kwa Maafisa Utumishi wa Taasisi za Umma, Wakala Tendaji na Mashirika ya Umma Unguja na Pemba. Aidha, Semina hizo zitaendelea kwa wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Watendaji Wakuu kwa upande wa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ziara 9 zimefanyika kwa upande wa Pemba zinazohusu masuala mbali mbali ya Kiutumishi. Rasimu ya Muongozo wa Ukaguzi wa Afya na Usalama kazini imeandaliwa. Malalamiko 8 na rufaa moja zimepokelewa na kutolewa uamuzi. Aidha, mapendekezo ya Miundo ya Utumishi, Miundo ya Taasisi na Miundo ya Mishahara kutoka katika Taasisi mbali mbali za Umma yamepokelewa na kushughulikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

G09: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Programu: Usimamizi wa Watumishi Serikalini
Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina lengo la kusimamia uajiri na kuimarisha maadili na haki za Watumishi Serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia machi 2017, kupitia programu hii, jumla ya nafasi za ajira 348 zilitangazwa kupitia *ZBC Redio* na Televisheni, kufanyiwa usaili, na kutolewa kibali cha ajira kwa Unguja na Pemba. Aidha, malalamiko 2 yaliwasilishwa na kutolewa maamuzi. Angalia kiambatanisho nambari 2

Mhe. Mwenyekiti, watumishi 15 wameongezwa muda wa utumishi na ajira za mkataba kwa watumishi 14 zimeidhinishwa. Watumishi 4 wamepewa ruhusa ya likizo bila ya malipo, 31 wamestaafu kazi kwa hiari, watumishi 9 wamestaafishwa kazi kwa maradhi na watumishi 577 wamestaafishwa kazi baada ya kufikia umri wa lazima.

Mhe. Mwenyekiti, watumishi 477 wamethibitishwa kazi, 29 wamebadilishwa kada na watumishi 9 wameacha kazi kwa hiari. Aidha, makosa ya kinidhamu kwa watumishi 2 yamewasilishwa na kutolewa maamuzi ambapo watumishi hao wamefukuzwa kazi baada ya kuthibitika wamefanya makosa ya kinidhamu. Angalia kiambatanisho nambari 3.

Mhe. Mwenyekiti, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa zikiwemo mafunzo, upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

MUELEKEO WA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kuchukua nafasi hii kutoa maelezo ya muelekeo wa programu zinazosimamiwa na Ofisi yangu kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

VIPAUMBELE VYA OFISI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imejipanga kutekeleza vipaumbele vifutavyo:-

i. Ujenzi wa jengo la Mahkama Kuu Tunguu.
ii. Kuratibu Mradi wa Huduma za Serikali Mtandao awamu ya pili *(e-health na e-Tax).*
iii. Kuimarisha misingi ya Utawala Bora.
iv. Kuimarisha Utumishi wa Umma na Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, vipaumbele hivi vinaendana na Malengo Makuu ya Taifa (Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar – MKUZA III) pamoja na Malengo ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu na Sera za Kisekta. Pia, vipaumbele vimezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2015-2020, Mwelekeo wa Sera za Chama cha Mapinduzi 2010-2020 na Hotuba za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt Ali Mohamed Shein.

Malengo Makuu ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuimarisha upatikanaji wa haki na Utawala wa Sheria;

ii. Kuimarisha Miundo mbinu katika Sekta ya Sheria na Utumishi wa Umma;
iii. Kuweka Miundo ya Taasisi na kusimamia mipango endelevu ya upatikanaji wa Rasilimali Watu wenye sifa;
iv. Kuimarisha usimamizi wa masuala ya dini;
v. Kuimarisha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma;
vi. Kuimarisha uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa;
vii. Kuimarisha Mawasiliano ya Serikali Mtandao; na
viii. Kuimarisha misingi ya Utawala Bora na maadili katika utendaji wa shughuli za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Katiba Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ina jumla ya Programu kuu 13 na Programu ndogo 29. Kati ya hizo programu 5 kuu na 13 ndogo zinasimamiwa na kutekelezwa kupitia Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu; na programu 8 kuu na 16 ndogo zinatekelezwa na Taasisi zinazojitegemea. Programu hizo zote zinagawika katika sehemu mbili kuu; ambazo ni utekelezaji wa majukumu ya msingi pamoja na shughuli za uendeshaji wa Ofisi. Maelezo kamili ya programu hizo ni kama ifuatavyo;-

Programu kuu: Mipango na Utawala

Programu ndogo: Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kuandaa mipango ya bajeti na mapitio ya utekelezaji wake, kuandaa Mpango wa Ufuatiliji na Tathmini wa Ofisi kwa miaka mitano, Mipango ya Utekelezaji wa Sera ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa, Sera ya Msaada wa Kisheria, Sera ya Mafunzo ya Watumishi wa Umma na Sera ya Malipo ya Watumishi wa Umma na Wanasiasa. Aidha, Idara imepanga kuratibu shughuli za uanzishwaji wa Bima ya Afya Zanzibar na kufanya Tafiti ndogo ndogo kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, Ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.1,445,696,820/= ambapo kati ya hizo Tzs.249,914,820/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.120,400,000/= zitatumika kwa matumizi mengineo. Aidha, Tzs.50,000,000/= kwa matumizi ya miradi ya maendeleo ikiwa ni mchango wa SMZ na Tzs.1,025,382,000/= kutoka kwa washirika wa maendeleo

Programu ndogo: Uongozi na Utawala

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imepanga kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi 38 ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao, kuimarisha usalama wa majengo, afya za wafanyakazi na mazingira yanayozunguka Ofisi, kuimarisha matumizi ya miongozo mbalimbali ya kiutumishi ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji kwa lengo la kutoa huduma bora kwa Umma, kuimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha na manunuzi wa Ofisi na kutoa huduma za Uendeshaji wa Ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.1,588,805,700/= ambapo kati ya hizo Tzs.978,805,700/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.610,000,000/= zitatumika kwa matumizi mengineyo.

Programu ndogo: Kuratibu shughuli za Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Pemba

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kuendelea kuratibu shughuli za Ofisi Pemba, kusimamia shughuli za jumla za Uendeshaji wa Ofisi, kuwajengea uwezo watumishi wa Ofisi walioko Pemba ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo na kulipa stahiki za watumishi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.1,020,819,860/= ambapo kati ya hizo Tzs.850,819,860/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.170,000,000/= zitatumika kwa matumizi mengineyo.

Programu kuu: Usimamizi wa Watumishi wa Umma

Programu ndogo: Usimamizi wa Mipango na Maendeleo ya Watumishi

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kuendesha mafunzo kwa watumiaji wa mfumo wa kieletroniki wa taarifa za watumishi Unguja na Pemba, kufanya tathmini ya mfumo wa kieletroniki wa Rasilimali watu, kutoa mafunzo juu ya muongozo wa uandaaji viongozi katika Utumishi wa Umma, kukamilisha Muongozo wa Tathmini ya Mafunzo, kufanya majadiliano juu ya Mpango wa Rasilimali Watu kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kuidhinisha Mpango wa Uratibu kwa wizara zote, kuendesha vikao

kwa Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi na kujenga mashirikiano ya kimataifa katika masuala ya kiutumishi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.273,092,040/= ambapo kati ya hizo Tzs.180,092,040/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.93,000,000/= zitatumika kwa matumizi mengineyo.

Programu ndogo: Usimamizi wa Miundo, Mifumo na Maendeleo ya Watumishi

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kufanya uhakiki na ukaguzi wa Mishahara ya Watumishi, kutoa uelewa kuhusu upimaji utendaji kazi katika Taasisi za Umma, kupitia na kuimarisha Miundo ya Utumishi, kuadhimisha siku ya Utumishi wa Umma Duniani, kuwajengea uwezo maofisa wa Idara ya Miundo ya Taasisi, kutayarisha na kutoa ufafanuzi kuhusu Miongozo na Matoleo ya Kanuni za Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.349,216,480/= ambapo kati ya hizo Tzs.234,216,480/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.115,000,000/= zitatumika kwa matumizi mengineyo.

Programu kuu: Uimarishaji wa Kumbukumbu na Mawasiliano ya Serikali

Programu ndogo: Usimamizi na Uendeshaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kuandaa Mhe miongozo mbali mbali ya usimamizi wa TEHAMA na utoaji wa huduma kwa wananchi, kuelimisha watendaji na wananchi juu ya dhana na huduma za Serikali Mtandao awamu ya pili *(e - health and e – tax)*, kuratibu na kusimamia miradi ya Serikali Mtandao na kuwajengea uwezo wa kitaalamu maafisa TEHAMA.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.10,658,144,200/= ambapo kati ya hizo Tzs.283,144,200/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi,

Tzs.325,000,000/= zitatumika kwa matumizi mengineo. Aidha, Tzs.50,000,000/= ikiwa ni mchango wa SMZ na Tzs.10,000,000,000/= kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Programu ndogo: Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kufanya ukaguzi wa Kumbukumbu na kutoa ushauri wa utunzaji na uhifadhi bora wa Kumbukumbu kwa Wizara pamoja na taasisi zake, kuhaulisha majalada kutoka mfumo wa karatasi kwenda mfumo wa ki-eletroniki, kuondoa mirundikano ya majalada yaliofungwa katika Wizara, Idara na Taasisi za Umma, kukusanya Kumbukumbu Simulizi na kuzihifadhi, kuendelea kutoa huduma kwa watafiti mbalimbali wanaofika katika Jumba la Nyaraka.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.524,677,000/= ambapo kati ya hizo Tzs.331,677,000/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.193,000,000/= zitatumika kwa matumizi mengineyo.

Programu kuu: Usimamizi wa Utawala Bora

Programu ndogo: Usimamizi wa Utawala Bora na Haki za Binadamu

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kutayarisha Mpango Mkakati wa Utawala Bora Zanzibar, kufanya mapitio ya Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011, kuendelea kuelimisha jamii juu ya misingi ya utawala bora kwa kufanya makongamano na semina kwa taasisi za Serikali na mikutano kwa makundi mbali mbali ya kijamii na kuendesha mikutano ya robo mwaka kwa Kikundi Kazi cha Utawala Bora. Pia, Idara imepanga kuendeleza mashirikiano baina ya SMT na SMZ katika masuala ya Utawala Bora ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.233,806,720/= ambapo kati ya hizo Tzs.133,806,720/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.100,000,000/= zitatumika kwa matumizi mengineyo.

Programu kuu: Usimamizi wa Masuala ya Dini

Programu ndogo: Usimamizi wa Masuala ya Dini

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kufanya mikutano kwa mabaraza ya Misikiti na Madrasa, kuendeleza mashirikiano na Taasisi za Nje na ndani za kiislamu, kufanya ziara za kutembelea Misikiti na Madrasa, kutatua migogoro ya ndoa, talaka, misikiti, madrasa, kufanya vikao vya Baraza la Ulamaa, kuchapisha mtaala wa madrasa za Qur-an, kufanya vikao vya kuthibitisha kuandama kwa mwezi, kuchapisha Sheria ya Ofisi ya Mufti na kutoa uelewa kwa wananchi juu ya Sheria hiyo na kufanya mikutano ya Amani na utulivu na kupiga vita vitendo vya udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.500,455,260/= ambapo kati ya hizo Tzs.308,455,260/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.192,000,000/= zitatumika kwa matumizi mengineyo.

G02: MAHKAMA

Programu: Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kusikiliza na kutoa maamuazi ya kesi za madai na jinai katika ngazi zote za Mahkama, kutumia mfumo wa kisasa wa uendeshaji wa kesi kwa njia ya kielektroniki, kutoa huduma za Uendeshaji wa Mahkama na kuanza rasmi ujenzi wa jengo jipya la Mahkama Kuu Tunguu.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.6,996,601,200/=ambapo kati ya hizo Tzs.4,761,601,200/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za wafanyakazi, na Tzs.1,335,000,000/= zitatumika kwa matumizi mengineo. Tzs.500,000,000/= zinatarajiwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya Serikali. Aidha jumla ya Tzs.900,000,000/= zimeingizwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

GO3: AFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Programu: Mageuzi ya Utoaji Huduma za Sheria na Usimamizi wa Shughuli za Utawala

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali na Taasisi zake. Kuandaa Miswada, Kanuni, Matangazo ya Kisheria, kutoa miongozo ya kisheria, kufuatilia indhari za kushtakiwa Serikali na kuiwakilisha Serikali Mahkamani kwenye kesi za Madai.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya Tzs.1,646,109,000/= zitatumika. Kati ya hizo Tzs.752,509,000/= kwa mishahara na stahiki za wafanyakazi na Tzs.893,600,000/= kwa matumizi mengineo.

GO4: AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Programu: Uendeshaji na Usimamizi wa Kesi za Jinai

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga uendeshaji na usimamizi wa kesi za jinai kiraia, kukuza mipango na uendeshaji wa Ofisi na kukiendeleza Kituo cha Mafunzo, Sheria na Utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.2,329,100,000/= ambapo kati ya hizo Tzs.1,378,500,000/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.895,000,000/= zitatumika kwa matumizi mengineo na Tzs.55,600,000/= kwa ajili ya Ruzuku ya kukiendeleza Kituo cha Mafunzo na Sheria na Utafiti Zanzibar.

GO5: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Programu: Usimamizi wa Mapitio ya Sheria za Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kuzifanyia mapitio Sheria 7, Sheria ya Jumuiya namba 6/ 1995, Sheria ya Msimamizi wa Mirathi sura ya 23/1925, Sheria ya Mahkama Kuu namba 2/1985, Sheria za Mahkama za Chini namba 6/1985, Sheria ya Udhibiti wa Kodi sura ya 98/1957, Sheria ya Kuhifadhi Utamaduni wa Taifa namba 1/1973

na Sheria ya Kamati ya Uongozi namba 10/1986. Aidha, Tume imepanga kutoa elimu kwa Umma, kutafsiri Sheria kwa lugha nyepesi ya Kiswahili, kuimarisha utendaji wa kazi za Tume na kuimarisha Ushirikiano na Taasisi zenye majukumu sawa na Tume Kikanda na Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.584,400,000/= ambapo kati ya hizo Tzs.233,200,000/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.351,200,000/= zitatumika kwa matumizi mengineyo.

GO6: AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Programu: Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kukagua hesabu za Serikali na Taasisi zake zote kwa kutumia mfumo wa ukaguzi unaozingatia matokeo ya malengo ya bajeti ya mfumo wa *program (PBB Audit).* Aidha, itaendelea kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kitaaluma katika fani mbali mbali za ukaguzi kama vile ukaguzi unaozingatia matokeo *(Performance Audit),* ukaguzi wa mazingira, ukaguzi wa komputa *(IT Audit),* ukaguzi yakinifu *(Value for Money Audit),* kupitia na kurekebisha muongozo wa ukaguzi *(Regulatory Audit Manual)* na kushajihisha matumizi ya viwango vya ukaguzi vilivyowekwa kitaifa na kimataifa katika ufungaji wa hesabu.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.2,627,200,000/= ambapo kati ya hizo *Tzs.1,389,200,000/=* zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.1,238,000,000/= zitatumika kwa matumizi mengineo na Tzs.84,555,000/= ikiwa ni makusanyo katika kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

GO7: MAMALAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI

Programu: Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi. Kuendelea na shughuli za kiuchunguzi kwa makosa mbali mbali ya Rushwa. Kuandaa

Mpango Mkakati wa Mamlaka, kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya madhara ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa katika programu hii katika mwaka 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.1,334,700,000/= ambapo kati ya hizo Tzs.754,000,000/= kwa matumizi ya Mishahara na Tzs.580,700,000/= kwa matumizi mengineyo.

GO8: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Programu: Usimamizi wa Utumishi wa Umma

Mhe. Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa katia programu hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018 naliomba Baraza lako tukufu programu hii imepanga kuendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi katika kusimamia masuala yote ya kiutumishi ikiwemo kuwezesha na Kusimamia Tume za Utumishi, Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Wakala wa Serikali kufikia utawala unaolenga matokeo bora. Kufuatilia na kutathmini usimamizi wa Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma kwa kufanya Uchunguzi na Ukaguzi wa Kawaida na Ukaguzi wa Kushitukizia. Kupokea na kushughulikia Rufaa na Malalamiko dhidi ya maamuzi yaliyotolewa na Mamlaka za Ajira na Mamlaka za nidhamu katika Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.940,300,000/= ambapo kati ya hizo Tzs.390,600,000/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.549,700,000/= zitatumika kwa matumizi mengineyo.

GO9: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Programu: Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kuandaa na kusimamia shughuli za ajira kwa kuzingatia sifa na vigezo vinavyostahiki, kupokea na kusikiliza malalamiko ya watumishi dhidi ya maamuzi yaliyotolewa na mamlaka za nidhamu na kuratibu uidhinishwaji wa ajira za mkataba, kuthibitisha kazi, kubadilisha kada, kuidhinisha likizo bila ya malipo na kustaafisha kisheria watumishi wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tzs.511,800,000/= ambapo kati ya hizo Tzs.191,000,000/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.320,800,000/= zitatumika kwa matumizi mengineyo.

TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU

KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

Programu ndogo: *Usimamizi wa Masuala ya Dini*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, programu hii imepanga kuimarisha utoaji huduma za mirathi, Wakfu na Mali za Amana, kuimarisha shughuli za uratibu na mawasiliano, kujenga mazingira bora ya kazi kwa watendaji, kushajihisha wananchi na wafadhili mbali mbali juu ya utoaji zakka na misaada ya kheri, kusimamia Sala na Mabaraza ya Idd Kitaifa na kuratibu shughuli za Hijja.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha program hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha ruzuku ya Tzs.825,800,000/= ambapo kati ya hizo Tzs.577,400,000/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.248,400,000/= zitatumika kwa matumizi mengineo na kukusanya Tzs.130,084,00/= kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

CHUO CHA UTAWALA WA UMMA

Programu ndogo: *Kuwajengea Uwezo Watumishi wa Umma*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Chuo kimepanga kuwaendeleza Watumishi wa Umma kiutendaji, kuibua na kuandaa Tafiti mbalimbali zinazohusiana na Utumishi wa Umma pamoja na kutoa huduma za ushauri elekezi na kukuza uwezo wa kitaaluma kwa Watumishi wa Umma na wanafunzi wengine katika ngazi ya Msingi, Cheti, Stashahada na Shahada.

Mhe. Mwenyekiti, ili kukiwezesha program hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha ruzuku ya Tzs.604,500,000/= ambapo kati ya hizo

Tzs.567,700,000/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.36,800,000/= zitatumika kwa matumizi mengineyo.

AFISI YA HAKIMILIKI

Programu ndogo: *Usimamizi wa Hakimiliki*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, program hii imepanga kuimarisha usimamizi wa Hakimiliki kwa kuongeza idadi ya kazi zinazosajiliwa na kukusanya mirabaha yenye thamani ya Tzs.80,000,000/= na kuimarisha shughuli za utawala.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha Ofisi kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha ruzuku ya Tzs.260,000,000/= ambapo kati ya hizo Tzs.100,000,000/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.160,000,000/= zitatumika kwa matumizi mengineyo.

TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Programu ndogo: *Kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii imepanga kupokea, kuhifadhi na kusajili taarifa za mali na madeni ya Viongozi wa Umma, kufanya uhakiki wa taarifa za Viongozi wa Umma, kupokea malalamiko na kufanya uchunguzi wa uvunjwaji wa Sheria ya Maadili, kuelimisha Viongozi wa Umma na Wananchi kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili na kuijengea uwezo Tume.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha Ofisi kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha ruzuku ya Tzs.579,267,920/= ambapo kati ya hizo Tzs.79,267,920/= zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Tzs.500,000,000/= zitatumika kwa matumizi mengineo.

SHUKURANI

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu. Naomba niwashukuru kwa dhati wahusika na washirika mbali mbali wa maendeleo kwa ushirikiano mzuri walioutoa kwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao umerahisisha utekelezaji wa

malengo tuliojipangia. Miongoni mwao ni Jumuiya ya Ulaya *(EU)* Shirika la Maendeleo ya Kimataifa *(UNDP), UNICEF*, *UNFPA*, Shirika la Kimataifa la Mali za Ubunifu (WIPO), Jumuiya ya Kiafrika ya Uongozi na Utawala wa Umma *(AAPAM),* Benki ya Dunia, Afrika Muslim *Agency*, na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB).*

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kutoa shukrani za dhati kwa Benki ya Maendeleo ya Kiislam *(IDB),* Mamlaka ya Wakfu wa Uturuki, Wizara ya Awkaaf ya Algeria, Serikali ya Saudi Arabia, taasisi ya *World Monument Fund*, taasisi zinazopeleka mahujaji na taasisi za misaada ya kheri Zanzibar. Aidha, tunawashukuru Save the Children, Nchi ya China, India, Korea, Japani, Indonesia, Uingereza, Marekani, South Africa, Oman, Uturuki na Egypt.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi inatoa shukrani kwa vyombo vinavyosimamia Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora vya Jamhuri ya Muungano kwa mashirikiano yao mema. Vile vile tunatoa shukrani kwa Chama cha Wanasheria Zanzibar (ZLS), Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC), Chama cha Wanasheria Wanawake (ZAFELA), Chama cha Waandashi wa Habari Wanawake (TAMWA) na Shirikisho la vyama vya Wafanyakazi Zanzibar. Aidha, shukrani zetu ziwaendee Masheha na wananchi wote kwa jumla. Mwisho navishukuru sana vyomba vyetu vya habari kwa kazi nzuri walioifanya ya kutoa elimu na kutangaza matukio mbali mbali yaliyohusu shughuli za Ofisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla naomba niwashukuru wote walioisaidia Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Shukrani zangu za pekee ziwaendee Watendaji Wakuu na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano wao wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, naomba kuwambia washirika wetu wote kwamba Ofisi itaendelea kuthamini kwa dhati michango yao ya hali na mali pamoja na ushirikiano wanaotupatia kila tunapowahitaji. Sina cha kuwalipa zaidi ya kusema ahsante sana na tunawathamini. Kwa niaba ya Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tunaomba mzipokee shukrani zetu, ahsanteni na Mungu awabariki.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kukumbusha kuwa Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inayo dhima ya

kuhakikisha kuwa masuala yanayohusu ufikishwaji wa huduma kwa wananchi pamoja na upatikanaji wa haki zao kwa wakati yanasimamiwa ipasavyo. Utekelezaji wa Mkakati wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria na Mkakati wa Mabadiliko katika Utumishi wa Umma unalenga kuongeza ufanisi katika kufikia malengo ya MKUZA III, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu Duniani.

Mhe. Mwenyekiti, naomba wajumbe wa Baraza lako tukufu wachangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimaye waidhinishie Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora jumla ya Tzs.35,778,892,200/= kwa matumizi ya mwaka wa fedha 2017/2018. Kati ya fedha hizo Tzs.14,725,910,200/= ni kwa matumizi ya mishahara, Tzs.9,027,600,000/= kwa matumizi ya mengineyo, aidha Tzs.1,000,000,000/= ni kwa matumizi ya miradi ya maendeleo kwa SMZ na Tzs.11,025,382,000/= kwa washirika wa maendeleo. Naomba pia Baraza lako likubali Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ichangie Tzs.714,639,000/= kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitowe iamuliwe)

SHUGHULI ZA TUME YA UTUMISHI SERIKALINI KUANZIA JULY, 2016 HADI KUFIKIA MARCH, 2017

WIZARA/TAASISI-	KUTHIBITISHWA KAZINI	NYONGEZA YA MUDA WA UTUMISHI	UAJIRI WA MKATABA	KUSTAAFU KWA MARADHI	KUSTAAFU KWA LAZIMA	KUSTAAFU KWA HIARI	LIKIZO BILA MALIPO YA	KUBADILISHWA KADA	KUACHA KAZI	KUFUKUZWA KAZI
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	315	1	1	4	274	10	1	3	3	2
Wizara ya Fedha	-	1	-	-	-	2	-	1	1	1
Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo	21	-	3	1	30	-	-	-	-	-
Wizara ya Afya	-	6	3	1	83	1	1	1	3	1
Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, U/Umma na Utawala Bora	12	-	1	-	-	-	-	2	-	-
Wizara Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi	18	1	-	-	117	5	2	-	-	-
Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Mwenyekiti wa BLM	-	1	1	-	1	-	-	3	-	-
Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira	23	1	1	-	3	3	-	1	-	2
Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais	25	-	-	-	5	1	-	5	1	-
Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji	-	-	2	-	47	6	-	4	-	-
Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko	6	1	-	-	-	-	-	-	-	1
Tume ya Kurekebisha Sheria	2	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu	-	1	-	-	-	-	-	-	-	-
Chuo cha Utawala wa Umma (IPA)	-	-	-	-	1	-	-	-	-	-
Baraza la Manispaa	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Mamlaka ya Mafunzo ya Amali	-	-		-	-	-	-	-	-	-
Kamisheni ya Utalii	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Kamisheni ya Utumishi wa Umma	1	-	-	-	-	-	-	1	-	-
Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi	2	-	-	-	-	1	-	-	-	-

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto	2	1	-	-	1	-	-	-	1	-
Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Mamlaka ya Usafiri Baharini	-	-	-	-	2	-	-	-	-	-
Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Tume ya Mipango	7	-	2	-	-	-	-	-	-	-
Tume ya Uchaguzi	-	1	-	-	1	-	-	-	-	-
Tume ya Utumishi Serikalini	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Shirika la Huduma za Maktaba	6	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja	13	-	-	-	-	-	-	4	-	-
Afisi ya Mwanasheria Mkuu	6	-	-	-	2	-	-	-	-	-
Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba	2	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Shirika la Bima	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Shirika la Bandari	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Shirika la Meli	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	-	-	-	1	5	-	-	-	-	-
ZSTC	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Tume ya Ukimwi	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ	7	-	-	2	5	1	-	3	-	-
SUZA	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho	-	-	-	-	-	-	-	1	-	-
Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa kiuchumi	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
ZIPA	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
ZBC	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
JUMLA KUU	**477**	**15**	**14**	**9**	**577**	**31**	**4**	**29**	**9**	**2**

WATUMISHI WALIOAJIRIWA KUANZIA JULY, 2016 HADI KUFIKIA MARCH, 2017

	WIZARA / TAASISI	**JUMLA**
1	Wizara ya Afya	26
2	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	260
3	Mamlaka ya Kuzuia Rushwa	22
4	Ofisi ya Raisi, Tawala za Mikoa na Vikosi maalum vya SMZ	11
5	Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto	7
6	Jeshi la Kujenga Uchumi	22
JUMLA		**348**

MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

FUNGU/IDARA	KAZI ZA KAWAIDA					KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	UNGUJA	PEMBA	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO
GO2 Mahkama	6,096,601,200	4,761,601,200	1,335,000,000			900,000,000		900,000,000
G03 Ofisi ya M/Mkuu	1,646,109,000	752,509,000	893,600,000					-
G04 Ofisi ya M/Mashtaka	2,273,500,000	1,378,500,000	895,000,000					-
G05 Tume ya K/Sheria	584,400,000	233,200,000	351,200,000					-
G06 Mdhibiti na Mkaguzi wa hesabu	2,627,200,000	1,389,200,000	1,238,000,000					-
G07 Mamlaka ya Kuzuwia Rusha	1,334,700,000	754,000,000	580,700,000					-
G08 Kamisheni ya Utumishi wa Umma	940,300,000	390,600,000	549,700,000					-
G09 Tume ya Utumishi Serikalini	511,800,000	191,000,000	320,800,000					-
G01 Idara ya Uendeshaji na Utumishi	1,588,805,700	978,805,700	610,000,000					-
G01 Ofisi kuu Pemba	1,020,819,860	850,819,860	170,000,000					-

G01 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	370,314,820	249,914,820	120,400,000			50,000,000	1,025,382,000	1,075,382,000
G01 Ofisi ya Mufti	500,455,260	308,455,260	192,000,000	142,000,000	50,000,000			-
G01 Idara ya Utawala Bora	233,806,720	133,806,720	100,000,000					-
G01 Idara ya E Government	608,144,200	283,144,200	325,000,000			50,000,000	10,000,000,000	10,050,000,000
G01 Idara ya Mipango ya Raslimali Watu	273,092,040	180,092,040	93,000,000					-
G01 Idara ya Miundo ya Taasisi	349,216,480	234,216,480	115,000,000					-
G01 Idara ya Nyaraka	524,677,000	331,677,000	193,000,000					-
G01 Ruzuku Chuo cha Utawala	604,500,000	567,700,000	36,800,000					-
G01 Ruzuku Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	825,800,000	577,400,000	248,400,000					-

G01 Ruzuku Afisi ya Hakimiliki	260,000,000	100,000,000	160,000,000					-
G01 Ruzuku DPP	55,600,000		55,600,000					-
G01 Tume ya Maadili ya Viongozi	579,267,920	79,267,920	500,000,000					
jumla kuu ya Ruzuku G01	**2,190,300,000**	**1,245,100,000**	**945,200,000**					
Jumla kuu ya Ruzuku	**2,245,900,000**	**2,245,900,000**	**1,000,800,000**					
Vote G01	**5,548,600,000**	**3,630,200,000**	**1,918,400,000**	**142,000,000**	**50,000,000**	**100,000,000**	**11,025,382,000**	**11,125,382,000**
Jumla G01&Ruzuku G01	**7,738,900,000**	**4,875,300,000**	**2,863,600,000**	**142,000,000**	**50,000,000**	**100,000,000**	**11,025,382,000**	**11,125,382,000**
Vote G02 -G09	**16,014,610,200**	**9,850,610,200**	**6,164,000,000**			**900,000,000**		**900,000,000**
Jumla kuu	**23,753,510,200**	**14,725,910,200**	**9,027,600,000**	**142,000,000**	**50,000,000**	**1,000,000,000**	**11,025,382,000**	**12,025,382,000**

KESI MAHAKAMANI

MAHKAMA	**Idadi ya kesi zilizofunguliwa za zamani**	**Idadi ya kesi zilizofunguliwa mwaka 2017**	**Jumla**	**Idadi ya kesi zilizotolewa maamuzi**	**Idadi ya kes zinazoendelea**	**JUMLA**
Mahkama ya Rufaa	20	9	**29**	20	9	**29**
Mahkama Kuu	173	188	**361**	19	342	**361**
Mahkama ya kazi	12	18	**30**	6	24	**30**
Mahkama ya Watoto	12	43	**55**	16	39	**55**
Mahkama ya Mkoa	158	288	**446**	75	371	**446**
Mahkama ya Wilaya	2112	1080	**3192**	2154	1038	**3192**
Mahkama ya Mwanzo	6282	4129	**10411**	9534	877	**10411**
Mahkama ya kadhi ya Rufaa	34	35	**69**	34	35	**69**
Mahkama ya kadhi ya Wilaya	1057	1145	**2202**	737	1465	**2202**
JUMLA	**9860**	**6935**	**16795**	**12595**	**4200**	**16795**

MISWADA YA SHERIA ILIYO TAARISHWA

NAM	MSWADA
1	Mswaada wa Sheria ya marekebisho ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya 2016
2	Msaada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar
3	Mswaada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali
4	Mswaada wa sheria ya marekebisho ya Kumi na moja ya katiba ya Zanzibar ya 1984
5	Mswaada wa sheria ya kufuta sheria ya Nembona sheria ya Benndera na kutunga sheria mpya
6	Mswaada wa sheria ya kurekebisha sheria ya Maadili ya Vionozi wa Umma
7	Mswaada wa sheria ya Marekebisho ya sheria ya Chakula dawa na Vipodozi
8	Mswaada wa sheria ya kufuta na kueka upya sheria ya Manunuzi

KANUNI ZILIZO TAARISHWA

Nam	KANUNI
1	Tobaco Control Regulation, 2016
2	The Urban Municipal Council Outdoor Advertising Control Regulations, 2016
3	The Trade Transaction Regulations of 2016
4	The Verified Gross Mass of a Containers Carrying Cargo Regulations, 2016
5	Kanuniza Malipo ya Ufunguaji Madai, Mahakama ya Ardhi, za 2016
6	The Urban Municipal Council Outdoor Advertising Control Regulations, 2016
7	The Petroleum supply Regulations,2017
8	The Petroleum (bulk Procurement) Regulations,2017
9	Zanzibar Broadcasting Regulations,2017

MAKADIRIO YA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018				
JINA LA MRADI	**MCHANGO WA SERIKALI**	**MCHANGO WA WAHISANI**	**MHISANI**	**JUMLA KUU**
Programu ya Mabadiliko ya Sekta ya Sheria	50,000,000	1,025,382,000	UNDP	1,075,382,000
Mradi wa Serikali Mtandao	50,000,000	10,000,000,000	Exem Bank of china	10,050,000,000
Programu ya Mabadiliko ya Sekta ya Sheria	900,000,000			900,000,000
JUMLA KUU	**1,000,000,000**	**11,025,382,000**		**12,025,382,000**

MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

IDARA/TAASISI	**MAKADIRIO 2016/2017**	**MAKUSANYO HALISI**	**%**	**MAKADIRIO 2017/2018**
G01 KAMISHENI YA WAKFU	85,604,000	53,303,929	62	130,084,000
G02 MAHKAMA	301,776,000	281,446,320	93	500,000,000
G06 OFISI YA CAG	65,864,000	8,000,000	12	84,555,000
JUMLA KUU	**453,244,000**	**342,750,249**	**76**	**714,639,000**

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa kwa uwakilishaji wako kwa hotuba sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria kuwasilisha hotuba yake.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: (Kny.Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum) Kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria naomba kuwasilisha hutuba ya maoni ya Kamati ya Kudumu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutumia fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma, muumba mbingu na ardhi pamoja vilivyomo kwa kutujaalia afya njema, kutupa pumzi na uhai kwani hii ni rehma kubwa aliyotujaalia ambayo wengine amewanyima. Pia napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa niaba ya kamati kwa lengo la kutoa maoni ya Kamati Ya Sheria, Utawala Bora Na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha, 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii pia kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Mwalim Haroun Ali Suleiman kwa ushirikiano wake mkubwa anao utoa kwa kamati ambao unapelekea ufanisi katika kutekeleza majukumu yake, na Naibu waziri Mheshimiwa Khamis Juma Mwalim kwa kuwa bega kwa bega na Kamati hii. Lakini pia, shukrani za dhati zimuendee, Katibu Mkuu wake ndugu Yakout Hassan Yakout, Naibu Katibu Mkuu ndugu Kubingwa Mashaka Simba na Seif Shaaban Mwinyi. Aidha, shukrani za pekee zielekee kwa Afisa Mdhamin Pemba, ndugu Masoud Ali Mohammed pamoja na watendaji wote wa Ofisi yake kwa kushirikiana nasi katika kazi zote za kamati ikiwemo na hii ya kuipitia Bajeti ya Wizara yao.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni Wizara muhimu ambayo inajumuisha taasisi muhimu za nchi, ambazo zipo kwa ajili ya kuwatumikia wananchi, kutoa haki kwa wananchi na kuisaidia Serikali katika uendeshaji bora wa nchi. Hivyo, ni busara zaidi Serikali ikaitizama Wizara hii kwa umuhimu wake ili kuipatia vitendea kazi pamoja na fedha za kuendeshea majukumu yake wanayojipangia. Kamati yangu inawatakia kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa hekma na uadilifu kwa

yale waliojipangia kuyatekeleza katika bajeti hii ya mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, napenda kutoa pole kwa wananchi wote walioathirika na mvua za masika zinazoendelea ambapo baadhi ya maeneo ndani ya Zanzibar Unguja na Pemba yamepata athari hizo pamoja na kupoteza maisha ya wananchi wawili, kwa niaba ya kamati tunatoa mkono wa pole kwa waathirika wote, kwa mtihani huu na Mwenyezi Mungu inshaallah atawajaalia subra na kheri katika kipindi chote cha kukabiliana na mtihani huu, kwani Allah (S.W.) ndie muweza wa kila jambo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza kutoa maoni ya Kamati, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa kamati hii kwa uwezo na umahiri mkubwa wa kuchambua na kuelewa majukumu yao ya uongozi katika kipindi chote cha kufatilia bajeti za Wizara hii pamoja na kazi kubwa waliyoifanya ya kupitia, kuchambua na hatimae kuipitisha bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa niaba ya kamati yangu napenda kuwatambua Wajumbe waliounda kamati hii kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
4. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	Mjumbe
5. Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
6. Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf	Mjumbe
7. Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo)	Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni	Katibu
9. Ndg. Ali Alawy Ali	Katibu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo kwa ruhsa yako na kwa mujibu wa kanuni ya 96 (1) na 106(3) katika jadweli la Kwanza la kanuni za Baraza la Wawakilishi ya Toleo la mwaka 2016 sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi kuhusu bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

OFISI YA RAIS – KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Mhe. Mwenyekiti, Napenda kuipongeza Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa jitihada kubwa wanazozifanya katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku, kwani jitihada zimekua zikionekana kuwasaidia wananchi na Serikali kupitia huduma mbali mbali wanazozitoa kutoka idara na taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Kamati inawaomba kuendelea na moyo wa kuwatumikia wananchi na kujenga Nchi kwa faida ya Nchi na vizazi vijavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kimuundo ina jumla ya Taasisi 22 zikiwemo Idara 8 zilizo chini ya Wizara moja kwa moja na Taasisi 14 zinazojitegemea, zilizo chini ya Wizara hii kupitia mfumo wa utekelezaji wa Bajeti wa PBB *(Program Based Budget).*

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum inaipongeza Wizara kwa vipaumbele walivyoweka kwa mwaka wa fedha ujao 2017/2018 ikiwemo :-

i. Ujenzi wa jengo la Mahkama Kuu Tunguu.
ii. Kuratibu Mradi wa Huduma za Serikali Mtandao awamu ya pili yaani *(e-health na e-Tax).*
iii. Kuimarisha misingi ya Utawala Bora.
iv. Kuimarisha Utumishi wa Umma na Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inasisitiza kufanyiwa kazi vipaumbele vilivyowekwa kwa mwaka wa fedha ujao, ili lengo lililokusudiwa kufikiwa. Lakini zaidi kamati inasisitiza kuchukuliwa hatua za haraka katika kuimarisha Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kwani idara hii hadi sasa ina changamoto kubwa ya ukosefu wa vifaa vinavyotumika katika kuhifadhia Nyaraka. Kitu ambacho kinakwaza utekelezaji wa kazi hizo na kupelekea ile dhana nzima iliyokusudiwa kutofikiwa ikiwemo ya kuhifadhi historia ya Nchi pamoja na Nyaraka muhimu za Serikali kwa faida ya Nchi pamoja na vizazi vijavyo.

Mhe. Mwenyekiti, pia, katika kipaumbele cha Ujenzi wa Mahkama Kuu Tunguu kamati inashauri kujengwa kwa jengo la kisasa la Mahkama ambalo litaendana na mabadiliko ya mahitaji, kwani tutakua tumepiga hatua kubwa na

kupanua Utawala wa Sheria, lakini pia, Kamati yangu inashauri kuchukuliwa hatua za makusudi kufanyiwa ukarabati na baadhi kujengwa upya kwa Mahkama zilizopo Unguja na Pemba kwani zipo ambazo haziridhishi hata kidogo kutokana na uchakavu, ubovu na ufinyu wa maeneo ya kufanyia kazi. Hali ambayo kamati yangu imesikitishwa sana na baada ya kuona changamoto hizo wakati ikiwa katika kazi za kamati, hivyo tunashauri Mahkama zote hizi zinahitaji kupewa kipaumbele kwa kufanyiwa ukarabati ili ziwe katika hali nzuri na inayoridhisha katika mazingira ya kazi wakati tukisubiria jengo la Mahkama kuu likijengwa.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa Mahkama hizo ni Mahkama ya Mfenesini, Mahkama ya Mwanakwerekwe, Mahkama ya Mahonda kwa upande wa Unguja na kwa Upande wa Pemba Mahkama ya Wete na Mahkama ya Mkoani. Tunajua fedha zinazotengwa kuendeshea Mahkama hizi hazitoshelezi lakini kamati inaishauri Serikali kufanya jitihada za makusudi kuzifanyia matengenezo Mahkama zetu kwani haziridhishi kwa hali ilivyo sasa.

AFISI YA AFISA MDHAMINI PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaishukuru sana Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba kwa kutekeleza jukumu la kuratibu kazi za Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa upande wa Pemba. Mbali na jukumu hilo Afisi ya Afisa Mdhamini Pemba inakabiliwa na tatizo la uchakavu wa jengo la ofisi pamoja na uhaba wa vyombo vya usafiri kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi hii. Aidha, Kamati inashauri kwa Ofisi kuu Unguja kuendeleza mashirikiano yao na Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba kwa kuishauri, kuiongoza na kuwapatia kila namna ya maelekezo ili kuweza kuboresha utekelzaji wa majukumu yao ya kila siku.

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa tunapenda kutoa shukurani za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kukamilisha ahadi yake aliyoitoa kwa wananchi wa Zanzibar ya ongezeko la mshahara kuanzia kipindi cha April 2017 wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Tunamuombea kila la kheri katika uongozi wake mahiri wa kuiongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Pili, Kamati inaishukuru Tume ya Utumishi Serikalini kwa kuendelea kutekeleza shughuli za uajiri Serikalini kwa watumishi wa Umma, kusikiliza malalamiko ya watumishi, kuidhinisha ajira za mkataba, kuthibitisha kazi, kubadilisha kada nakadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, Kamati kupitia Tume ya Utumishi Serikalini kwa mwaka wa fedha ujao, inawashauri vijana wa Kizanzibari wenye sifa zinazohitajika kuomba nafasi katika ajira za Muungano, pindi zinapotokea nafasi hizo za ajira kila mwaka kwa Wizara za Muungano, kwani Kamati imegundua kuwa bado kuna muamko mdogo sana kwa Wazanzibari kutumia fursa hiyo ambayo hutolewa kila mwaka kwa asilimia 21% ya nafasi hizo kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, Kamati inaiomba Serikali kuwapatia ofisi Tume ya Utumishi Serikalini kwa mwaka wa fedha ujao, kutokana na sehemu wanayotumia sasa ni kuwa ndogo, chakavu na isiyokidhi mahitaji ya wafanyakazi wao, hairidhishi na mbovu, hali ambayo inawalazimu baadhi yao kukaa watumishi wengi ndani ya ofisi moja. Kamati inasisitiza kupatiwa Ofisi yao Makamishna wa Tume ya Utumishi Serikalini, kwa kuwa hadi sasa hawana ofisi na wanategemea ofisi hiyo hiyo ya Tume ambayo ni ndogo kulingana na majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, suala la usafiri kwa Tume ya Utumishi nalo ni changamoto hadi sasa, kitu ambacho kinakwaza utekelezaji wa kazi zao. Hivyo basi, kamati inaishauri serikali kuwapatia japo gari moja kwa kuanzia na bajeti hii, ili waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi na kuondokana na usumbufu uliopo sasa. Aidha, suala la usafiri si changamoto ya Tume tu bali na Makamishna wa Tume nao hawana usafiri na wanakwazika katika kutekeleza majukumu yao.

OFISI YA MUFTI

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Ofisi ya Mufti Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yake. Kamati inaitaka wizara ndani ya mwaka huu wa fedha ihakikishe inachukua jitihada za kushughulikia suala zima la kupatiwa voti yake Ofisi ya Mufti ili kuondokana na changamoto iliyopo katika utekelezaji wa kazi zake kwa kutokua na voti. Lakini pia ndani ya bajeti hii kamati yangu inaisisitiza wizara kulifanyia haraka suala la kuajiriwa wafanyakazi katika kitengo cha Fat-wa kwa Unguja na Pemba, kwani kitengo hicho kwa muda sasa kimekua na uhaba wa wafanyakazi na kusababisha usumbufu katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, aidha kamati yangu inaisisitiza Ofisi ya Mufti katika masuala ya usafirishaji wa Mahujaji ihakikishe kila jumuiya ya usafirishaji inakamilisha taratibu zake mapema na kutolewa taarifa zao kwenye vyombo vya habari ili wananchi wapate kujua jumuiya inayoruhusiwa na isiyoruhusiwa

kusafirisha Mahujaji kwa lengo la kuepuka changamoto zinazojitokeza kwa Mahujaji. Baada ya kusikia taarifa juu ya kuzuiliwa kusafiri Mahujaji kutoka Tanzania kwa kushindwa kulipa deni.

OFISI YA MWANASHERIA MKUU

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutekeleza programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria, yenye lengo la kuishauri serikali katika masuala ya kisheria, ikiwemo kuandaa mikataba ya Kitaifa na Kimataifa, kutayarisha Miswada ya Sheria, kusimamia mashauri kwa niaba ya serikali na kuandaa hati na nyaraka za kisheria.

Kamati inashauri kwa mwaka wa fedha ujao Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ijitahidi katika kutekeleza programu zake kwa ufanisi zaidi, ili zile changamoto ndogo ndogo zinazojitokeza ziweze kuepukwa. Aidha, kamati inashauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha ujao kufanya jitihada za makusudi za kuanzisha ofisi yake Kisiwani Pemba, ili kuwasaidia wananchi na Taasisi za Serikali kuepuka usumbufu wa kufatilia huduma katika ofisi kuu Unguja.

OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni moja kati ya ofisi nyeti ndani ya Wizara ya Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma ambayo ina jukumu la kuhakikisha inaendesha na kusimamia kesi za jinai. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ili kuweza kukamilisha vyema kazi zake kamati yangu inaiomba serikali kuipatia Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ruhusa ya kuajiri kwani wana uhaba mkubwa wa Waendesha Mashtaka, kupatiwa usafiri hasa Pemba, pamoja na kupatiwa ofisi kwa upande wa Pemba kwani hadi sasa wana changamoto ya ofisi hali ambayo inagharimu pesa nyingi za serikali kwa ajili ya kulipa kodi.

MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaipongeza wizara kwa kuiongezea bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, bajeti ambayo itasaidia katika uendeshaji wa Mamlaka hiyo ijapokua bado inakabiliwa na changamoto ikiwemo ya vitendea kazi na usafiri. Kupitia bajeti hii kamati inashauri fedha zilizoengezwa kutumiwa vizuri ili kuweza kufikia malengo waliojipangia. Vile vile, kamati inaishauri wizara itenge bajeti kwa mwaka wa fedha ujao kujenga Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na

Uhujumu wa Uchumi kwa upande wa Pemba ili kupunguza gharama za kukodi Ofisi kama ilivyo sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla, Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inajitahidi kutekeleza majukumu yake ipasavyo, ijapokua kuna baadhi ya idara zina changamoto katika utekelezaji wake kutokana na ufinyu wa bajeti, ukosefu wa vitendea kazi, uhaba wa vyombo vya usafiri, upungufu wa ofisi. Zaidi ya hayo, uhaba wa baadhi ya taasisi zake kutoa elimu kwa jamii nao unakwaza kufikiwa kwa lengo lililokusudiwa ni wizara pamoja na serikali kwa ujumla. Hivyo basi, kamati inaitaka wizara kwa mwaka wa fedha ujao wa 2017/2018 kuweka jitihada zaidi katika kutekeleza majukumu yake ili manufaa yaliyokusudiwa yaweze kupatikana kwa serikali na nchi kwa ujumla. Sambamba na hayo, kamati inaiomba serikali iwapo hali ya fedha itaruhusu, iongezewe bajeti wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwani changamoto zote zilizopo haziwezi kutatuka bila ya kuwa na fedha za kutosha za kuendeshea shughuli zao.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inachukua nafasi hii kuliomba Baraza lako Tukufu kufanya juhudi za kuvipitia vifungu vyote vya fedha, vilivyoainishwa katika programu zote kuu na ndogo kwa kutoa michango na mapendekezo yao, ili kuiboresha na kuijenga bajeti hii iwe ni yenye kufanikiwa na kuleta maslahi kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Bajeti ya Wizara kwa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum katika Baraza lako Tukufu. Pia, niwashukuru wajumbe kwa kunisikiliza kwa utulivu wakati wa kuwasilisha hotuba hii, na ninawaomba waichambue, waichangie na hatimae waipitishe bajeti ya Tzs. 35,778,892,200/= (T/shilingi Bilioni thelathini na Tano, Milioni Mia Saba, Sabiini na Nane, Laki Nane, Elfu Tisiini na Mbili na Mia Mbili) kwa matumizi ya mwaka wa fedha 2017/2018 kwa Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya kamati yangu naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwasilishaji sasa naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali kuleta hotuba yake.

Mhe. Shaib Said Ali (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*PAC*): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako nnaomba kuwasilisha hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyenzi Mungu *Azza wa Jalla* kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wazima na wenye afya njema katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na wananchi wetu Kikatiba ya kujadili, kushauri na hatimae kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti**,** napenda kukushukuru wewe binafsi kwa niaba ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Baraza la Wawakilishi (*PAC*) kwa kuniruhusu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii pia, kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu na Watendaji wengine wa wizara hii pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mashirikiano yao ya dhati kwa kamati hii waliyotupa tulipofanya kazi za kuchambua na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii muhimu kwa maendeleo ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mkosefu wa fadhila nisipowashukuru Wajumbe na Sekretarieti ya Kamati ya *PAC* kwa busara zao na mashirikiano yao makubwa waliyotuonesha ambayo yameiwezesha kamati hii kuipitia na kuichambua bajeti ya ofisi hii na kutoa mapendekezo yake kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba sasa kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya *PAC* walioipitia bajeti hii kama ifuatavyo:

1. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Mwenyekiti.
2. Mhe. Shaib Said Ali - Makamo Mwenyekiti.
3. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi - Mjumbe
4. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mjumbe
5. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Mjumbe
6. Mhe. Salma Mussa Bilal - Mjumbe

7.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
8.	Ndg. Haji Khatib Haji	-	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa uzito wa majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kikatiba unapaswa uende sambamba na uzito wa bajeti inayopaswa kuingiziwa ofisi hii na serikali, ili malengo ya kuanzishwa kwa ofisi hii yaweze kufikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, ni matarajio yetu kuwa, uwepo wa ofisi hii ni chachu katika kuimarisha uwajibikaji, uwazi na kuweka nidhamu ya matumizi ya mali na fedha za umma. Kwani, serikali yoyote inayofuata misingi ya Sheria na Utawala Bora hulazimika kuonesha uaminifu na uadilifu wake kwa wananchi walioichagua.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba sasa niende moja kwa moja kwenye mjadala uliopo mbele yetu. Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya *PAC* imeridhika na utendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuthibitisha hili tumeshuhudia mnamo tarehe 12 Mei, 2017 Mhe. Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora amewasilisha Ripoti za Ukaguzi za mwaka 2014/2015. Mhe. Mwenyekiti, ripoti hizi ni miongoni mwa kazi kubwa iliyotekelezwa na ofisi hii katika kuimarisha Demokrasia na Utawala Bora Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine muhimu lililotekelezwa na Ofisi ya Mdhibiti ni kuwapatia mafunzo watendaji wake ili wazidi kutekeleza vyema majukumu yao. Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunaipongeza ofisi hii kwa kuzingatia suala la jinsia wakati inavyotekeleza majukumu yake. Hii ni kutokana na kuwa kati ya wafanyakazi 25 waliopatiwa mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 11 ni wanawake na wafanyakazi 14 ni wanaume.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya *PAC* ilifarajika na kauli iliyopewa na Watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya kuruhusiwa kuajiri watendaji wapya. Mhe. Mwenyekiti, maamuzi haya ya serikali ni muhimu kwa ofisi hii. Hii ni kutokana na kuwa jambo hili lilikuwa linasubiriwa kwa hamu kubwa kwani Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inahitaji wafanyakazi hususan wakaguzi wasiopungua hamsini (50). Mhe. Mwenyekiti, ni matarajio yetu kuwa watendaji hawa wataongeza ufanisi wa kazi katika ofisi hii pindi wakiajiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Mhe. Waziri kuwa, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ilikadiriwa kukusanya Tsh. 65,864,000 ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi, 2017, fedha zilizokusanywa ni Tsh 8,000,000 tu sawa na asilimia 12.1 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya *PAC* ilishtushwa na kauli hiyo, hata hivyo, ilielezwa kuwa makusanyo hayo yamekuwa madogo kwa kuwa baadhi ya Mashirika ambayo yamekaguliwa hayajajibu hoja zilizobainika ndani ya Taasisi zao. Hivyo, Ofisi ya Mdhibiti haijafanya Mkutano wa Kutokea "*Exit Meeting*" ambapo baada ya mkutano huo kufanyika ndio Ofisi ya Mdhibiti huzitaka taasisi hizo kulipa gharama ya ada ya ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo Watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti walizidi kuieleza kamati hii kuwa ingawa zoezi hilo halijafanyika hata hivyo, wanatarajia kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kukusanya jumla ya Tsh. 35,000,000 kiwango ambacho hakitafikia malengo yaliyopangwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ofisi hii haifanyi biashara, Kamati ya *PAC* inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kupitia idara yake inayohusiana na masuala ya Mapato kufanya utafiti juu ya chanzo hiki cha mapato cha Ofisi ya Mdhibiti ili ofisi hii iweze kukadiriwa kukusanya mapato kwa mujibu wa uwezo wa kianzio chake. Mhe. Mwenyekiti, ieleweke kuwa ingawa Ofisi ya Mdhibiti inafanya ukaguzi kwa Taasisi zote za Umma, hata hivyo sio taasisi zote zinazolipa ada ya ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya *PAC* inashauri hili kwa kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Mdhibiti imekadiriwa kukusanya Tsh. 84,555,000 wakati katika mwaka wa fedha 2016/2017 imekusanya Tsh. 8,000,000 ingawa inatarajia kukusanya Tsh. 35,000,000 kama tulivyoeleza hapo kabla.

Mhe. Mwenyekiti, kiwango cha mapato kilichokadiriwa kukusanya ofisi hii kwa mwaka fedha 2017/2018 ni kikubwa sana hasa ikilinganishwa kile cha mwaka wa fedha 2015/2016 ambapo ofisi hii ilikadiriwa kukusanya Tsh. 28,213,000 na ilifanikiwa kukusanya Tsh. 29,000,000.

Mhe. Mwenyekiti, wakati kamati ilipokuwa inajadili Bajeti ya Ofisi hii, imebaini kuwa katika Kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa 2017/2018 yapo baadhi ya maeneo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho na Wizara ya Fedha na Mipango, ili iende sambamba na uhalisia uliopo katika ofisi hii. Maeneo yenyewe ni kama ifuatavyo:-

Katika ukurasa wa G06 -6 unaohusiana na Idadi ya Watendaji Kazi na Makadirio kwenye Programu Ndogo ya Usimamizi na Uendeshaji wa Udhibiti na Ukaguzi - kifungu 98424 neno “Mrajis” lisomeke “Karani wa Masjala” kwa kuwa ofisi hii haina mtendaji mwenye cheo cha Mrajis.

Aidha, kwenye Programu Ndogo ya Udhibiti na Ukaguzi Pemba, kamati imependekeza katika Programu Ndogo hii ifanyiwe marekebisho katika maeneo manne kama ifuatavyo:-

(i) Kifungu 11215 maneno “Mkurugenzi Mkuu” yafutwe kwa kuwa hakuna cheo hicho katika ofisi husika.
(ii) Kifungu 41111 kisomeke kuwa “Karani Masjala” yupo “mmoja”.
(iii) Kifungu 96369 neno “Walinzi” lisomeke “Mhudumu” kwa kuwa tayari kifungu cha mlinzi kipo na kifungu cha mhudumu kimekosekana.
(iv) Kifungu 96372 maneno “Afisa Dawati” yafutwe kwa kuwa hakuna cheo hicho katika Afisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hayo, kamati yetu ilifanya marekebisho kwenye ukurasa wa G06 – 5 unaohusiana na Huduma Zinazotolewa na Taarifa za Utekelezaji kwa kupendekeza kuwekwa asilimia kwa Viashiria vya Matokeo kwenye Programu Ndogo ya Ukaguzi wa Fedha na Rasilimali za Umma. Hii ni kutokana na kuwa katika eneo hilo viashiria hivi havikuwekewa asilimia ya shabaha, jambo ambalo ilipaswa kuwekewa ili ofisi hii iweze kupima utendaji wa huduma wanazozitoa.

Mhe. Mwenyekiti, imekuwa ni kawaida sasa kwa Watendaji wa Taasisi za Umma kuieleza Kamati ya *PAC* kuwa Mkaguzi baada ya kumaliza ukaguzi wake huwa hafanyi Mkutano wa Kutokea na Watendaji husika wa Taasisi hizo. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kamati hii kuzisikiliza pande zote mbili zinazolalamikiana tumebaini kuwa Ofisi ya Mdhibiti huandaa ratiba maalumu kwa ajili ya shughuli ya ukaguzi. Hivyo, kutokana na ufinyu wa muda wakaguzi hao hupaswa kuifuata ratiba hiyo ipasavyo ili zoezi la ukaguzi liweze kufanyika katika kipindi kilichopangwa. Isipokuwa kwamba, tatizo linalojitokeza ni kuwa siku ambayo Mkaguzi amepanga kufanya Mkutano wa kutoka ni mara chache Viongozi Wakuu wa Taasisi husika kupatikana hususan Makatibu Wakuu, jambo ambalo linapelekea Mkaguzi kukutana na Watendaji wengine wa Taasisi hali ambayo huonekana kama kwamba mkutano huo haujafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, ili Mkaguzi aweze kutoa ripoti ambayo haitokuwa na malalamiko baina ya Mkaguzi na Mkaguliwa, Kamati ya *PAC* inawashauri Watendaji Wakuu wa Taasisi kutoa mashirikiano ya dhati kwa Mkaguzi ili aweze kutekeleza shughuli zake kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya *PAC* inalisisitiza hili kwa kuwa hivi sasa tupo ukingoni mwa mwaka wa fedha 2016/2017 na Mkaguzi Mkuu ndio kwanza amewasilisha Ripoti za Ukaguzi za mwaka 2014/2015. Hivyo, yuko nyuma miaka miwili kiukaguzi, kitendo ambacho kinawapa mzigo mkubwa watendaji, kwani ni mara chache kuwakuta watendaji waliotumia fedha ambazo zinakaguliwa katika mwaka wa fedha husika pamoja na kutokuwa na utunzaji mzuri wa kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati ya *PAC* imeyaridhia mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Hivyo basi, nawaomba na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wayapitie, wayajadili na hatimae wayapitishe makadirio hayo ili wazidi kutekeleza vyema majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie hotuba yangu hii kwa kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwa umakini wao wa kunisikiliza wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa kwa niaba ya Kamati ya *PAC* tunawapa pole wale waathiriwa wote waliopata majanga ya mvua na upepo mkali uliotokea, Mwenyezi Mungu awape uvumilivu na wawe na subra.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa kwa uwasilishaji wako naomba nitoe tangazo dogo hapa kuna wageni kwa ajili ya kusikiliza bajeti iliyopo mbele yetu. Ni wageni wa Mhe. Waziri Haroun Ali Suleiman ambao jumla yao ni 10 naomba niwataje.

1.	Sheikh Mohammed Kamilagwa	-	Mwenyekiti wa Kalam Foundation
2.	Balozi Kindamba	-	MakamuMwenyekiti
3.	Said Abdulla Azizi	-	Makamu Mwenyekiti
4.	Juma Nchia	-	Makamu Mwenyekiti
5.	Aisha Londu	-	Mkuu wa Utawala
6.	Fadhila Issa Abrahman	-	Mhasibu

7.	Ally Mohammed Haji	-	Meneja, Tawi la Zanzibar
8.	Dkt. Fauzi Abdulrazaq	-	Mjumbe wa Tawi la Zanzibar
9.	Amina Sijaona	-	Mjumbe
10.	Nasma Inado	-	Mjumbe
11.	Rehema Khamis	-	Mjumbe

Karibuni sana.

Sasa waheshimiwa tunaendelea na kuchangia hotuba hii wa wetu atakuwa ni Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf akifuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid na baadae atafuatiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: *Bismilahi Rahman Rahiim*. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia mimi nafasi ya kwanza, lakini pia nimpongeze langu la kwenye kamati Mhe. Wanu Hafidh Ameir, jembe makini ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa sijajua kama nitakuwa mtu wa mwanzo, lakini nitachangia yale ambayo niliyojitayarisha nayo nitaanza na kwenye suala la sheria. Kwa sababu nikisema tusome kitabu tuangalie itakuwa muda hautoshi na mambo mengi, lakini nitagusa mambo machache tu na hasa kwa sababu wizara hii sina shaka nayo sana kama wizara nyengine nitagusa vile vitu muhimu ambavyo nitataka kuzungumzia hii leo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la sheria bado nahisi kuna sheria nyengine ipo haja kabisa Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na tume ya kutunga sheria na sisi wenyewe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuwe tayari ili kuleta sheria ambazo zitakuwa zina meno na zitazoweza kuwafanya wale wavunjaji wa sheria na wenye mazonge kuogopa na kupata haki yao vizuri kabisa ya adhabu. Nazungumza hivi kwa sababu tumeona kuna mambo mengi sana ndani ya nchi yetu yale ambayo yanatokezea ya ubakaji, udhalilishaji, madawa ya kulevya, majambazi na hata wale mashoga wenye jinsia moja. Kwa kweli sheria hizi za hivi vitu vinne nilivyovitaja maana yake imefika hatua sasa hivi nchi yetu maadili yamepotea. Nchi yetu ilikuwa na ulinzi mzuri, usalama mzuri, lakini ukiangalia hivi vitu vimezidi, madawa ya kulevya sasa hivi ndani ya nchi yetu yamepita kiasi na nafikiri dunia nzima inatambua kwamba Zanzibar kwenye masuala ya madawa ya kulevya yamekuwa mengi sana na wametunga mpaka baadhi ya *video* na mambo mengine katika hii Televisheni ya *Al-jazeera* zinaonesha na nyenginezo kwamba Zanzibar imekuwa *effected* sana na mambo ya *drug*.

Sasa mimi naomba kumwambia Mhe. Waziri pamoja na Mwanasheria Mkuu kwamba waweke sheria wazikubali, tutapokuja kuzipendekeza au kutaka kuzileta sheria za hao watu ambao wauwaji, wabakaji, pamoja na wanaoleta madawa ya kulevya iwekwe sheria ya kunyongwa.

Mhe. Mwenyekiti, kama hatujaweka sheria hizi nzito ndani ya nchi hivi vitu vitakuwa havimaliziki wala havipungui, kwa sababu tunajuana Zanzibar, Tanzania au nchi za Afrika rushwa nyingi, muhali mwingi na ukiangalia mtu anaweza akaja akafungwa badala yake ikafanyika njia yoyote akaja akatolewa. Mtu atakamatwa na unga atapelekwa mahkamani, atafungwa, lakini baada ya miaka mitano au sita tu keshasahau atakuja kutolewa au utaambiwa kaumwa sana inabidi kalazwa sehemu fulani, kapelekwa mtu mwengine ni vitu vya udanganyifu. Lakini atapokamatwa mtu baada ya uchunguzi na ushahidi kamili keshahakikishwa kwamba huyu kabaka, huyu kaleta madawa ya kulevya, huyu jambazi basi anyongwe hilo suala litakuwa mzizi wa fitina ushakwisha. Lakini leo tukitaka kuleta hili suala au tunapolipendekeza suala hili Mhe. Mwanasheria Mkuu anapolisema kwenye *human rights* halipendezi, masuala ya *human rights* tuwaachie Wazungu wenyewe sisi Waswahili, Waafrika *human right* tuweke pembeni, tuweke sheria ambayo itaweza kukomesha hili suala ndani ya nchi yetu. Hizi *human rights* ndizo zinazoharibu watoto wa Zanzibar na wananchi wote kwa ujumla.

Mimi ningependelea sana tufuate *human rights* ambazo zina maadili mazuri, lakini *human rights* ambazo zinaletwa na hawa wenzetu nyengine hazina maadili mazuri na hizi ndizo tunawapa mikono na visu wazidi kuendeleza kufanya hivi vitu vya ubakaji.

Juzi kumetokezea kesi mtoto mdogo kabakwa sehemu zote mbili unazozijua wewe kafanyiwa na vitu vyengine, leo hii tusiombe Mwenyezi Mungu kabisa haya mambo yaje kutukuta sisi na watoto wetu na watoto wa wenzetu. Nafikiri sana mimi inafika hatua kwamba labda tunachukulia haya mambo mepesi kwa sababu hayajawahi kutukuta, lakini Mwenyezi Mungu atujaalie wale yanayowakuta yasiwakute na sisi yasitukute, lakini mambo haya ya kubakwa watoto, wanaoharibiwa kwenye masuala ya madawa ya kulevya, majambazi na hata mashoga na wenye jinsia moja wanyongwe tu nchi hii. Wapo maana yake mtu unaona kumewekwa mambo *too much* ndani ya Zanzibar, Zanzibar imekuwa inanuka kwenye masuala kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, leo Mhe. Mkuu wa Mkoa amefika anakamata mjini wameshakuwa na wao kama wanawake wanajiuza watu wenye jinsia moja. Kuna watu hapa tumeona ndani ya Zanzibar zimefanyika harusi kabisa za jinsia

moja, watu wanaowana Zanzibar mwanamke na mwanamke, mwanamme na mwanamme na wapo wanafugana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini kwa jitihada hii ya kukamata wale makahaba wanaojiuza, hawa watu wenye jinsia moja na nawaomba Wakuu wa Mikoa wote wafanye kazi hii wawafunge ikiwezekana hata wawauwe huko huko ndani jela.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumza suala hili kwa sababu nahisi Mhe. Mwanasheria Mkuu sheria hii tunapotaka kuipendekeza kama yeye hajawa tayari nayo, anafata mambo ya Kizungu. Mhe. Mwanasheria Mkuu tunamuomba sana sheria hii uje uipokee kwa mikono miwili *human rights* kwenye suala hili tuweke pembeni. Sheria nyengine Mhe. Mwanasheria Mkuu tutamuachia lakini sheria hii tunamuomba sana. Watoto wanadhalilishwa kila siku Zanzibar imekuwa inanuka kwenye kubakwa watoto, Zanzibar imekuwa inanuka kwenye masuala ya madawa ya kulevya, imekuwa inanuka kwenye masuala ya jinsia moja, *this is too much;* imeshafika wakati sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu akubali hii nchi imejaa Waisilamu asilimia 99.9. Sasa *human rights* nyengine sio nzuri lazima ifike wakati akubali tu kwenye sheria hizi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda kwenye Ofisi ya Mufti Mkuu. Ofisi ya Mufti Mkuu ina tatizo gani, kwanza mpaka leo *vote* yake haijapewa. Mufti Mkuu hana makuu anataka *vote* yake angalau awe na kifungu chake anajijua, lakini leo utakuta wizara inampangia anaambiwa apeleke bajeti yake, anatayarisha bajeti yake ya shilingi milioni mia moja, mia mbili matokeo yake anakuja kugaiwa shilingi milioni 30 hana cha kusema. Naomba sana, hivi leo mimi nitazuia kifungu chochote kwa suala la *vote* kwamba Mufti Mkuu apewe *vote* yake tufahamu kwamba imethaminika. Leo Zanzibar hii tuko sisi serikali sawa tutasema haina dini lakini ni uongo, serikali lazima iwe na dini kwa sababu sisi sote wengi wetu ni Waisilamu na hata kama kuna ndugu zetu wa Kikristo tunawapenda lakini tutizame *majority* iko vipi, *majority* ya nchi yetu ni Waisilamu kwa nini Mufti Mkuu adharauliwe. Maana yake kwamba hana *vote* ndani ya kitabu hiki maana yake kwamba Mufti Mkuu amedharauliwa.

Mimi naomba sana Mhe. Waziri akija kutujibu atoe sababu za msingi kuhusiana na suala la *vote,* lakini kifungu nasema kabisa kwa suala hili la dini yangu la Mufti Mkuu leo hakitopita. Nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa suala la dini kama hili wasikubali tukaachilia asipewe *vote,* kwa nini wasipewe wakati Mhe. Mufti Mkuu anapeleka vitu kwa niaba ya kutumia matumizi hapeleki vitu kwa matumizi yake mwenyewe.

Leo Pemba hii hapa bajeti yao wameomba safari hii shilingi 65,440,000 haya ndio makisio yao Ofisi ya Mufti Mkuu Pemba, na ya mwaka 2018/2019 wameshaweka bajeti yao mpaka mwaka 2020, lakini utakuja kushitukizia mara wanapewa shilingi 12 milioni. Hii yote inasababishwa kwa sababu *vote* yao hawana, kuna sababu zipi ambazo mpaka leo serikali wakati Mufti Mkuu keshaleta maombi mnazuwia *vote* ndani ya nchi hii. Mimi naomba sana, leo hapa kwa sababu nimekuja vizuri na nimesema mapema kwenye wizara hii sina mambo mengi ya kuya-*pressure* lakini kwa vitu hivi ninavyovizungumza pindipo tutakuwa hatujafahamiana lugha hakitopita kifungu kwa upande wangu. Naomba sana nije nijibiwe *vote* kwa nini hawajapewa hawawezi kufanya kazi zao vizuri na mtindo wa kumegewa megewa wakati hawajijui wamekaa nyumbani huko wanaambiwa tu mmetiliwa hiki sio vizuri lazima tuwaingize kama tulivyowaingiza wengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda kwenye suala jengine la Mahkama, Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na Polisi. Idara hizi lazima zishirikiane kwa pamoja ili kuhakikisha mambo yao yanakwenda vizuri, lakini kwenye ziara kila mmoja unapokwenda anamrushia mpira mwenzake na hili litasababisha kwamba kazi za nchi zisiende. Mimi ninachoomba sana kwenye wizara hii kwamba hizi sehemu tatu zishirikiane zifanye kazi kwa pamoja ziaminiane tukisema tunarushiana mpira tutakuta hatuipendi nchi yetu, hatuitengezi nchi yetu, tufike sehemu nzuri wakubaliane wafanye kazi vizuri basi nchi itaweza kwenda hata maamuzi yatakuwa mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nipongeze sana kwa Mahkama kwa kuzuia baadhi ya dhamana hasa kwa hawa watu wa madawa ya kulevya hivi karibuni wamezuwia. Mimi nawapongeza sana waendelee kuwazuwia hawa pamoja na mashoga na wanaoleta madawa ya kulevya wazuiliwe dhamana kama walivyokuwa wanafanya. Suala kama hili linaleta picha nzuri kuzuwia dhamana kwa watu kama hawa, kwa sababu hawa tumezungumza ni watu hatari, ni watu ambao wanaharibu nchi, leo ukiangalia sheria ndani ya nchi yetu zipo nzuri baadhi yao nyengine ndio kama hizi tunataka ziwe nzuri zaidi, lakini Mwanasheria Mkuu tunamuomba tena, mimi nampongeza sana kwanza kwa kuwa anawabeba sana *front benchers* kwa kuwatetea vizuri kabisa, nampongea anatumia uanasheria wake mkuu vizuri kwa kuwatetea, lakini na mambo mengine nayo ayatetee ya sheria kali asizipinge, wanaoleta *human right* si wenzetu mambo mengine lazima tuyapime.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia ile *human rights* si kunakuwa baadhi ya mambo inazidi kuharibu, sasa *human rights* hizo waachiwe wakae nazo wenyewe ndio maana sasa hivi utakuta hata hao mashoga wanawatambua, watu wanaowana,

ndio mfano wa Rais wa Zimbabwe aliyetoa mfano. Alisema kama unataka tulete hii sera ndani ya Zimbabwe basi njoo nikuowe wewe kwanza Obama halafu mimi nitaileta nchini kwangu, lakini Obama alikataa kuolewa. Sasa na sisi hizi sheria tukiziachilia wameshazipendekeza sana nchini Tanzania kwamba mashoga wathaminiwe, mashoga waachiliwe waolewe lakini huko tutakuwa hatufiki na hapa sisi tunawajua watu ambao wapo, utakuta wengine viongozi, ushanifahamu, nje mawizarani, sehemu tofauti wanashirikia mambo haya wamo mashoga, wamo wanaowana jinsia moja, wamo wanaoshughulikia masuala hayo na wanaya-*support*. Sasa tufikie hatua tuambizane ukweli ikibidi kama kuna sheria ya kuwataja baada ya kugundulika watajwe, maana yake mimi wengine nawajua kama nitaruhusiwa kuwataja nitawataja wala sioni tabu, lakini ukiangalia hatutaki kufika huko, hizi sheria nyepesi nyepesi tuziweke lakini tuweke na nzito kwa ajili ya watu wa kuwashughulikia kwenye masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaingia upande wa *CAG*. Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli hiki kitengo au idara hii ni nzito sana na ukiangalia mambo mengi ndani ya nchi hii yanaharibika, *value for money* haipo. Lakini cha ajabu zaidi kwamba unakuta vile vitu vya muhimu huvioni kwenye masuala ya kuchunguzwa, wenye mahesabu unakuta vitu ambavyo sio vizito sana, lakini pia si vypesi.

Mimi nitawapongeza Ofisi ya *CAG* kwa kuleta hii ripoti baadhi ya mambo pamoja na kutaja kwamba Shirika la *ZECO* limefanya manyago yake ambayo yameelezwa huku ndanu halijaridhishwa kabisa ni jambo zuri sana kuweka vitu wazi kama hivi. Lakini tuangalie mfano mdogo Kariakoo imejengwa karibuni mpya kwa mabilioni, lakini mvua ya juzi imejaa maji mpaka nusu mashine nyengine zimefunikwa, wakati Kariakoo ile kipindi cha nyuma kabla haijajengwa ilikuwa ikifurika maji na ikatengenezwa wakasema kwamba maji yatakuwa hayakai sasa hivi yamekaa vipi maji, inamaanisha kwamba, pale tayari kushafanyika madudu mainjinia waliotumika pale si wazuri na hapa ndio *CAG* anatakiwa akafanye kazi pesa zilizotumika pale ni zaidi ya shilingi bilioni kumi na tano, leo imekuja mvua ile kumejaa maji hakupitiki Kariakoo maji mpaka ndani kwenye mashine.

Tukiangalia suala la *airport* dola 128 milioni, 300 bilioni *airport* imefanyika uzembe wa watu wachache ambao wanaharibu serikali, wanaharibu na Chama cha Mapinduzi kinasemwa kwa upuuzi uliofanyika. Shilingi 300 bilioni karibu *airport* ile haijamaliza na mimi ripoti ninayo hii hapa imefeli na kufeli kwake malengo ya mwanzo yaliyotarajiwa sivyo yalivyo, ndio maana yake kufeli na fedha iliyotumika ni fedha nyingi sana. Kwanza ni katika *airport* ghali duniani

udogo ule ni ya Zanzibar, lakini *CAG* mpaka leo ripoti ya *airport* pia hatuioni wakati *airport* ipo zamani.

Kipindi cha nyuma aliomba shilingi 30 milioni kwa mujibu wa uchunguzi, aliomba kwa *Finance Ministry*, Waziri wa Fedha apatiwe pesa hizo akafanye uchunguzi matokeo yake kajibiwa kuna shilingi milioni tano sijui saba, maana yake kwamba asifanye ile kazi hawataki wafanye kazi kuna watu wanafichwa ndani. Sasa ifike hatua *CAG* apewe meno, *CAG* apewe ulinzi wa kutosha wapewe mshahara wa kutosha, wajaaliwe wafanya kazi zao, kuna mambo mengi yanaendelea hapa lakini *CAG* hawajapewa nafasi ya kutosha hawana uhuru wa kutosha, vitu vizito bado havijachunguzwa katika nchi hii vikatolewa ripoti kamili, vitu vilivyokuwemo humu kwenye vitabu vilivyokuja ni vitu vyepesi na karibu wizara zote zimeandikwa zimepewa usajili wa hati iliyoridhisha.

Mimi kwa ripoti hii sikubaliani nayo, lakini kwa alichokileta nakipongeza. Kwa sababu ukiangalia kama ripoti ya mawasiliano unaileta imekamilika wakati kuna *airport* imefanyika vurugu mechi kwa mawaziri waliopita na wizara iliyopita kabla ya hii mpya iliyokuja, kwa nini iseme imekamilika wakati kuna vitu vimefanyika vizito. *Airport* ile sasa hivi imekwenda kutafuta pesa nyengine nchini China, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kaenda huko tena kuzungumza na serikali zilete fedha nyengine imalizwe *airport, airport* ile waliosababisha matatizo yale watachukuliwa hatua gani? *Airport* kama ile itafeli vipi wakati ma-*engineer* tunaotakiwa tuwatumie n ma-*engineer* ni wale waliobobea na *airport* ndogo kama ile itafeli vipi kwenye masuala ya ujenzi? Leo unakuta hata haijamaliza zimeshatumika shilingi 300 bilioni.

Sasa hivi kuna suala la Kariakoo imejaa maji, kuna majumba yanayojengwa *value for money* hakuna, hivi vitu ifike wakati *CAG* apewe sheria kitachojengwa kikimaliza tu *CAG automatically* akachunguze tusingojee tuseme sisi Wawakilishi au kitu kina wasiwasi ndio akaambiwe akachunguze; vitu vyote vya nchi hii vyenye miradi mikubwa basi *CAG automatic* aingie kwenye lile suala la kuchunguza bila ya kuambiwa, ikiwezekana mwanzo au mwisho itapomaliza tu akafanye uchunguzi. Kwa sababu hivi vitu tumeshachoka watu wanaona, wananchi nchi wanaiona kwamba mambo yanaharibika, lakini leo unakuta watu wanafanya wanavyotaka katika nchi hii na hii ndio inayoharibu chama na serikali. Rais wetu mtu msafi tunasema siku zote na baadhi ya viongozi tunapozungumza kwenye wizara simaanishi mawaziri au manaibu waziri inawezekana labda yeye, inawezekana mtendaji wa chini au wa chini kabisa. Sasa tunatakiwa tuwe wasafi ili nchi iende, hii nchi ya wanyonge.

Mimi ningeomba sana *CAG* anapoleta ripoti alete zote, alete ripoti ndogo alete na kubwa na suala kama hili kama hayo masuala niliyoyataja kwa nini azuiliwe, kwa nini Waziri wa Fedha asitoe shilingi 30 milioni akafanya uchunguzi wa *airport* au kwa kuwa *airport* kuna watu wazio hawataki kutajwa walioharibu? Tunavyofahamu sisi mtu kama kaharibu *contractor* au *engineer* au kampuni imeharibu...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemaliza.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi naiunga mkono hoja asilimia 90, asilimia 10 naomba nije nijibiwe maswali yangu ndio labda nitai-*support.* Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, anayefuata ni Mhe. Omar Seif Abeid lakini kwa sababu simuoni machoni hapo atafuatia Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nami nishukuru kuniruhusu kuchangia hotuba hii na niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu Allah (*SW*) kwa kuniwezesha kusimama hapa ikiwa ni uwezo wake wala si ujanja wangu, wala mawazo yangu, wala fikra ni neema zake kubwa sana kwa pumzi alizoniazima.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu niendelee tena kumshukuru Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohamed Shein. Nazungumza haya Mhe. Mwenyekiti, ikiwa yanatoka ndani ya sakafu ya moyo wangu kwa kutokuingilia mihimili hasa ya Mahkama. Nasema tena saa moja na dakika moja hivi sasa ni Rais ambaye hajawahi kuingia katika mihimili hii, sijawahi kusikia kunako Baraza, sijawahi kusikia Mahkama na viongozi wengine wajaribu kufuata nyayo zake, lile ndio kimbilio la wanyonge. Umakini wake Dkt. Ali Mohamed Shein nitakuja kueleza kuna waziri mmoja huko mbele baadae.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nitakuwa sijamfanyia haki Mrajis wa Mahkama Kuu, Bwana George anaitwa. Kama kuna mtu anayefika kazini mapema katika maisha yangu kumuona mmoja ni huyu, msema kweli mpenzi wa Mungu; saa moja unakuta ofisi imeshafunguliwa chini pale. Bwana George sijui kama yupo mwenyewe Mrajis, lakini kuna msemo ule unaosema, misamiati hatukatazwi humu ndani "Mgema akisifiwa....", endelea na kazi hiyo. Sio hivyo tu, hata majukumu yake anasimamia vizuri, niendelee kuwaomba Mahakimu wote wa Unguja na Pemba, kusimamia haki za wananchi kwa uadilifu waendelee kusimamia haki hizi, hizi ni kimbilio la wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitagusia moja kwa moja Mahakama Kuu, moja kwa moja nitagusia Mahakama Kuu. Mhe. Waziri naomba hapa kidogo tusikilizane kwa makini kabisa huku ndani sote Wawakilishi tunapokea sawa sawa karibu pesa au mishahara na posho sawa sawa mbali na Wawaziri kidogo mmetuzi na Manaibu Waziri huko mbele lakini humu ndani tunapokea sawa. Leo ni sababu gani Waziri mnawalipa Mahakimu hawa kwa elimu yao sio haki, hii siyo haki, leo mnawalipa Mahakimu kutokana wenye *degree*, mwenye *master* hali tuelezane ndo uhalali huu, wewe Waziri mshahara unaopa haukutoshi unataka ukakope kwengine na sisi tunapata kuliko wao tuzungumze ukweli.

Hawa Sheria ya sikubaliana nayo kwa kuwa na elimu yake ana *degree* na *master*, wawakilishi sote tunalipwa sawa sawa ndani hakuna mdogo, hakuna mrefu, hakuna rangi hakuna hili lirekebishwe huu ndio ukweli. Lakini Mheshimiwa nipongeze mafanikio yaliyopatikana Mahkama ziendelee kufanyiwa ukarabati Mahakama ya Chake Chake, Mahakama Biashara Vuga, ukarabati uko vizuri na unaendelea, Mahakama ya Wilaya ya Mwanakwerekwe na hapa niombe Wizara ya Ardhi, kidogo sijui waziri yupo sijui kama hayupo lakini serikali ipo kwa pamoja, pana kiofisi kidogo pale Mahakama ya Ardhi inalaza mafaili yake kile kibanda wapeni hawa jamaa naomba nyie hamkitumii na kiko kitupu Waziri wa Ardhi kama yupo au ikiwa hayupo apelekewe salamu, pana ofisi yao wanalaza mafaili hawa wapeni hawa serikali inafanya kazi kwa pamoja mafaili hivyo hivyo wapate kutumia.Tatizo sugu la madeni na sisi ni mashahidi limekwisha kidogo limefanyiwa kazi, nishikuru na ipokeze serikali kwa hili imefanya kazi mashahidi wanatoka Bara wanakuja wanalipwa.

Jengine zaidi Wawakilishi tulikuwa tunapiga kelele humu ndani hivi sasa tukenda Kinua miguu kesi za uzalishaji watu waliokuwemo ndani sijui kama hawapungui sitini au arubaini, baada ya kazi kubwa tuliofanya Waheshimiwa sisi, nikupongezeni Mhe. Wawakilishi kwa dhati kabisa, hivi sasa tukenda Kinua miguu naamini watu kiasi ya sitini na arobaini wamo, Mahkama imefanya kazi baada ya kusimamia nawapongeze. Lakini bado katizo hili nalisimimia kwa mara ya pili au mara ya tatu kwa mwaka huu. Bajeti bado hairidhishi kabisa, tumeshuhudia Rais wa Tanzania John Magufuli aliongeza Mahakama fedha, leo bili ya umeme pale Vuga kwa mwezi milioni tano, sita itakwenda wapi.

Kuna Mahakama Mfenesini hali yake hairidhishi, Wete kamati imesema hapa na hizi ni ofisi muhimu, hizi ni kimbilio la wanyonge, wanyonge wanakwenda kutafuta haki huko yale yale. Mnyonge anamtuta Waziri gari ina- *tinted* hamuoni wakaja ofisini wiki tatu mnyonge hamuoni waziri, kiongozi mzuri ni yule anaewasikiliza wananchi, kwa Mahakama hizi niongezewe bajeti yake

kwa asilimia 100. *O.C* hizi haziwezi kujenga majengo haya ni matatizo, mishahara hii kwa elimu hii ni suala langu kubwa hawawezi kufanya kazi kuwa na *degree* ana *diploma* ana *master* ikiwa sisi Wawakilishi tuchukulie mfano tuangalie hili jambo mkafanyiwa mimi nitakubali, kwa nini nimfanyie mwenzangu.

Lakini jengine kubwa niwaombe vingozi, wanasiasa, tuwache tabia ya kuingilia Mahakama tunawanyima watu haki zao, leo mara jaji huyu kaitwa mara hakimu huyu kaitwa kuna hichi, tusijaribu kuingia tuwaache hebu ufuate nyayo za kiongozi wetu Dkt. Ali Mohamed Shein.

Haingilii Mahakama za viongozi wakuu baadhi huja kuna hili kuna hili tunafanya nini, mimi nikuombeni Mahakimu kama haikufika wakati tukaoneana haya hapa tutapata kazi tuondoshe uvivu, Sheria ifanye mkondo wake, Mahakama haiingiliwi, ikafika wakati naona kiongozi ana hatia, tuwabisheni bila ya kujali. Mheshimiwa tokea Baraza lililopita miaka mitano iliyopita, miaka mitano iliyopita ile nilipigia kelele kuhusu nyumba ya Jaji Mkuu, kuna sababu gani ya msingi mpaka serikali inashindwa kumjengea Jaji Mkuu nyumba. Leo Rais anaapishwa na Jaji Mkuu hadhi gani leo miaka mingapi kujenga nyumba ya Jaji Mkuu shilingi ngapi zinalipwa dola gapi za Jaji Mkuu kuna sababu gani ya msingi, kuwa asijengewe nyumba Jaji Mkuu.

Halafu kuna kitu chengine Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba Jaji Mkuu stahili zitoke katika Mfuko Mkuu wa Serikali, kuomba si kosa hadhi ya Jaji Mkuu ni kubwa nchi hii, Jaji Mkuu stahili zake zitoke kwenye Mfuko wa Serikali. Niliyaona juzi mie nipo pale kulikuwa na safari sijui kama alikwenda na kama kenda, kenda peke yake msaidizi pengine hakwenda ni kitu cha aibu tuangalie wenzetu tujifunze. Jaji Mkuu, Tanzania anavyo hadhi alindwa na *field force* leo Jaji Mkuu tumepata, hatari kubwa.

Mhe. Jaji Mkuu ni muhimili leo pesa hizi hizi, alizoingiziwa Mrajis ampangie safari Jaji Mkuu, atumie umeme, kalamu, karatasi ni hatari. Mheshimiwa niombe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu *A.G* nafikiri sijui utakuwa wa kumi na mbili sasa hivi au kumi tatu, katika *A.G* walofika kukaa nafasi hiyo. *A.G* Ofisi yako ningeiomba kabisa vyenginevyo serikali mtaitia hasara, kama hamkuwa makini jaribuni kuziangalia kesi na uzito wake pamoja kwamba mnasikitika nje, kesi mnapigwa Mahakamani hamjajipanga tafuteni njia nyengine zinazozungumzika, leo kuna kesi ya mchele wa Thailand mpaka leo hakimu anashindwa kutoa hukumu. Mengine hatuwezi kuyazungumza ndani humu kuhusu Meli tungepata muhadhara serikali tuwache nisije nikaja nikateleza zaidi ya hapa.

Kaangalieni mkataba wa Uwanja wa Ndege Serikali imeumia vipi, hii mikataba karibu ya Uganda, Tanzania, Kenya ndio ile *copy* and *paste* hebu tafuteni *standard* ya mikataba Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kazungumza shilingi ngapi zimepotea kwa mkataba pale.

Mkonga tuangalie serikali imepoteza kiasi gani, *CCTV camera* hii yenyewe, tuangalie suala la mikataba ni suala muhimu leo tunachukulia vyengine kwa *A.G* serikali itakuja kupoteza pesa nyingi kama hatutokuwa makini tutafute *standard* ya haya mambo na mliwahi kufanya semina na kuwapeleka watu *UNDP* mkawapa *train* sijui imekwendaje ile. Mikataba, Uwanja wa Ndege tumeshuhudia huo hapo, sijui kuna Bandari hiyo inataka kujengwa mikataba yake *A.G* lazima muisimamie kikamilifu vyenginevyo sisi kesi tu ke-*win* Uwanja wa ndege hii usimamizi jengeni uwezo. Mhe. niombe tena Jaji Mkuu, kama itawezekana wale Mahakimu wazuie kwenda pale Mahakama ya ardhi ni hatari. Serikali jambo likishatokea ndio baadae unakuja kujua athari yake. Jengo la Mahakama ya Ardhi haliridhishi liko chini ya Mahakama ya Ardhi lakini haliridhishi hata kidogo. Mhe. Mzee Ali Abdalla akipanda ile ngazi basi anafikiria tumelipigia kelele jambo likishakutokea aaa! wapi mtu msifu wakati yuko hai sio baada ya kwisha kuondoka ndio ukasema yule alikuwa ni mzuri.

Mimi ningeomba na kama hakufika ile watu wanakwenda pale kudai haki zao wanapigwa na mvua hapana hata pahali pa kukaa, choo, halikadhalika dirisha hulioni liko wapi, kitu cha kusikitisha sana. Akeshakuzuia Wizara ya Ardhi ina majengo mengi watatafuta pahali. Lakini pale wananchi wanyonge wanatoka Kiboje, wanatoka Makunduchi wanatoka Paje wanapigwa na mvua pale wakati kama huu wanakwenda kufata haki zao hairidhishi hali ile.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niwaombe sana Mahakimu hawa muwaangalie sio kwa elimu yao kuwalipa nasisitiza karibu mara tatu mara nne. Na niendelee tena kumshukuru Dr Ali Mohd Shein kwa umakini wake kwa kusimamia sheria hii. Nafikiri alitokea Wizara ya Katiba na Sheria anaujua umuhimu wake. Niwaombe wale Waziri au Naibu atakaepeleka fitina kule aangalie hizi sheria zinasemaje, huu muhimili wa Baraza hauungiliwi kama tutafanya makosa humu ndani tutaitwa.

Namshukuru sana Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein akasema mimi siwezi kuingia muhimili huu tuna Spika sisi kama tutafanya makosa tutaitwa na Kamati ya Maadili yeye kama nani "asirukie gari asieijua mwendo wake utakuja kumtoa meno", "akiona vinaelea vimeundwa", "funika kombe mawanaharamu apite" tunayajua mengi sisi humu ndani, asijaribu kurukia rukia mambo yeye akija kuambiwa atoe milioni hamsini kwenye Chama bila ya

Maandishi atatoa si atateleza miguu, toa shilingi milioni hamsini kwa ajili ya Chama hicho utateleza miguu. Sasa hii fitina ndogo ndogo za kazi gani hivi vyeo kesho havipo, hatuwezi kufika, fitina ngapi na umeshafanya mangapi, umetoka huku ukenda huku ukarukia wapi jui unafanya nini fitina kitu kibaya ni zaidi ya mtu kuliko alieua. Msingilie muhimili huu hizi ni starehe za kupita njia tu hizi kesho hazipo. Jaribu kukaa na watu maneno mazuri ni sadaka. Leo unataka kuingilia muhimu. Mwakilishi Mheshimiwa kafanya kosa kuna kamati ya maadili unaitwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nimshukuru Mhe. Dr Ali Shein kwa umakini wake niendelee kumshukuru bwana. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa michango yako anaefuatia Mhe. Hidaya Ali Makame kwa vile Mhe. Omar hajafika baadaye kama muda utaruhusu Mhe. Abdalla Ali Kombo.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa hii kuweza kuchangia maoni yangu kwenye hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kurudi tena kwa mara ya pili kwenye kikao hichi cha Baraza na kuendelea na michango yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanza moja kwa moja na mimi nianze kwenye suala la Mahakama. Mhe. Mwenyekiti, kwenye hotuba hii Mhe. Waziri katueleza lakini pia tumeona mambo mbali mbali ambayo yamefanyika. Lakini ningezungumzia pia kidogo kwenye suala la Mahakama, kuna Mahakama ambazo zimeoneshwa kwamba zitafanyiwa marekebisho na zimeoneshwa kwamba ni mbovu, lakini nimwambie Mhe. Waziri kwamba apite pite pia aikague ile Mahakama ya Mfenesini. Kwa kweli Mahakama ile inafanyakazi zake kila siku muda wote wa kazi. Lakini kwa kweli hali yake nayo hairidhishi haiko vizuri. Kwa hiyo, ningekuomba sana Mhe. Waziri ungepita na wewe angalau ukaiona kwa jicho la huruma basi japo rangi. Ila kwa sehemu zile za ndani kwa kweli Mahakama ile nayo iko hali si nzuri.

Kwa hiyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri katika marekebisho haya ambayo yatafanyika kwa hizi baadhi ya Mahakama basi na hii ya Mfenesini nayo itizamwe kwa jicho la huruma ili nayo iweze kupatiwa marekebisho katika kipindi hiki.

Mhe. Mwenyekiti, pia nije kwenye ukurasa wa 22 kuhusu suala la dini mambo ya Mufti na usimamizi wa hakimiliki. Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la usimamizi wa haki za mirathi nalo hili kwa kweli tuliangalie kwa hali ya umakini zaidi, kwa sababu tunaona kesi nyingi zipo na usimamizi unaendelea lakini sijui unafikia hatua gani katika maamuzi juu ya kuwapatia haki hawa watoto au hawa watu wanaokwenda kesi hizi ili kuweza kupata haki zao kwa usahihi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kesi hizi zipo nyingi na kwa kweli tunawaona jinsi watu wanavyodhalilika na kuhangaika juu ya kutafuta haki zao. Muda mwengine unawakuta wanaokwenda kwenye kesi hizi ni watoto wadogo ambao wanasimamiwa aidha na wazee wao wengine kwa kupoteza wazazi wao ili kupata zile haki zao za mirathi basi inakuwa hali ni ngumu kwa upande wao na unakuta manyanyaso makubwa. Lakini mwisho wa siku unakuta yule mtoto hata ile haki yake haipati. Kwa hiyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri juu ya suala hili akishirikiana na Ofisi yake ya Mufti ifanye kazi ipasavyo ili kuona hawa wananchi wanapata haki zao kwa urahisi zaidi, lakini pia kujenga akhera yao huko mbele ya haki wanapokwenda kwa sababu suala la usimamizi wa haki ya mtu ni suala kubwa si kwa binadamu tu bali hata kwa mwenyewe Allah Subhana Wataala.

Mhe. Mwenyekiti, pia ningekwenda kwenye suala jengine sehemu hiyo hiyo kuhusu usimamizi wa vyuo vya madrasa na misikiti. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri pia ametueleza kwamba walifanya ukaguzi wa kutembelea kwenye sehemu hizo za vyuo vya madrasa na misikiti, lakini kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, ipo haja ya kuweza kuisaidia Ofisi ya Mufti ili kuweza kuwapatia japo misaada midogo midogo ikiwemo ya mas-hafu na vijuzuu. Sitosema fedha kwa kweli suala hili nalo liangaliwe kwa sababu tunaona kwamba wadhamini wamo wengi, watu wanaojitolea wapo wengi lakini na ofisi nayo ingetia mkono wake ingeonekana kwamba kweli nayo inafanya kazi na inasimamia suala hili la vyuo vya madrasa. Na hata wale walimu wetu pia wangepata moyo kuona kweli ofisi yetu inatujali na inatutendea haki juu ya suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kukaa tukafikiri juu ya walimu wa madrasa lakini pia na wasimamizi wa misikiti wetu ambayo wanatusalisha na wanatusomesha kwa hali hii inapaswa kuwepo haja ya kuweza kuwaangalia hawa nao hata kama kwa mwaka siku moja. Ipo haja ya kuweza kuwasaidia walimu wetu wa madrasa wasipewe mishahara kwa sababu mshahara ni kitu kikubwa, lakini japo vile viposho vidogo vidogo japo miezi mitatu au miezi miwili kwa kweli ni suala la kuwekewa umakini zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, pia ningependa kulizungumzia suala la ajira kwenye Ofisi za Viongozi. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunaona msongamano na tunapata tabu sana kwenye suala hili endapo pale zinapotoka nafasi za ajira kwenye ofisi hizi, tunaona kwamba vijana wengi wanapeleka barua za maombi na kwa kweli wanajitahidi kufuata masharti na maelekezo yanayotokana na hizi kazi zinazotolewa. Matangazo tunayasikia redioni kweli, lakini kwa kweli kunakuwa kuna hali ngumu inayotokana na huu upatikanaji wa hizo ajira. Kwa sababu inaonekana kwamba yaani muhudumu anapotoa hili tangazo tayari labda kunakuwa kuna watu wake ambao keshawalenga kabisa mwenyewe, hawa watakapokuja watapata hizi ajira na hawa wengi watakuwa tu kama ni kuja kuleta kwa kuwa waonekane kwamba lile tangazo limetoka na wamelifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hapa napo naweza kusema udhalilishaji unapita, kwa sababu unakuta mtu anafuatilia mwisho anachoka na hajui nini afanye juu ya suala hili, na kila siku zinapotoka hizi nafasi za ajira yeye anakuwa ni mtu wa mwanzo kupeleka mabarua na kuhangaika huku na huku. Kwa kweli wengine wenyeji hatuna lakini kinachosaidia hapa ni ile kwamba mtu tayari lile tangazo keshalisikia na vile vigezo vilivyotajwa pale vyote anavyo na anaweza kuvifanyia kazi na akafaulu, lakini unamkuta mtu huyu bado anashindwa na anakaa mitaani.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningependa sana suala hili nalo ungelisimamia kwa umakini zaidi ili tukawaona vijana wetu hawa ambao wamefikia hivi viwango vya kupata hizi ajira na wao wapatiwe ili tu tuondokane na lile wimbi kubwa la vijana wetu kukosa ajira.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisingependa nizungumze mengi juu ya hotuba hii, lakini ningeiomba sana wizara ikaiangalia sana Ofisi ya Mufti juu ya usimamizi wake wote wa hizi kesi za ndoa, kesi za ndoa migogoro nayo ipo mingi sana kwa sababu tunasikia maredioni, lakini tunawasikia wananchi pia wanavyolalamika, lakini pia wanavyodhalilika juu ya ufuatiliaji wa haki zao kwenye masuala ya ndoa. Ndoa imeumbwa na Mwenyezi Mungu kama tulivyoumbwa sisi binadamu na haki zake na sheria zake zote zipo tunajua, japo kuwa wengine hayajatufika lakini tunayasikia, tunayaona. Kwa hivyo, kwa vile yapo na sheria zipo basi yafanyiwe utaratibu ili hizi sheria zifuatwe na kanuni zitumike, ili hawa watu wapate haki zao, wanapokwenda kwenye Mahakama za Ndoa mambo mengi wanakabiliana nayo na wanahangaika sana.

Mhe. Mwenyekiti, utamkuta mwanamke hana uwezo wa kufuatilia kesi yake ile, pengine huku jibaba limeshamtelekeza miaka hamjui hata alipo. Unamkuta

mwanamke yule ile kazi ya kwenda na kurudi mahakamani kila siku inamchosha, kwa hivyo unakuta mwanamke yule anadhalilika wakati haki yake ile ni rahisi kuweza labda kupata talaka au mafao yake mengine na kuweza kutafuta riziki yake upande mwengine.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri aiangalie sana kwa jicho la huruma na kwa jicho la pekee Ofisi ya Mufti. Kama kuna mafao yoyote ambayo yapo basi yapatikane. Lakini kama kuna usimamizi mkubwa zaidi ambao unapaswa kufanyika kwenye Ofisi ya Mufti, kwa sababu Ofisi ya Mufti tunaona kama ni jicho letu Waislamu. Kwa hivyo, ofisi hii inatuhusu sana na inatufanyia kazi zetu kwa urahisi zaidi, endapo nayo itajaaliwa au nayo itapewa haki zake kama tunazozihitaji sisi wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nikimalizia hapo mimi niseme tu naiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja. Lakini asijeacha kutoa maelezo juu ya hawa vijana au hawa watu wanaokwenda kudai haki zao za mirathi. Pia wanaokwenda kusimamia kesi zao za ndoa na talaka ili tujuwe je, ni hukumu au nini hatima ya watu hawa katika kusimamia kesi zao hizi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hidaya Ali. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo atakuwa Mhe. Abdalla Ali Kombo.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru. Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu naanzia na huu mfumo wa *electronic* wa taarifa za watumishi. Nasikitika sana na mfumo huu wa kisasa ambao tumepatiwa kompyuta 8 za kisasa, watumishi tumeambiwa wana *degree* za *master* na wengine 47 wamekwenda kwenye mafunzo. Lakini cha kusikitisha wafanyakazi hewa wao wanaongezeka, kila tukizidisha utaalamu huku kwenye utumishi wafanyakazi hewa nao wanaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, ningeiomba wizara hii itufahamishe kwa kina na kwa kisayansi mambo haya yanakuaje, kwamba kila tukiongeza *technology* wizi nao unaongezeka. Mhe. Mwenyekiti, la kwanza hilo. Hapa nataka maelezoya kina na ya kisayansi. *(Makofi)*

Jambo la pili Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba AG au Mwanasheria Mkuu anipe tafsiri ya shirika na Idara ya Serikali. Katika safari zetu za kamati, wakati huo tuko kwenye Kamati ya Mawasiliano na Uchukuzi, umeme maji uwanja wa ndege, tunakwenda tunaambiwa haya ni mashirika, lakini hayana tofauti kabisa na Idara za Serikali. Ninavyofahamu mimi shirika kiasi kwamba

asilimia 75 huwa angalau ina *authority* ya kumtafuta huyu *daily paid* kwamba akakate minazi au misufi. Sasa haya mashirika yakoje, au mashirika ya kwetu Zanzibar tafsiri yake iko tofauti na mashirika mengine.

Kwa hivyo, hii ni wizara ya sheria na Naibu Waziri ni mtu wa sheria anaweza akatutafsiria shirika na Idara hizi za Serikali zikoje. Hata wakitafuta chochote hawaruhusiwe mpaka wakutane na Idara ya Utumishi, watakuambia Idara ya Utumishi hakuna, sasa haya mashirika yakoje ambayo hayana maamuzi ya aina aina yoyote.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, sijui kuna vigezo gani vya kupanga mishahara hii, kuna malalamiko sina uhakika kama itakuwa sivyo basi Mhe. Waziri atanijibu sivyo, kwamba kuna wahasibu, maafisa mipango na maafisa utumishi, inaonekana wahasibu maafisa utumishi na maafisa mipango hata kama wana cheti kimoja. Hayo ni malalamiko sina uhakika, kama sivyo nitajibiwa sivyo. Hawa wengine mishahara inakuwa mikubwa kuliko hao maafisa mipango. Afisa Mipango Mhe. Mwenyekiti, sio mtu mdogo maana yake hata waziri tuliyekuwa naye hapa ni Waziri wa Fedha na Mipango, huwezi kuzichambua hizi pesa kama huna mipango, utumishi utasema tu una idadi ya watu wangapi. Kwa hivyo hili nalo naomba ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine wenzetu Bara sasa hivi wanahangaika na vyeti feki, kinachonikitisha kuna wafanyakazi wa serikali yetu ya Zanzibar nina wasi asi kama wana vyeti kwa utendaji mbovu uliokuwa hauna maana. Sasa nadhani imefika wakati na sisi tuwatizame kwenye serikali yetu. Ni muhimu tusije tukadhani mtu labda anafanya makusudi, kumbe hajui. Sasa nadhani imefika wakati hata sisi Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali upo, utumishi mpo hebu na sisi tufanyeni hii kazi. Sisemi kwamba watapata njaa au nini wengine. Mimi changu cha halali nina uhakika, lakini lazima kuwe na haja sasa hivi tutizameni, hii hali imekuwa sio nzuri. Kuna wafanyakazi nina wasiwasi wanafanya mambo haya hawakusudii hawana utaalamu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo nitatia na utamaduni msije mkashangaa. Mhe. Mwenyekiti, hii ni mara ya tatu tunazungumzia. Leo kidogo kidogo, tunazungumzia habari ya nyaraka. Leo sina maneno mengi wala sitowi shilingi, lakini kuna ngoma moja kule kwetu Mhe. Waziri anaijua inaitwa mdalanga, hiyo ngoma ni ya shetani, hupigwa ngoma wee, yule anayepungwa huwa hapandi shetani. *(Makofi)*

Sasa kuna mzee mmoja alikuwa anaitwa Zungu mpiga zumari, Mhe. Waziri pia anamjua. Sasa huitwa Zungu akapiga zumari yake masikioni, papapa!! kama

shetani hakupanda, basi utasikia 'huyo kana marogo sio shetani' *(Kicheko/Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nina wasiwasi hizi kelele zetu zote za nyaraka hapana kwa zumari hii haifai. Mbaya zaidi hata hii serikali ambayo iko huku, kuna ule mchezo wa kuigiza wa Yombayomba. Alivyokwenda kwa mganga akaambiwa kila kitu sema naona giza, naona giza. Sasa hata serikali huku ukisema tupige kura iwe sivyo, ita-*support* tu sivyo inaona giza. Sasa mimi nadhani tufike pahala, tusifike kwenye zumari ya Zungu wala tusifike kwenye mchezo wa Yombayomba, tuifikirie hii Zanzibar yetu kwamba ni aibu, tusigeuke mbuzi kutafuna kibanda chetu. Maana ikifika saa 9:00 mbuzi hujamfunga basi anatafuna kibanda, nadhani tumefahamiana. Mhe. Mwenyekiti, nimemaliza. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe kwa mchango wako. Kwa sababu ya muda, muda wetu uliobakia ni mchache kiasi ambacho hawezi kumaliza mjumbe. Naomba niwatangazie wajumbe ambao kesho tutaanza nao tukijaaliwa. Mhe. Abdalla Maulid Diwani, akifuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi, na baadae Mhe. Simai Mohammed tukijaaliwa hao ndio watakuwa wa kuanzia kesho asubuhi.

Kwa sababu muda uliobakia ni dakika chache, kwa hivyo naomba niahirishe kikao hiki hadi kesho saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:28 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 19/05/2017 saa 3:00 za asubuhi)